JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)

TAARIFA YA KAMATI KUHUSU RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2024 NA TAREHE 30 JUNI 2025

Imetolewa Chini ya Kanuni ya 139 (16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2025

NOVEMBA, 2026

DIBAJI

Taarifa hii imeandaliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa lengo la kuwasilisha mbele ya Bunge matokeo ya utekelezaji wa majukumu yake ya kikatiba na kisheria ya kusimamia uwajibikaji, uwazi na matumizi yenye tija ya rasilimali za umma. Katika kipindi kinachoripotiwa, Kamati ilichambua na kujadili taarifa za hesabu zilizokaguliwa za taasisi za umma kwa miaka ya fedha 2023/2024 na 2024/2025, kwa kuzingatia hoja zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya Kwanza inaeleza maelezo ya jumla, majukumu ya Kamati, njia zilizotumika kutekeleza kazi zake, matokeo ya utekelezaji, ufuatiliaji wa mapendekezo ya awali na vigezo vya uchambuzi. Sehemu ya Pili inawasilisha matokeo ya uchambuzi wa hoja katika maeneo makuu nane; udhibiti wa fedha za umma; ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba; udhibiti wa ndani; utendaji wa taasisi na thamani ya fedha; uzingatiaji wa sheria na kanuni; kaguzi za kiufundi; Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; na usimamizi wa mali za Serikali.

Sehemu ya Tatu inawasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu maeneo makuu yafuatayo: ufanisi wa ukusanyaji wa mapato; usimamizi wa mikataba na miradi ya Serikali; ufanisi wa kifedha na kiutendaji wa taasisi za umma; mifumo ya udhibiti wa ndani; usimamizi wa tozo na mapato; uzingatiaji wa viwango vya uhasibu; usimamizi wa mali za Serikali; pamoja na uboreshaji wa ukokotoaji wa mafao ya pensheni. Sehemu ya Nne inatoa

hitimisho na shukurani, huku randama ya mapendekezo ikiambatishwa ili kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wake.

Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilizingatia hoja za ukaguzi, maelezo na ufafanuzi wa menejimenti za taasisi husika, pamoja na hatua zilizochukuliwa au zilizopangwa kurekebisha mapungufu yaliyobainika. Matokeo ya uchambuzi huo yameiwezesha Kamati kubaini changamoto na kupendekeza hatua za kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma.

Kamati inaamini kuwa utekelezaji madhubuti wa mapendekezo haya utaimarisha uwazi na uwajibikaji, kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha za umma na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Hivyo, inaliomba Bunge kuzingatia taarifa hii na kutoa maelekezo stahiki kwa Serikali ili mapendekezo yatimizwe kwa wakati na utekelezaji wake ufuatiliwe kikamilifu kwa manufaa ya Taifa.

YALIYOMO

Ukurasa

YALIYOMO iii
ORODHA YA MAJEDWALI vii
ORODHA YA VIELELEZO viii
SEHEMU YA KWANZA 1
1.0 MAELEZO YA JUMLA 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 Muundo wa Taarifa 2
1.3 Majukumu ya Kamati 2
1.4 Njia Zilizotumika Katika Utekelezaji wa Kazi za Kamati 3
1.5 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati 6
1.6 Ufuatiliaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa na Kamati 9
1.7 Vigezo vya Uchambuzi 9
SEHEMU YA PILI 11
2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI 11
2.1 Uchambuzi wa Hoja za Udhibiti wa Fedha za Umma *(Financial Management Issues)* 11
2.1.1 Uchambuzi wa Hali ya Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) 12
2.1.2 Uchambuzi wa Taarifa ya CAG kuhusu Hoja za Ukaguzi Zinazoathiri Ufanisi wa Kifedha na Kiutendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) 29
2.1.3 Mapungufu Katika Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma Yaliyojitokeza Katika Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) 34
2.2 Uchambuzi wa Hoja za Ununuzi wa Umma na Usimamizi wa Mikataba *(Procurement and Contract Management Issues)* 40
2.2.1 Changamoto Katika Usimamizi wa Mradi wa Mabasi ya BRT Awamu ya II 41
2.2.2 Malipo ya Shilingi Milioni 523.15 Yaliyofanyika kwa Kazi za Ukarabati wa Barabara za Ndani ya Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu Mzumbe Zisizokidhi Viwango 44
2.2.3 Zabuni Zenye Thamani ya Shilingi Bilioni 1.54 na Shilingi Bilioni 29.7 Mtawalia Zilizotolewa kwa Wazabuni Wasiokidhi Baadhi ya Vigezo Vilivyotakiwa Katika Chuo Kikuu Mzumbe 47
2.2.4 Dosari Katika Ununuzi wa Pikipiki 700 za Chanjo ya Mifugo Uliofanyika Katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi 49

2.2.5 Mapungufu Katika Utekelezaji wa Mkataba wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Fungu - 68 54
2.2.6 Mapungufu Katika Usimamizi na Utekelezaji wa Mkataba wa Upangishaji wa Ardhi kati ya UDSM na Mlimani City Holding Limited (MHL) 57
2.3 Uchambuzi wa Hoja za Udhibiti wa Ndani *(Internal Control Issues)* 61
2.3.1 Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani Katika Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) 61
2.3.2 Uendeshaji wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF) Bila ya Kuwa na Muundo Rasmi wa Kiutendaji na Kiuwajibakaji 66
2.4 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi Zinazohusu Utendaji *(Performance/ Value for Money Issues)* 76
2.4.1 Uchambuzi Kuhusu Hali ya Kifedha na Utendaji wa Benki ya Kilimo Tanzania (TADB) 77
2.4.2 Changamoto Zinazoikabili Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama – Shinyanga (KASHWASA) 84
2.4.3 Uchambuzi wa Taarifa ya CAG Kuhusu Mafanikio, Changamoto na Hatua za Kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) 87
2.5 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi Zinazohusu Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni *(Compliance Issues)* 95
2.5.1 Ukusanyaji wa Mapato Yasiyotokana na Utalii Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) 96
2.5.2 Kutokuwepo Usahihi Katika Kubaini Malipo ya Mwaka Yanayostahili Pensheni (APE) Katika Mifuko ya PSSSF na NSSF 97
2.5.3 Usimamizi wa Mapato ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL) 99
2.5.4 Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS) 103
2.6 Uchambuzi wa Kaguzi za Kiufundi *(Technical Audit Reports)* 109
2.6.1 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ukarabati wa Viwanja va Benjamin Mkapa na Uhuru na Ujenzi wa Uwanja wa Arusha 110
2.7 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT Issues)* 118
2.7.1 Udhaifu katika Usimamizi na Usalama wa Mifumo ya TEHAMA katika TAFICO 119
2.7.2 Udhaifu katika Usalama wa Chumba cha Seva na Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA katika Wizara ya Kilimo — Fungu 43 119
2.7.3 Udhaifu katika Udhibiti na Uunganishaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Shirika la Bima la Taifa (NIC) 120

2.7.4 Kutokuwepo kwa Mfumo Jumuishi wa Kusimamia Miradi na Mikataba katika Kampuni ya Ujenzi ya Umeme (ETDCO) 120
2.7.5 Udhaifu katika Urejeshaji na Uunganishaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Idara ya Uhamiaji — Fungu 93 121
2.7.6 Udhaifu katika Usimamizi wa Makosa, Adhabu na Taarifa za Leseni katika Mifumo ya TEHAMA ya Tume ya Madini 121
2.8 Uchambuzi wa Hoja za Usimamizi wa Mali za Serikali (*Assets Management Issues*) 123
2.8.1 Taasisi Zisizokamilisha Urasimishaji wa Umiliki wa Ardhi 123
2.8.2 Kutokukamilika kwa Usajili wa Mali za Serikali Katika Mfumo wa GAMIS 126
SEHEMU YA TATU 130
3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO 130
3.1 Maelezo ya Jumla 130
3.2 Maoni 130
3.3 Mapendekezo 133
3.3.1 Kuhusu Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) 134
3.3.2 Kuhusu Usimamizi na Utekelezaji wa Mikataba ya BRT Awamu ya II 136
3.3.3 Kuhusu Changamoto za Usimamizi wa Ujenzi na Uboreshaji wa Miundombinu ya Viwanja vya Michezo 138
3.3.4 Kuhusu Ufanisi wa Kifedha na Kiutendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) 140
3.3.5 Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) 141
3.3.6 Kuhusu Usimamizi wa Mikataba na Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma 143
3.3.7 Kuhusu Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani Katika Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) 144
3.3.8 Kuhusu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF) 146
3.3.9 Kuhusu Usimamizi wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL) 147
3.3.10 Kuhusu Mkataba wa Upangishaji Ardhi Kati ya Chuo Kikuu Dar es Salaam na Mlimani City Holding Limited (MHL) 149
3.3.11 Kuhusu Mapungufu katika Usajili, Udhibiti na Usimamizi wa Mali za Serikali 150
3.3.12 Kuhusu Uzingatiaji wa Viwango vya IPSAS na IFRS katika Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Taasisi za Umma 151
3.3.13 Kuhusu Changamoto za Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA Katika Taasisi za Serikali 152

3.3.14 Kuhusu Utata wa Kisheria na Kiutendaji Katika Usimamizi wa Mapato Yasiyotokana na Utalii na Mapato ya Uwekezaji wa NCAA 154
3.3.15 Kuhusu Kutokuwepo kwa Ulinganifu katika Ukokotoaji wa Mafao ya Pensheni kwa Wanachama Wanaounganisha Vipindi vya Michango..... 155
SEHEMU YA NNE..... 157
4.0 HITIMISHO..... 157
4.1 Shukurani..... 157
4.2 Hoja..... 159
RANDAMA YA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..... a

ORODHA YA MAJEDWALI

Ukurasa

JEDWALI NA. 1.1: MCHANGANUO WA MAFUNGU YALIYOFIKA MBELE YA KAMATI MWEZI AGOSTI - OKTOBA, 2026 7
JEDWALI NA. 2.1: MWENENDO WA UKUSANYAJI WA MAPATO 2020/21 - 2024/25 14
JEDWALI NA. 2.2: ORODHA YA TAASISI NA IDADI YA VIWANJA VISIVYOKUWA NA HATI ZA UMILIKI 125
JEDWALI NA. 2.3: MCHANGANUO WA TAASISI NA UZINGATIAJI WAKE KATIKA MFUMO WA GAMIS.....127

ORODHA YA VIELELEZO

Ukurasa

KIELELEZO NA. 1.1: MGAWANYO WA MAFUNGU KATIKA ASILIMIA YALIYOFIKA MBELE YA KAMATI YA AGOSTI - OKTOBA, 2026. 8

KIELELEZO NA. 2.1: MWENENDO WA MAKISIO, MAKUSANYO HALISI NA ASILIMIA YA ZIADA/(PUNGUFU) KATI YA MWAKA 2020 -2025. 15

KIELELEZO NA. 2.2: ONGEZEKO LA IDADI YA MASHAURI YA KODI AMBAYO HAYAJATATULIWA (2019/ 2020 - 2024/2025) 17

TAARIFA YA KAMATI KUHUSU TAARIFA ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2024 NA TAREHE 30 JUNI, 2025

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Miaka ya Fedha iliyoishia tarehe 30 Juni, 2024 na 30 Juni, 2025, mtawalia, kama zilivyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Taarifa hii ni kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu matumizi ya Fedha za Umma na kubaini iwapo fedha hizo zilitumika kwa madhumuni yaliyoidhinishwa na Bunge, kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia usimamizi na matumizi ya Fedha za Umma.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha ufuatiliaji wa Taarifa hii, imegawanywa katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu muundo wa Taarifa, majukumu na msingi wa kazi za Kamati, pamoja na muhtasari wa matokeo ya uchambuzi. Sehemu ya Pili inawasilisha uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa miaka ya fedha 2023/2024 hadi 2024/2025, ikibainisha dosari na changamoto katika usimamizi na matumizi ya Fedha za Umma. Sehemu ya Tatu inawasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya Fedha za Umma.

1.3 Majukumu ya Kamati

Mheshimwa Spika, Kwa mujibu wa Kifungu cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ina majukumu yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025.

1.4 Njia Zilizotumika katika Utekelezaji wa Kazi za Kamati

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Bunge Toleo la 2025 zimeweka masharti kwamba Taarifa yoyote ya Kamati inayoingia Bungeni, inatakiwa kubainisha njia zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi inayotolewa Taarifa. Kwa msingi huo naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii. Njia hizo ni zifuatazo: -

a) Kufanya mapitio ya jumla ya Ripoti za CAG kwa lengo la kubaini hoja za ukaguzi zinazohitaji kupewa kipaumbele na kuweka msingi wa upangaji na utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kuzingatia Ratiba iliyoidhinishwa;

b) Kupokea na kuchambua vidokezo (*briefs*) vya Ripoti za CAG kuhusu hoja za ukaguzi za mafungu yaliyopangwa kujadiliwa, kabla ya Kamati kukutana na Maafisa Masuuli. Mbinu hii iliwezesha Kamati kufahamu kwa kina hoja husika, kubaini maeneo yanayohitaji ufafanuzi na kuandaa maswali ya msingi kwa ajili ya mahojiano;

c) Kufanya vikao vya mahojiano na Maafisa Masuuli kwa lengo la kupata ufafanuzi kuhusu hoja za ukaguzi, kubaini chanzo na ukubwa wa dosari zilizojitokeza, pamoja na kutathmini hatua zinazohitajika kurekebisha mapungufu na kuzuia matumizi yasiyo sahihi ya fedha za umma;

d) Kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa za ukaguzi pamoja na majibu ya Menejimenti za Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyokaguliwa, ili kutathmini hoja zilizobainishwa na CAG, kujiridhisha kuhusu uzito wa majibu yaliyotolewa na kubaini hatua stahiki za kushughulikia dosari zilizobainika; na

e) Kufanya tafiti kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha za umma kwa lengo la kupata maarifa na uzoefu unaosaidia kutathmini hoja za ukaguzi zilizobainishwa na CAG, kulinganisha na mbinu bora za usimamizi wa fedha za umma na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, njia na mbinu hizo ziliiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina kwa nia ya kulishauri Bunge kuhusu

hatua za kuchukua. Mbinu hizo ziliendana na matumizi na marejeo ya miongozo ifuatayo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoonesha dhamana ambayo Serikali imepewa na wajibu wa Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwemo eneo la matumizi ya fedha za umma.

b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 inayofafanua masharti muhimu kwa ajili ya kuwezesha ukaguzi, uandaaji wa Ripoti za CAG, uwasilishaji wake na hatimaye kujadiliwa na Kamati;

c) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 inayoweka miongozo ya matumizi ya fedha za umma na kusaidia kuamua iwapo kuna matumizi mabaya ya fedha za umma;

d) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, inayohusika na usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma kwa kuweka taratibu za utekelezaji wa bajeti na usimamizi wake;

e) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 inayogusa usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma katika mashirika ya umma;

f) Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410, inayoweka taratibu za kufuatwa wakati wa ununuzi wa bidhaa, huduma na kuingia mikataba kwa gharama ambazo zinahusisha matumizi ya fedha za umma;

g) Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286, inayosimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi ili kuwezesha kumbukumbu za kutumainiwa za fedha na usimamizi bora wa matumizi ya Fedha za Umma;

h) Sheria ya Kinga Madaraka na Haki za Bunge, Sura 296 inayoliwezesha Bunge, Wabunge na Kamati za Bunge kupata stahili kutokana na madaraka yake na kupata ushahidi bila vikwazo wakati wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma; na

i) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025 zinazobainisha utaratibu wa Ripoti za CAG kuhusu matumizi ya fedha za umma kuwasilishwa Bungeni, kushughulikiwa na Kamati na hatimaye Kamati kutoa Taarifa hii.

1.5 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Agosti hadi Oktoba 2026, shughuli za Kamati zilijikita katika maeneo makuu mawili; kuchambua na kushughulikia hoja za ukaguzi katika Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma zilizobainishwa katika Ripoti za CAG za miaka ya fedha 2023/24 na 2024/25; na kufuatilia utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati ya miaka iliyopita ili kubaini hatua zilizochukuliwa kurekebisha mapungufu

na kuimarisha uwajibikaji katika usimamizi na matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Kamati, ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa za hesabu zilizokaguliwa za mafungu 76 yakijumuisha Wizara 11, Wakala 7, Mashirika ya Umma 18, Taasisi na Idara Zinazojitegemea 36, pamoja na Sekretarieti za Mikoa 4.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa Taasisi zilizofika mbele ya Kamati kwa ajili ya mahojiano umeainishwa katika Jedwali Na. 1.1 hapa chini.

Jedwali Na. 1.1: Mchanganuo wa Mafungu yaliyofika mbele ya Kamati Mwezi Agosti - Oktoba, 2026.

Na.	Aina ya Taasisi/ Idara	Idadi	Asilimia (%)
1.	Taasisi na Idara Zinazojitegemea	36	47.4
2.	Mashirika ya Umma	18	23.7
3.	Wizara	11	14.5
4.	Wakala za Serikali	7	9.2
5.	Sekretarieti za Mikoa	4	5.3
Jumla		76	100


Chanzo: ***Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa za kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2025.***

Mheshimiwa Spika, mgawanyo huo unaonesha kuwa Taasisi na Idara Zinazojitegemea zilikuwa na mafungu mengi zaidi yaliyofanyiwa uchambuzi, asilimia 47.4, zikifuatiwa na Mashirika

ya Umma kwa asilimia 23.7, Wizara asilimia 14.5, Wakala asilimia 9.2 na Sekretarieti za Mikoa asilimia 5.3. Mgawanyo huu unaonesha wigo wa uchambuzi uliofanywa na Kamati katika taasisi mbalimbali za Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, uwajibikaji na uzingatiaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Mheshimiwa Spika, Chati Na. 1.1 hapa chini imeainisha katika asilimia mafungu yaliyofikia mbele ya Kamati kwa mahojiano.

Kielelezo Na. 1.1: Mgawanyo wa mafungu katika asilimiayaliyofika mbele ya Kamati ya Agosti - Oktoba, 2026.



Chanzo*: Uchambuzi wa Kamati Katika Taarifa za Ukaguzi Kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30, Juni, 2025.*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati kwa kila fungu unapatikana katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

1.6 Ufuatiliaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa na Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 13(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025, Kamati hufuatilia utekelezaji wa maoni, ushauri, mapendekezo na maazimio yake pamoja na ya Bunge. Ufuatiliaji huo hufanywa kwa kushirikiana na CAG, ambaye huwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati kwa kila fungu husika kabla ya kuanza kwa uchambuzi wa taarifa za ukaguzi za fungu hilo.

1.7 Vigezo vya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati iliandaa vigezo vya kuongoza uchambuzi na tathmini ya hoja za ukaguzi katika Ripoti za CAG, kwa kuzingatia uzito wa hoja, athari zake kwa fedha za umma na maeneo yaliyohitaji ufafanuzi wa Maafisa Masuuli. Vigezo hivyo vilitumika pia kuchagua mafungu ya kipaumbele ili kuelekeza uchambuzi na mahojiano katika maeneo yenye umuhimu mkubwa kwa uwajibikaji na usimamizi bora wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika kuchagua mafungu yatakayofanyiwa uchambuzi wa kina na kuhojiwa kwa Maafisa Masuuli, Kamati ilizingatia vigezo vifuatavyo:-

a) Uzito na umuhimu wa hoja za ukaguzi zilizoibuliwa na CAG;

b) Maslahi ya umma yanayohusiana na hoja za ukaguzi za fungu husika;

c) Aina ya hati ya ukaguzi iliyotolewa kwa fungu husika;

d) Kujirudia kwa hoja za ukaguzi katika Wizara, Idara, Wakala, Balozi na Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa;

e) Kiasi cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi na athari zake kwa matumizi ya fedha za umma;

f) Uendelevu wa ufuatiliaji wa ushauri, maoni na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hapo awali kwa fungu husika;

g) Umuhimu wa sekta na Mashirika ya Umma ya kimkakati (*strategic sectors and parastatals*) katika kufanikisha malengo na vipaumbele vya Serikali;

h) Matokeo ya kaguzi maalum (*special audits*) zilizofanyika hivi karibuni; na

i) Uzingatiaji wa matokeo ya kaguzi za ufanisi zilizofanyika katika mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo viliisaidia Kamati kuendelea na mchakato wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Ripoti za CAG.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika aya 1.7 ya taarifa hii, Kamati ilichambua kwa kina Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa miaka ya fedha 2023/2024 na 2024/2025. Uchambuzi huo ulibaini hoja na masuala mbalimbali kuhusu usimamizi, udhibiti na matumizi ya fedha za umma, ambazo zinawasilishwa kama ifuatavyo:-

2.1 Uchambuzi wa Hoja za Udhibiti wa Fedha za Umma *(Financial Management Issues)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la udhibiti wa fedha, Kamati ilichambua na kujadili hoja za ukaguzi zilizobainishwa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwa lengo la kutathmini ufanisi wa mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha za umma. Uchambuzi huo ulizingatia uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu za usimamizi wa fedha, hatua zilizochukuliwa na Taasisi katika kushughulikia hoja za ukaguzi na kutekeleza mapendekezo ya CAG, pamoja na athari za mapungufu yaliyobainishwa, ikiwemo matumizi yasiyo sahihi ya fedha, upotevu wa rasilimali za umma, kutokusanywa kwa mapato

stahiki, madeni yasiyolipwa kwa wakati na udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya uchambuzi wa hoja za ukaguzi kuhusu udhibiti wa fedha za umma katikaTaasisi zilizofika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

2.1.1 Uchambuzi wa Hali ya Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato ya Serikali ni msingi muhimu katika kugharamia huduma za kijamii, kutekeleza miradi ya maendeleo na kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Kamati ilichambua mifumo ya ukusanyaji wa mapato, ufanisi wa usimamizi wa kodi na changamoto zilizobainishwa katika Ripoti ya CAG kuhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kwa lengo la kubaini maeneo yanayohitaji maboresho.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025, TRA ilikusanya Shilingi trilioni 30.747, ikilinganishwa na makisio ya Shilingi trilioni 30.015, sawa na ziada ya Shilingi bilioni 731.81 au asilimia 2.4. Mafanikio haya yanaonesha kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ikilinganishwa na miaka iliyotangulia, ingawa bado zipo

changamoto katika usimamizi na udhibiti wa kodi zinazohitaji kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa muundo wa mapato yaliyokusanywa umebaini kuwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ilikuwa chanzo kikuu cha makusanyo, ikiwa na mchango wa Shilingi trilioni 9.12, sawa na asilimia 30.31 ya makusanyo yote. Kodi ya Mapato ilichangia Shilingi trilioni 8.65, sawa na asilimia 28.75, huku Ushuru wa Forodha ukichangia Shilingi trilioni 6.84, sawa na asilimia 22.73. Aidha, Ushuru wa Bidhaa ulichangia Shilingi trilioni 4.52, sawa na asilimia 15.02, na kodi na ushuru mwingine ukichangia Shilingi trilioni 0.96, sawa na asilimia 3.19. Muundo huu unaonesha umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa vyanzo vikuu vya mapato na kutathmini fursa za kupanua wigo wa kodi katika vyanzo vingine vinavyostahili.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2024/2025, unaonesha kuwa makusanyo yaliongezeka kutoka Shilingi bilioni 17,897.86 hadi Shilingi bilioni 30,747.18, sawa na ongezeko la takribani asilimia 71.8. Hata hivyo, katika miaka minne ya fedha kuanzia 2020/2021 hadi 2023/2024, makusanyo yalikuwa chini ya makisio yaliyowekwa, kabla ya kuvuka lengo katika mwaka wa fedha 2024/2025. Mwenendo huo unaonesha kuimarika kwa makusanyo katika mwaka wa mwisho wa kipindi hicho, pamoja na umuhimu wa kuendeleza hatua za kuboresha ufanisi wa usimamizi wa kodi.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa ukusanyaji wa mapato kwa upande wa Tanzania Bara ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na.2.1 hapa chini: -

Jedwali Na. 2.1: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato 2020/21 - 2024/25.

Mwaka wa fedha	Makisio (Sh.bilioni)	Makusanyo halisi (Sh.bilioni)	Makusanyo ya ziada/pungufu (Sh.bilioni)	(%) ya ziada/ upungufu
2024/25	30,015.37	30,747.18	731.81	2.4
2023/24	27,246.05	26,573.61	(672.44)	(2.5)
2022/23	24,106.81	23,039.73	(1,067.09)	(4.4)
2021/22	22,191.17	21,303.87	(887.30)	(4.0)
2020/21	20,709.32	17,897.86	(2,811.46)	(13.6)

Chanzo: ***Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa TRA kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2025.***


Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa, ongezeko la makusanyo katika mwaka wa fedha 2024/2025 lilichangiwa na kuongezeka kwa ushiriki wa walipakodi, utoaji wa elimu ya kodi, kampeni za kuhamasisha ulipaji kodi, ikiwemo kampeni za nyumba kwa nyumba, kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, pamoja na kuimarishwa kwa ufuatiliaji na mapambano dhidi ya biashara za magendo.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio hayo, Kamati ilibaini kuwa taarifa ya ukaguzi ya mwaka wa fedha 2024/2025 imebainisha hoja kadhaa zinazohitaji hatua za kiutawala na

kimfumo ili kuimarisha usimamizi wa kodi, kuongeza uhakika wa mapato ya Serikali na kuhakikisha kodi stahiki zinakusanywa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya mwenendo wa miaka mitano wa makusanyo ya mapato inabainisha kupungua taratibu kwa upungufu wa makusanyo kutoka upungufu wa juu wa asilimia 13.6 katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi kufikia makusanyo ya ziada katika Mwaka wa Fedha 2024/25, yakiashiria kuimarishwa kwa mifumo ya usimamizi. Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa miaka mitano (2020 – 2025) unaoneshwa katika Kielelezo Na. 2.1 hapa chini.

Kielelezo Na. 2.1: Mwenendo wa Makiso, Makusanyo Halisina asilimia ya ziada/(Pungufu) kati ya Mwaka 2020 -2025.



Chanzo: ***Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa TRA kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2025.***

Mheshimiwa Spika, kielelezo Na. 2.1 kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa makusanyo ya mapato ya Serikali, ambapo makusanyo yaliongezeka kwa asilimia 71.8 kutoka Sh. bilioni

17,897.86 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 30,747.18 mwaka 2024/25. Pamoja na ukuaji huo, makusanyo hayakufikia malengo yaliyokadiriwa kwa miaka minne mfululizo hadi 2023/24. Hata hivyo, mwaka 2024/25, hali ilibadilika ambapo makusanyo yalizidi makisio kwa Sh. bilioni 731.81, jambo linaloonesha mafanikio katika kufikia na kuvuka lengo la mapato.


Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kupitia TRA katika kuongeza makusanyo ya mapato. Hata hivyo, uchambuzi wa taarifa za ukaguzi za mwaka wa fedha 2024/25 umebaini mapungufu katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato yanayohitaji hatua madhubuti za kurekebisha ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha malengo ya mapato ya Serikali yanafikiwa. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: –

2.1.1.1 Kuongezeka Kwa Idadi ya Mashauri ya Kodi ambayo Hayajatatuliwa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa idadi ya mashauri ya kodi ambayo hayajatatuliwa imeongezeka kutoka mashauri saba (7) katika mwaka wa fedha 2019/2020 hadi mashauri 325 katika mwaka wa fedha 2024/2025. Mashauri hayo yako katika ngazi mbalimbali za utatuzi wa migogoro ya kodi, ikiwemo Bodi ya Rufani ya Kodi (TRAB), Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) na Mahakama ya Rufani ya Tanzania (CAT).

Mheshimiwa Spika, Ongezeko husika la mashauri ya kodi limeainishwa katika Kielelezo Na. 2.2 hapa chini:-

Kielelezo Na. 2.2: Ongezeko la Idadi ya Mashauri ya kodi ambayo hayajatatuliwa (2019/2020 - 2024/2025).



Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi za CAG kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025*

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo linaashiria changamoto katika mchakato wa utatuzi wa migogoro ya kodi, hususan katika kuhakikisha mashauri yanashughulikiwa na kukamilishwa kwa wakati. Kuendelea kwa hali hiyo kunaweza kuongeza mlundikano wa mashauri, kurefusha muda wa kupata maamuzi ya mwisho na kuchelewesha Serikali kupata uhakika kuhusu kiasi cha kodi kinachostahili kukusanywa.

2.1.1.2 Ongezeko la Thamani ya Mapato ya Serikali Yaliyo Kwenye Mgogoro

Mheshimiwa Spika, sambamba na ongezeko la idadi ya mashauri ya kodi, Kamati ilibaini kuwa thamani ya kodi inayohusishwa na migogoro hiyo imefikia takribani Shilingi trilioni 10.72. Aidha, wakati wa mahojiano, Menejimenti ya TRA ilieleza kuwa madai ya kodi yaliyofikia takribani Shilingi trilioni 11 yalihusisha, kwa kiasi kikubwa, kodi zilizopingwa na walipakodi na zilizokuwa katika hatua mbalimbali za mashauri mbele ya vyombo vya utatuzi wa migogoro ya kodi na mahakama. Kati ya kiasi hicho, Shilingi trilioni 5 zilihusishwa na walipakodi wasiozidi 10.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kwa madai hayo bila kupata uamuzi wa mwisho kunaweza kuathiri utabiri wa mapato na upangaji wa matumizi ya Serikali. Hata hivyo, ni muhimu kutofautisha kati ya kodi inayodaiwa na TRA, kodi iliyopingwa na mlipakodi, na kiasi kitakachothibitishwa kisheria kuwa kinastahili kulipwa baada ya kukamilika kwa taratibu za rufaa.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili uhalisia wa madai hayo, Mhe. Charles M. Njama, Mbunge na Mjumbe wa Kamati, alisisitiza umuhimu wa kuchambua umri wa madeni ya kodi ili

kubaini uwezekano wa kuyakusanya. Sehemu ya maelezo yake wakati wa mahojiano na Bodi na Menejimenti ya TRA alisema[1]:-

Nanukuu

"... Mheshimiwa Mwenyekiti, out of that hii weka aging , the earliest or the youngest, yaani tulitaka tuone kwamba inawezekana tuendelee na trilioni 11 lakini unakuta labda na yenyewe labda ina 9 trilioni, is above five years. Sasa kama its above five years ina maana risk yake ni kubwa zaidi..."

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi, uhalisia wa madai hayo unahitaji kuthibitishwa kupitia zoezi la kuhakiki na kusafisha kumbukumbu za madeni (data clean-up). Kwa hiyo, ni muhimu TRA kukamilisha zoezi hilo ili kubaini kiasi halisi cha madeni, umri wake, uwezekano wa kukusanywa na hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa kila kundi la madeni. Suala hili linapaswa kupewa kipaumbele kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati yaliyowasilishwa katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii.

[1] Rejea Ukurasa wa 41 wa Mahojiano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 3, Tarehe 15 Juni, 2026.

2.1.1.3 Mapungufu Katika Tathmini ya Kodi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa mapitio ya mafaili ya ukaguzi wa kodi yaliyokamilishwa na Idara ya Mapato ya Ndani (Domestic Revenue Department – DRD) na Idara ya Uchunguzi wa Kodi (Tax Investigation Department – TID) yalionesha kuwepo kwa mapungufu katika tathmini ya baadhi ya kodi. Mapungufu hayo yalihusu:-

a) Kodi ya Mapato ya Kampuni na Watu Binafsi yenye jumla ya Shilingi 26,466,897,576, ambapo Shilingi 25,471,522,250 zilihusu DRD na Shilingi 995,375,326 zilihusu TID;
b) Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) yenye jumla ya Shilingi 6,439,508,794, ambapo Shilingi 5,876,419,704 zilihusu DRD na Shilingi 563,089,090 zilihusu TID; na
c) Kodi ya Zuio (Withholding Tax) yenye thamani ya Shilingi 812,196,383, iliyohusu DRD.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, kodi zilizobainika kuwa na mapungufu katika tathmini zilifikia Shilingi 33,718,602,753. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 23,881,683,007.80 zilithibitishwa baada ya uhakiki, huku Shilingi 8,310,477,597 zikihitaji uhakiki zaidi ili kubaini uhalali na kiasi kinachostahili kutozwa.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaonesha mapungufu katika uhakiki wa taarifa za walipakodi, mapitio ya mafaili ya ukaguzi

na udhibiti wa ubora wa tathmini za kodi. Endapo mapungufu hayo hayatafanyiwa kazi, yanaweza kusababisha tathmini zisizo sahihi, migogoro ya kodi na hatari ya kutokusanywa kwa mapato yanayostahili.

2.1.1.4 Mafuta Yaliyokusudiwa Kusafirishwa Nje ya Nchi Kutothibitishwa Kuondoka Nchini

Mheshimiwa Spika, CAG alibaini kuwa lita 182,506,657 za mafuta, zenye thamani ya Shilingi 163,160,946,649, zilizotangazwa kusafirishwa kupitia bomba la TAZAMA kwenda nje ya nchi, hazikuwa zimethibitishwa kufika katika vituo vya mwisho vilivyokusudiwa. Uchambuzi wa Kamati ulionesha kuwa changamoto hiyo ilihusishwa na mapungufu katika ufuatiliaji wa mtiririko wa mafuta kwa wakati halisi (real-time tracking) kati ya vituo vya kuingilia na kutoka nchini.

Mheshimiwa Spika, akifafanua hoja hiyo mbele ya Kamati, Ndugu Isaya Jeremiah, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, alisema[2]:-

Nanukuu

"... Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tumelileta kwako linahusu mafuta ambayo yanasafirishwa kwa bomba la TAZAMA. Mwanzoni wakati tunakagua tulibaini

[2] Rejea Ukurasa wa 26 wa Mahojiano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 3, Tarehe 15 Juni, 2026.

kwamba kuna kiasi cha lita milioni 182 ambazo zilikuwa declared kama za transit kupitia bomba la TAZAMA hazikuvuka pale inyala kule kwenda upande wa pili." ... "

Mwisho wa nukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya ukaguzi, CAG na TRA walifanya usuluhishi *(reconciliation)* wa kiasi cha mafuta kilichokuwa hakijathibitishwa kuondoka nchini. Baada ya usuluhishi huo, lita milioni 14 zilibaki bila uthibitisho wa kutoka nchini na zilitakiwa kufanyiwa ufuatiliaji wa kodi stahiki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wakati wa mahojiano yaliyofanyika tarehe 15 Juni 2026, Menejimenti ya TRA iliieleza Kamati kuwa hatua za usuluhishi zilikuwa zimeendelea na kiasi cha mafuta ambacho bado kilihitaji uthibitisho wa kutokukusanywa kwa kodi kilikuwa lita milioni 2. Aidha, TRA ilieleza kuwa imeweka maafisa katika vituo vya kuhifadhi mafuta *(terminals)* ili kuhakikisha kuwa mafuta yanayotolewa yana nyaraka zinazothibitisha ulipaji wa kodi au uhalali wa kusafirishwa bila kulipiwa kodi nchini.

Mheshimiwa Spika, licha ya hatua hizo, ni muhimu kuhakikisha kuwa tofauti kati ya kiasi kilichobainishwa katika ukaguzi na kiasi kilichobaki baada ya usuluhishi inathibitishwa kwa nyaraka, na kwamba kodi yoyote inayostahili kulipwa inafuatiliwa hadi kukusanywa.

2.1.1.5 Kuchelewa Kufanya Ukaguzi wa Kodi Kwa Wakati

Mheshimiwa Spika, CAG alibaini kuwa ukaguzi wa kodi katika mashauri 55 yaliyohusisha mikoa minane ya kodi ulichelewa kwa kipindi cha miaka sita hadi kumi. Ucheleweshaji huo ulihusisha tathmini ya kodi yenye jumla ya Shilingi bilioni 12.18. Kuchelewa kufanya ukaguzi wa kodi kunaweza kucheleweshaa ukusanyaji wa mapato ya Serikali, kuongeza hatari ya kushindwa kukusanya kodi stahiki kutokana na kupungua kwa uwezo wa walipakodi kulipa madeni yao, na kupunguza thamani halisi ya mapato yatakayokusanywa kadiri muda unavyopita. Aidha, ucheleweshaji huo unaweza kuathiri ufanisi wa utekelezaji wa sheria za kodi na uwezo wa TRA kuchukua hatua za kisheria ndani ya muda unaoruhusiwa. Akifafanua hoja hiyo mbele ya Kamati, Ndugu Isaya Jeremiah, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, alisema[3]:-

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ya msingi inahusu ucheleweshaji wa Mamlaka kupitia hesabu za walipa kodi. Kwa hiyo sample tuliyokagua tulibaini wamecheleweshaa kwa kwa takribani miaka sita hadi mpaka kumi. Ikumbukwe,kadri unavyochelewa kupitia hesabu za mlipa kodi ukienda sheria inasema baada ya miaka mitano huwezi

[3] Rejea Uk. 18 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha Tarehe 15 Juni, 2026.

ukawa na uhalali wa kwenda kupitia hesabu zile..."

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, maelezo hayo yanaonesha umuhimu wa TRA kuimarisha upangaji wa ukaguzi unaozingatia vihatarishi, ufuatiliaji wa muda wa kisheria na matumizi ya mifumo ya TEHAMA ili kuhakikisha ukaguzi wa kodi unafanyika kwa wakati na hatua stahiki zinachukuliwa kabla ya muda wa kisheria kuisha.

2.1.1.6 Kutowasilishwa kwa Marejesho ya VAT kwa Wakati na Baadhi ya Walipakodi

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa walipakodi 17,573 hawakuwasilisha marejesho 93,953 ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa wakati. Aidha, TRA haikuwa imechukua hatua stahiki kwa wakati kuhakikisha walipakodi hao wanatimiza wajibu wao wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kutowasilishwa kwa marejesho ya kodi kwa wakati kunapunguza uwezo wa TRA kufuatilia miamala ya walipakodi, kubaini kodi inayostahili kulipwa na kuchukua hatua kwa wasiozingatia sheria. Hali hiyo inaweza kusababisha ucheleweshaji au upotevu wa mapato ya Serikali, pamoja na kutokutozwa kwa adhabu zinazostahili kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Juni 2026, Kamati ilifanya mahojiano na Bodi na Menejimenti ya TRA kwa lengo la kupata ufafanuzi kuhusu hoja za ukaguzi zilizobainishwa na CAG, hatua zilizochukuliwa na Mamlaka, pamoja na mikakati ya kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Kuhusu mifumo ya TEHAMA, Menejimenti ya TRA ilieleza kuwa inatumia mifumo mikuu miwili, ambayo ni TANCIS na IDRAS. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa, mfumo wa TANCIS ulianza kutumika tarehe 20 Januari 2026 na umeunganishwa na mifumo mingine, huku IDRAS ukitumika kusimamia kodi za ndani. Aidha, Menejimenti ilieleza kuwa IDRAS ina moduli 17, ambapo moduli 15 zilikuwa zimekamilika na zinafanya kazi wakati wa mahojiano.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ilifafanua kuwa kukamilika kwa moduli zilizobaki, hususan zinazohusu taarifa za bidhaa na hesabu za bidhaa *(inventory)*, kutasaidia kuimarisha ufuatiliaji wa bidhaa zinazoingia nchini, mauzo na mabadiliko ya akiba ya bidhaa, na hivyo kuwezesha TRA kubaini kodi stahiki kwa usahihi zaidi.Akifafanua umuhimu wa maboresho hayo, Kamishna Mkuu wa TRA, Ndugu Yusuph J. Mwenda, alisema[4]:-

[4] Rejea Uk. 66 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha Tarehe 15 Juni, 2026.

Nanukuu

"... Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishakamilisha na hizo module nyingine maana yake ni nini? Ni kwamba mizigo yote inayoingia kwenye mipaka yetu, not only pale kwenye bandari, kwenye mipaka yetu itakuwa inasomana na module ya inventory. Kwa hiyo kama ni Mheshimiwa Hasunga na timu yake ameingiza mzigo bandarini, ameingiza stock ya kiasi fulani, itakuwepo kwenye inventory na ukiuza inapunguza, tukija ku audit tutajua una stock ya kiasi gani, mapato yetu ni kiasi na kodi ni kiasi gani..."

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya kodi *(tax receivables)* yaliyofikia takribani Shilingi trilioni 11, Menejimenti ya TRA ilieleza kuwa Shilingi trilioni 10.6 zilihusiana na kodi zilizopingwa na walipakodi na zilizokuwa katika hatua mbalimbali za mashauri mbele ya TRAB, TRAT na Mahakama ya Rufani. Aidha, ilieleza kuwa Shilingi trilioni 5 za madai hayo zilihusishwa na walipakodi wasiozidi 10.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ilifafanua kuwa walipakodi wana haki ya kisheria ya kupinga tathmini za kodi na kukata rufaa. Hata hivyo, ilieleza kuwa imeendelea na zoezi la kuhakiki na kusafisha kumbukumbu za madeni kwa kukutana na walipakodi, kupitia ushahidi uliowasilishwa na kuthibitisha kiasi halisi kinachodaiwa kabla ya kuchukua hatua za utekelezaji wa

sheria.Katika kueleza hatua hizo, Kamishna Mkuu wa TRA alisema[5]:-

Nanukuu

"... Mheshimiwa Mwenyekiti, Mhe. Rais ametutaka tusitumie nguvu, lazima kunapokuwepo na madeni tunafanya cleaning up. Cleaning ya madeni maana yake tunakutana na walipa kodi, tunawaeleza wanachodaiwa na hiki na na kabla hatujaconclude kuanza enforcement kama wana evidence wanapaswa walete. Kwa hiyo, ikitokea zipo na kwa sababu tulikuwa hatuna mfumo wa IDRAS kumekuwa na changes kwenye receivables, and that is one of the reasons kwa nini kumekuwa na hiyo,... from now onwards baada ya kuwa na IDRAS hizi changamoto zitakuwa hazipo..."

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya mafuta yaliyosafirishwa kupitia bomba la TAZAMA, Menejimenti ya TRA ilieleza kuwa imefanya usuluhishi wa taarifa za mafuta yaliyotangazwa kusafirishwa bila kuthibitishwa kuondoka nchini. Kufikia tarehe ya mahojiano ya Kamati, tarehe 15 Juni 2026, TRA ilieleza kuwa kiasi kilichobaki kuhitaji uthibitisho wa kutokukusanywa kwa kodi kilikuwa lita milioni 2. Aidha, Mamlaka ilieleza kuwa imeweka maafisa katika vituo vya kuhifadhi mafuta ili

[5] Rejea Uk. 67 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha Tarehe 15 Juni, 2026.

kuhakikisha kuwa mafuta yanayotolewa yana nyaraka zinazothibitisha ulipaji wa kodi au uhalali wa usafirishaji wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa ukaguzi wa kodi, Menejimenti ilieleza kuwa ukaguzi hufanyika kwa kuzingatia vihatarishi vya walipakodi. Kwa mujibu wa maelezo hayo, walipakodi wenye mwenendo unaoonesha uzingatiaji mzuri wa sheria hawapewi kipaumbele sawa na wale wanaobainika kuwa na vihatarishi vikubwa vya kutokuzingatia sheria za kodi.Aidha, kuhusu uchunguzi wa makosa ya kodi, Menejimenti ilieleza kuwa baadhi ya mashauri yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi yalikuwa yameanza kushughulikiwa baada ya kukamilika kwa ukaguzi wa CAG. Ndugu Hashim Ngoda kutoka TRA alifafanua kuwa katika mwaka wa fedha uliotangulia, Idara ya Uchunguzi ilikamilisha mashauri 470 yaliyohusisha kodi iliyokwepwa yenye thamani ya takribani Shilingi bilioni 523, ambayo ilikuwa katika hatua mbalimbali za ukusanyaji. Alisema[6]:-

Nanukuu

"... Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kuna cases ambazo tayari tumeshaziingiza kwenye uchunguzi, bahati mbaya wakati CAG anafanya ukaguzi kesi hizi

[6] Rejea Uk. 94 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha Tarehe 15 Juni, 2026.

ndiyo zilikuwa zinaletwa kwenye idara yetu, kwa hiyo kwa wakati ule ni kweli kesi zilikuwa hazijaanzishwa lakini hivi ninavyoongea kuna kesi ambazo tunaendelea nazo. Katika mwaka wa fedha uliopita idara yetu imekamilisha kesi 470 za uchunguzi, kiasi cha takribani shilingi bilioni 523 zilibainika zikiwa zimekwepwa na ziko kwenye hatua mbalimbali za ukusanyaji...”

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa hoja za ukaguzi na ufafanuzi wa Menejimenti ya TRA, ni maoni ya Kamati kuwa, licha ya mafanikio ya TRA katika kuongeza makusanyo ya mapato, bado zipo changamoto katika usimamizi wa kodi, ikiwemo mashauri na madai ya kodi, mapungufu ya tathmini, ucheleweshaji wa ukaguzi na udhibiti wa mapato. Hivyo, mapendekezo ya Kamati katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii yanalenga kutatua changamoto hizo, kuimarisha mifumo ya udhibiti na kuhakikisha mapato yote stahiki yanakusanywa kwa wakati.

2.1.2 Uchambuzi wa Taarifa ya CAG kuhusu Hoja za Ukaguzi Zinazoathiri Ufanisi wa Kifedha na Kiutendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia hoja za ukaguzi wa mwaka wa fedha 2024/25 uchambuzi wa ufanisi wa kifedha wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulijikita katika usimamizi wa mapato na madeni, udhibiti wa gharama na madai

ya huduma za afya, urejeshaji wa fedha zilizotokana na udanganyifu, pamoja na udhibiti wa matumizi ya mafao kwa mujibu wa mikataba. Hoja hizo zina uhusiano wa moja kwa moja na ukwasi, ulinzi wa rasilimali za Mfuko na uwezo wake wa kutekeleza majukumu yake kwa uendelevu.Hoja za msingi zilizobainishwa ni kama ifuatavyo:-

2.1.2.1 Mapungufu Katika Usimamizi wa Michango na Madeni ya Mfuko

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2025, NHIF ilikuwa na michango ya waajiri inayodaiwa ya Sh. bilioni 104.1, ikilinganishwa na Sh. bilioni 73.4 mwaka uliotangulia. Kati ya madeni hayo, Sh. bilioni 33.78 ilikuwa ni kiasi kisicholipwa kwa zaidi ya siku 30, ikiwemo Sh. bilioni 13.67 iliyodaiwa kwa zaidi ya siku 360. Hata hivyo, kwa uhakiki uliofanywa na CAG hadi Septemba 2026, Mfuko ulikuwa umekusanya Sh. bilioni 96.56, huku Sh. bilioni 5.59 zikibainika kuwa si madeni halisi kutokana na makosa ya ankara na uhamishaji wa taarifa, na Sh. bilioni 1.95 zikiendelea kudaiwa.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa michango unaathiri upatikanaji wa fedha kwa wakati, unaongeza hatari ya kutokukusanyika kwa madeni na unaweza kuathiri uwezo wa Mfuko kutimiza wajibu wake wa kulipia huduma za afya. Aidha, makosa ya taarifa za madeni yanaonesha udhaifu katika usimamizi wa mifumo ya kumbukumbu za kifedha.

2.1.2.2 Kiwango Kikubwa cha Madai ya Huduma za Afya Kukataliwa

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/25, madai yenye thamani ya Sh. bilioni 70.8 kati ya Sh. bilioni 716 yaliyowasilishwa na watoa huduma yalikataliwa, sawa na takribani asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, kiwango kikubwa cha madai kukataliwa kinaashiria changamoto katika uwasilishaji, uhakiki na uzingatiaji wa taratibu za madai. Hali hii inaweza kusababisha migogoro kati ya Mfuko na watoa huduma, kuchelewesha malipo na kuathiri upatikanaji wa huduma kwa wanachama.

2.1.2.3 Urejeshaji Usioridhisha wa Fedha Zilizotokana na Udanganyifu

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2025, Mfuko ulikuwa na madai ya kurejeshewa fedha zilizotokana na udanganyifu yenye thamani ya Sh. bilioni 3.4, ikiwemo Sh. bilioni 2.0 zilizorithiwa kutoka miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuwepo kwa madeni ya muda mrefu kunafunga rasilimali za Mfuko na kuongeza hatari ya kutorejesha fedha hizo kikamilifu. Kutokuwepo kwa utaratibu madhubuti wa urejeshaji na tathmini ya uwezekano wa

kukusanya madeni kunaweza kusababisha hasara ya kifedha na kudhoofisha udhibiti dhidi ya udanganyifu.

2.1.2.4 Dosari Katika Udhibiti wa Matumizi ya Vifurushi vya Ziada vya Mafao

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 30 Juni 2025, NHIF ilikuwa na madeni ya Sh. bilioni 20.15 yaliyotokana na kutoa huduma kwa waajiri waliokuwa wamemaliza fedha walizolipa kwa vifurushi vya ziada vya mafao, kinyume na masharti ya mikataba yaliyotaka malipo kamili yafanyike kabla ya huduma kutolewa. Deni hilo liliongezeka kutoka Sh. bilioni 8.89 mwaka 2022/23 hadi Sh. bilioni 20.15 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la takribani asilimia 127.

Mheshimiwa Spika, kutoa huduma bila fedha za kutosha zilizolipwa mapema kunahatarisha ukwasi wa Mfuko na kunaweza kusababisha matumizi ya fedha zilizokusudiwa kugharamia mafao ya wanachama wengine. Aidha, kutotekeleza masharti ya mikataba kwa wakati kunadhoofisha nidhamu ya malipo na udhibiti wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Oktoba 2026, Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya NHIF kupata ufafanuzi wa hoja za ukaguzi zilizochambuliwa. Kuhusu ulipaji wa madai ya watoa huduma, hadi tarehe 30 Juni 2026, kiwango cha ulipaji kilikuwa asilimia 92, kufuatia kuimarishwa kwa mifumo ya kielektroniki, miongozo ya matibabu na uhakiki wa ustahiki wa huduma. Hata

hivyo, Kamati ilihitaji takwimu za madai yaliyokataliwa ili kuthibitisha ufanisi wa hatua hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu urejeshaji wa fedha zilizotokana na udanganyifu, Menejimenti ilieleza kuwa Sh. bilioni 2.1, sawa na asilimia 62 ya Sh. bilioni 3.4 zilizobainika, zilikuwa zimerejeshwa. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa urejeshaji wa salio unakabiliwa na changamoto zinazohusiana na vituo vilivyofungwa, vilivyozuiwa kutoa huduma na vile vinavyoendelea kufanya kazi bila kukamilisha makato ya madeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni yatokanayo na matumizi ya ziada katika vifurushi vya mafao, hadi tarehe 30 Juni 2026, NHIF ilikuwa imekusanya Sh. bilioni 18.26 kati ya Sh. bilioni 20.15 zilizokuwa zinadaiwa, na kubakiwa na Sh. bilioni 1.88. Wakati wa uhakiki wa CAG mwezi Oktoba 2026, salio hilo lilikuwa bado halijakusanywa, hali inayoonesha umuhimu wa kuimarisha mikakati ya urejeshaji wa madeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa matumizi ya vifurushi vya ziada, Menejimenti ilieleza kuwa imeanzisha mfumo wa kielektroniki unaotoa tahadhari kadri matumizi yanavyoongezeka na kusitisha huduma matumizi yanapofikia asilimia 90 ya fedha zilizowekwa, endapo hakuna fedha za ziada zilizowekwa. Hata hivyo, Kamati iliona umuhimu wa kuthibitisha ufanisi wa mfumo huo kupitia uhakiki wa utekelezaji wake na mwenendo wa

madeni mapya yatokanayo na matumizi ya ziada. Kwa kuzingatia hoja hizo, Kamati imetoa mapendekezo katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha na ufanisi wa kiutendaji wa NHIF.

2.1.3 Mapungufu Katika Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma Yaliyojitokeza Katika Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) kwa mwaka wa fedha 2024/25 na kubaini mapungufu katika usimamizi wa fedha, mifumo ya udhibiti wa ndani na matumizi ya fedha za umma. Mapungufu hayo yalihusu maeneo saba kama ifuatavyo: –

2.1.3.1 Taarifa za Fedha Hazikuandaliwa Kikamilifu Kupitia Mfumo wa Uhasibu wa MUSE

Mheshimiwa Spika, kupitia taarifa ya ukaguzi, Kamati ilibaini kuwa Taarifa za Fedha za TEMESA kwa mwaka wa fedha 2024/25 hazikuandaliwa kikamilifu kupitia Mfumo wa Uhasibu wa Serikali (MUSE). Kutotumia mfumo huo kikamilifu kunaweza kudhoofisha udhibiti wa ndani, ufuatiliaji wa miamala na ulinganifu wa taarifa za fedha, hivyo kuathiri usahihi na uaminifu wa taarifa hizo.

2.1.3.2 Udhaifu katika Usuluhishi wa Taarifa za Benki na Tofauti katika Salio la Fedha

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini udhaifu katika usuluhishi wa taarifa za benki za Wakala, ambapo baadhi ya akaunti za makusanyo ya mapato hazikufanyiwa usuluhishi, huku nyingine zikicheleweshwa kwa kipindi cha mwezi mmoja hadi miezi sita.Aidha,ukaguzi ulibaini tofauti ya Sh. bilioni 15.91 kati ya kumbukumbu za Cash Book za MUSE na taarifa za usuluhishi; Sh. milioni 46.18 kati ya salio la benki lililooneshwa katika taarifa ya usuluhishi na salio lililothibitishwa moja kwa moja na benki; pamoja na Sh. bilioni 1.75 zilizoonekana katika taarifa za benki bila kurekodiwa kwenye *"Cash Book".* Mapungufu haya yanaonesha udhaifu katika ulinganifu na uthibitishaji wa miamala ya fedha, hali inayoweza kuficha makosa au miamala isiyoidhinishwa na kuongeza hatari ya upotevu wa fedha za umma.

2.1.3.3 Uhamisho wa Fedha Kwenda Ofisi za Kikanda Uliozidi Kiasi Kilichoombwa

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, Kamati ilibaini kuwa vituo vitano vya TEMESA vilipokea fedha zaidi ya kiasi kilichoombwa kwa jumla ya Sh.2,172,028,268, wakati vituo sita vilipokea fedha pungufu kwa jumla ya Sh.204,642,059.34.Tofauti hizo hazikuambatana na mawasiliano rasmi yaliyotoa sababu za kupokea fedha zaidi au pungufu ya kiasi kilichoombwa.Ni maoni ya Kamati kuwa suala

hili lina uzito zaidi kwa kuwa ukaguzi ulibaini kuwa sehemu ya fedha zilizotumwa zaidi zilitumika katika kufanya malipo ya udanganyifu kwa wazabuni wasiokuwepo na baadhi ya hati za malipo ziliharibiwa kwa makusudi.

2.1.3.4 Ubadhilifu wa Fedha Kupitia Mfumo wa Malipo ya Pamoja – Bulk Payment System

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, Kamati ilibaini matumizi yasiyo sahihi ya Mfumo wa Malipo wa Pamoja *(Bulk Payment System)* katika ofisi za TEMESA Kagera, Mwanza na Dodoma, ambapo mfumo huo ulitumika kuchakata malipo yaliyofichwa kama posho za watumishi na malipo kwa wafanyakazi hewa wa mikataba.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa kiuchunguzi ulibaini kuwa katika kipindi cha mwaka 2021/22 hadi 2024/25, jumla ya Sh.5,011,510,000 zilitumika au kupotezwa kupitia miamala isiyo ya kawaida na ya udanganyifu. Aidha, haukuwepo ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa baadhi ya wazabuni waliolipwa walikuwa wametoa huduma kwa ofisi za mikoa husika.Kamati ina maoni kuwa matumizi hayo yanaonesha udhaifu mkubwa katika udhibiti wa malipo na uthibitishaji wa madai kabla ya malipo kufanyika.

2.1.3.5 Malipo ya Kughushi ya Sh.124,475,958 Katika Kituo cha TEMESA Manyara

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Kituo cha TEMESA Manyara kilifanya malipo ya kughushi yenye thamani ya Sh. 124,475,958 kwa mtu aliyedaiwa kuajiriwa kufanya kazi za muda. Hata hivyo, Meneja wa Mkoa alithibitisha kuwa mtu huyo hakutoa huduma yoyote kwa TEMESA Manyara katika mwaka wa fedha uliokaguliwa wala miaka iliyotangulia.

Ni maoni ya Kamati kuwa kufanyika na kuidhinishwa kwa malipo hayo bila kuthibitisha uwepo wa huduma kunadhihirisha udhaifu katika udhibiti wa ndani na uhakiki wa madai kabla ya malipo kuidhinishwa, jambo linaloongeza hatari ya upotevu wa fedha za umma.

2.1.3.6 Fedha Zilizoombwa Kuzidi Madai Yaliyothibitishwa ya Wazabuni kwa Sh.431,744,930

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, Kamati ilibaini kuwa Kituo cha TEMESA Dodoma kiliomba Sh.5,802,496,613 kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni yenye thamani ya Sh.5,370,751,685, hivyo kuomba fedha zaidi kwa Sh.431,744,930 kuliko thamani ya madai yaliyothibitishwa.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa hali hiyo inaonesha udhaifu katika mchakato wa kuandaa na kuthibitisha maombi ya fedha kabla ya kuidhinishwa.

2.1.3.7 Ukiukwaji wa Taratibu Katika Kuripoti Madeni ya Wazabuni

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, Kamati ilibaini udhaifu katika usuluhishi na ulinganifu wa taarifa za madeni ya wazabuni. TEMESA iliripoti madeni ya wazabuni ya Sh.65,307,984,131 katika Taarifa za Fedha, wakati mfumo wa MMTE ulionesha Sh.64,814,319,358, na ukaguzi ukabaini tofauti ya Sh.1,258,664,868.Aidha, uthibitisho wa nje wa madeni kwa sampuli ulibaini tofauti ya Sh.6,492,003,888.38 kati ya salio lililothibitishwa na wazabuni na kiasi kilichorekodiwa katika MMTE.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii, Kamati ina maoni kuwa tofauti hizo zinaonesha udhaifu uliokuwepo katika ulinganifu wa taarifa za madeni kati ya Taarifa za Fedha, Mfumo wa Madeni Temesa (MMTE) na kumbukumbu za wazabuni. Hali hiyo inaweza kuathiri usahihi wa taarifa za madeni na usimamizi wa mipango ya ulipaji.

Mheshimiwa Spika, ili kupata ufafanuzi kuhusu hoja zilizoibuliwa hapo juu na kujua hatua zilizochukuliwa kurekebisha mapungufu yaliyobainika na kuzuia yasijirudie tena, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli wa TEMESA akiwa na

Menejimenti mpya ya Wakala tarehe 21 Agosti, 2026, jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi ulitolewa kwa kila hoja ambapo kuhusu matumizi ya mfumo wa MUSE katika uhasibu, Menejimenti ya TEMESA ilieleza kuwa Taarifa za Fedha za mwaka 2025/26 ziliandaliwa kwa kuzingatia Waraka wa Uhasibu Na. 03 wa mwaka 2022/23 na kuwasilishwa kwa CAG tarehe 30 Agosti 2026.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa malipo kupitia mfumo wa Bulk Payment System na urejeshaji wa fedha zilizolipwa kwa njia ya udanganyifu, Menejimenti ilieleza kuwa watumishi 16 walikuwa wamefukuzwa kazi, mapendekezo ya hatua za kinidhamu kwa watumishi wengine yalikuwa yametolewa, na suala hilo liliendelea kufuatiliwa na TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya mfumo wa TIMIS katika uhakiki wa madai na maombi ya fedha, Menejimenti ilieleza kuwa mfumo huo una hatua za usuluhishi *(reconciliation)*, uidhinishaji *(approval)* na idhini ya mwisho *(authorisation)* zinazolenga kuimarisha uhakiki na uidhinishaji wa miamala.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepokea maelezo na ufafanuzi wa Menejimenti ya TEMESA. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa hatua zilizoelezwa zinapaswa kuambatana na ushahidi wa

utekelezaji ili kuhakikisha mapungufu yaliyobainika yanarekebishwa kikamilifu. Kwa msingi huo, Kamati imesisitiza umuhimu wa kuimarisha udhibiti wa ndani, kuhakikisha mifumo ya MUSE, TIMIS[7] na mfumo wa malipo ya pamoja *(Bulk Payment System)* inatumika ipasavyo, kuthibitisha madai na maombi ya fedha kabla ya kuidhinishwa, kufuatilia na kurejesha fedha zilizopotezwa kwa njia ya udanganyifu, na kukamilisha hatua za kisheria na kinidhamu dhidi ya waliohusika. Hatua hizo ni muhimu katika kuimarisha uwajibikaji, kulinda rasilimali za umma na kuzuia kujirudia kwa mapungufu hayo.

2.2 Uchambuzi wa Hoja za Ununuzi wa Umma na Usimamizi wa Mikataba *(Procurement and Contract Management Issues)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba, Kamati ilichambua na kujadili hoja za ukaguzi zilizobainishwa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwa lengo la kutathmini uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu. Uchambuzi ulijikita katika uwazi na ushindani wa michakato ya ununuzi, maandalizi na utekelezaji wa mikataba, usimamizi wa malipo na mabadiliko ya mikataba, pamoja na madai yanayotokana na utekelezaji wake.

[7] TEMESA Intergrated Management Information System.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilitathmini hatua zilizochukuliwa na Taasisi husika kushughulikia hoja za ukaguzi na kuzuia kujirudia kwa mapungufu yaliyobainishwa. Kamati pia ilizingatia athari za mapungufu hayo, zikiwemo kuchelewa kwa miradi, kuongezeka kwa gharama, matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma na kutopatikana kwa thamani halisi ya fedha *(Value for Money)*.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwa hoja zinahosu masuala ya ununuzi na usimamizi wa mikataba ni kama ifuatavyo: -

2.2.1 Changamoto Katika Usimamizi wa Mradi wa Mabasi ya BRT Awamu ya II

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika hesabu za Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) ulibaini changamoto kadhaa katika mchakato mzima wa ununuzi na usimamizi wa mikataba mbalimbali iliyoingiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia mchakato wa ununuzi na usimamizi wa mikataba ya huduma kwa ajili ya utekelezaji wa BRT Awamu ya II, ikiwemo mikataba ya usambazaji, uendeshaji na matengenezo ya mabasi pamoja na mifumo na miundombinu inayohusiana na utoaji wa huduma. Katika mapitio hayo, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazohusu uhalali wa mabadiliko ya mikataba, usimamizi wa watoa huduma,

utekelezaji wa masharti ya mikataba, uwajibikaji na masuala ya kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa tarehe 31 Januari 2025, Wakala ulisaini Mkataba wa Huduma (*Service Agreement*) na Metro Link City Company Limited kwa ajili ya usambazaji, uendeshaji na matengenezo ya mabasi 334 yatakayotoa huduma katika njia za mlisho (*feeder routes*) za DART Awamu ya II. Ilipofika, tarehe 25 Aprili 2025, kampuni hiyo ilianzisha kampuni maalum ya kutekeleza mradi (*Special Purpose Vehicle – SPV*) ijulikanayo kama Metrolink City Phase Two Limited, iliyosajiliwa BRELA kwa Cheti Na. 184124440.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, Kamati ilibaini kuwa kulifanyika mabadiliko katika muundo wa utekelezaji wa mkataba, ambapo majukumu ya utekelezaji yalihusishwa na Dar Metro Limited, bila kuoneshwa ushahidi wa kutosha wa idhini ya Kamati Elekezi ya PPP na vyombo vingine husika. Hali hii inaleta changamoto kuhusu usahihi wa uhamishaji wa mkataba, mabadiliko ya SPV, uwajibikaji wa wahusika na ulinzi wa maslahi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, Kamati pia ilibaini kuwa katika baadhi ya makabidhiano ya vituo, maegesho na miundombinu kwa mtoa huduma, nyaraka za makabidhiano hazikuwa na sehemu mahsusi za saini za wawakilishi wa pande zote, hazikuonesha thamani ya mali

zilizokabidhiwa na hakukuwa na uthibitisho uliosainiwa na mtoa huduma wa kuthibitisha kupokea miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, mapungufu haya yanaweza kuleta changamoto katika kuthibitisha umiliki, hali ya mali wakati wa makabidhiano, wajibu wa matengenezo na uwajibikaji endapo mali zitaharibika au kutumika kinyume na masharti ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa masuala ya kifedha na kodi, Kamati ilibaini kuwepo kwa suala la Kodi ya Mapato ya Dola za Marekani 90,000 inayohusiana na mauzo ya makubaliano ya huduma yenye thamani ya Dola za Marekani 300,000. Aidha, suala hili linaonesha umuhimu wa kuimarisha taratibu za uhakiki wa miamala ya kimkataba na kuhakikisha kuwa mabadiliko ya kimuundo au kifedha katika utekelezaji wa mikataba yanafuatana na uthibitisho wa ulipaji wa kodi na matakwa mengine ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Kamati imebainisha kuwa changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi kwa haraka ili kuimarisha usimamizi wa mikataba ya BRTa awamu ya Pili zinajikita katika maeneo makuu sita (6) yafuatayo:-

a) uidhinishaji wa mabadiliko ya mikataba na SPV[8];
b) ufuatiliaji wa utekelezaji wa masharti ya mikataba;
c) makabidhiano na usimamizi wa mali za Serikali;
d) uwajibikaji wa watoa huduma;

[8] SPV (Special Purpose Vehicle).

e) udhibiti wa masuala ya kifedha na kodi; na

f) ufuatiliaji wa utekelezaji wa maelekezo ya vyombo vya usimamizi wa miradi ya PPP.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia changamoto hizo, mapendekezo ya Kamati yamelenga kuweka hatua madhubuti za kurekebisha mapungufu yaliyobainika, kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mikataba ya BRT Awamu ya Pili, kuongeza uwajibikaji wa wahusika, kulinda mali na maslahi ya Serikali, pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa mikataba na maelekezo ya vyombo vya usimamizi wa miradi ya PPP unazingatia matakwa ya kisheria na kimkataba.

2.2.2 Malipo ya Shilingi Milioni 523.15 Yaliyofanyika kwa Kazi za Ukarabati wa Barabara za Ndani ya Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu Mzumbe Zisizokidhi Viwango

Mheshimiwa Spika, Kipengele Na. 2.10.2 cha Orodha ya Makadirio ya Kazi na Gharama *(BOQ)* ya Mkataba Na. TR76/2023/2024/W/09, uliosainiwa tarehe 18 Machi 2024 kati ya Chuo Kikuu Mzumbe na M/S Judex Contractors Limited kwa ajili ya ukarabati wa barabara za ndani katika Kampasi Kuu kwa thamani ya Sh. 920,383,579.71, kilitaka kujengwa kwa tabaka la juu la zege lenye uimara wa MPa 25 na muda wa matumizi uliokadiriwa kuwa miaka 25.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, uhakiki wa ukaguzi wa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025, uliofanyika mwezi Julai 2025,

ulibaini kuwa tabaka gumu la barabara lililojengwa lilikuwa na wastani wa uimara wa MPa 18 pekee, sawa na asilimia 72 ya uimara wa zege uliobainishwa katika usanifu, kinyume na masharti ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapungu hayo ya kutokidhi kwa vigezo husika, Chuo Kikuu kilimlipa mkandarasi kiasi cha Sh. 523,148,280 kwa kazi zilizotekelezwa. Dosari hiyo ilitokana na kutokuwepo kwa Meneja wa Mradi aliyeteuliwa rasmi, pamoja na Meneja wa Mradi aliyekasimiwa jukumu hilo kutokuwa na utaalamu wa kutosha wa kusimamia kazi za ujenzi(civil works). Kutokana na hali hiyo, malipo ya Sh. 523,148,280 yalifanyika kwa kazi zisizokidhi viwango, jambo linaloweza kusababisha hasara ya fedha ya kiasi hicho na kushindwa kupata thamani inayolingana na fedha zilizotumika.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 18 Agosti, 2026, Kamati ilikutana na Mwenyekiti wa Baraza na Menejimenti ya Chuo Kikuu Mzumbe ili kupata maelezo ya hatua walizochukua kuhusu hoja hii. Menejimenti iliifahamisha Kamati kuwa imepokea mapendekezo ya Mkaguzi na imeeleza kuwa kazi za ukarabati wa barabara zinaendelea na mradi bado haujakabidhiwa kwa Chuo Kikuu. Aidha, wakati wa makabidhiano, utafanyika ukaguzi na upimaji rasmi kwa mujibu wa mpango wa ukaguzi *(Inspection and Testing Plan)* ili kuthibitisha ubora na uimara wa barabara kwa kuzingatia masharti ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Chuo iliifahamisha Kamati kuwa, Barabara itakubaliwa endapo matokeo ya vipimo yataonesha kuwa imefikia kiwango cha uimara cha 25MPa kilichoainishwa kwenye mkataba. Endapo vipimo vitaonesha kutofikiwa kiwango hicho, Menejimenti itachukua hatua stahiki za marekebisho kwa mujibu wa masharti ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine iliyochukuliwa kurekebisha dosari katika mradi huo ni kuimarishwa kwa usimamizi kupitia uteuzi wa Meneja Mpya wa Mradi. Kufuatia hatua hiyo, Mkandarasi anaendelea na shughuli za ukarabati wa barabara katika kipande cha Haile Selassie hadi Chang'arawe.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa kutokidhi kwa uimara wa zege kiwango cha MPa 25 kilichoainishwa katika mkataba kunaonesha udhaifu katika usimamizi na udhibiti wa ubora wa kazi za ujenzi, hali inayoweza kusababisha matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma na kupunguza muda wa matumizi ya barabara. Kamati imepokea maelezo ya Menejimenti kuhusu uteuzi wa Meneja mpya wa Mradi na mpango wa kufanya ukaguzi na upimaji kabla ya makabidhiano rasmi; hata hivyo, Kamati imependekeza kuwa Chuo kihakikishe kuwa kazi zote zinakidhi viwango vya mkataba, na endapo kiwango cha MPa 25 hakitafikiwa, Mkandarasi awajibishwe kufanya marekebisho yanayostahili kwa gharama zake kabla ya mradi kukabidhiwa rasmi.

2.2.3 Zabuni Zenye Thamani ya Shilingi Bilioni 1.54 na Shilingi Bilioni 29.7 Mtawalia Zilizotolewa kwa Wazabuni Wasiokidhi Baadhi ya Vigezo Vilivyotakiwa Katika Chuo Kikuu Mzumbe

Mheshimiwa Spika, taarifa ya CAG ilibainisha kuwa Chuo Kikuu Mzumbe kilifanya shughuli mbalimbali za ununuzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2025,. Katika hatua hiyo CAG alipitia mikataba 40 ya ununuzi wa kazi, bidhaa na huduma yenye thamani ya jumla ya Sh.3,128,467,718. Mapitio ya CAG yalibaini kuwa Chuo Kikuu Mzumbe kilitoa zabuni 12 zenye thamani ya Sh. 1,535,806,412 kwa wazabuni na wakandarasi ambao hawakukidhi baadhi vigezo vya lazima vya sifa vilivyoainishwa katika nyaraka husika za zabuni.

Mheshimiwa Spika, nyaraka za zabuni ziliwataka wazabuni kuthibitisha kuwa wana uwezo wa kupata rasilimali za kifedha za kutosha kwa kuwasilisha taarifa za sasa za benki au uthibitisho halali wa uwezo wa kukopa unaoonesha wastani wa fedha usiopungua Shilingi 50,000,000. Pia, walitakiwa kuthibitisha kuwa wana uzoefu unaohusika kwa kuwasilisha mikataba kati ya miwili na mitano ya kazi zinazofanana iliyotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2022 hadi 2024.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baadhi ya wazabuni waliofanikiwa *(successful bidders)* hawakuwasilisha ushahidi wa kutosha wa uwezo wao wa kifedha. Waliwasilisha taarifa za

benki zilizopitwa na wakati za mwaka 2022 hadi 2023, taarifa za fedha zilizokaguliwa ambazo hazikuwa zimesainiwa au kugongwa mihuri, taarifa za fedha zilizopitwa na wakati, au taarifa za robo mwaka badala ya taarifa za sasa za benki au uthibitisho halali wa uwezo wa kukopa.

Mheshimiwa Spika, wazabuni wawili kati ya wazabuni 12 waliofanikiwa waliwasilisha mkataba mmoja tu wa kazi inayofanana badala ya mikataba miwili hadi mitano iliyotakiwa. Kasoro hiyo ilitokana na udhibiti usioridhisha katika mchakato wa tathmini ya zabuni.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine kwa hoja inayohusu manunuzi,**k**atika utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), Chuo Kikuu Mzumbe kilitoa mikataba minne yenye thamani ya jumla ya Sh.29,772,110,771 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali, ikijumuisha majengo, mifumo ya maji na mifumo ya majitaka katika Kampasi Kuu ya Morogoro na Kampasi ya Tanga. Hata hivyo, Timu ya Tathmini ilikubali nyaraka zilizowasilishwa ambazo hazikukidhi vigezo vilivyowekwa, na baadaye wazabuni husika walipewa mikataba kinyume na matakwa ya nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka ufafanuzi kuhusu hatua zilizochukuliwa kushughulikia hoja hii. Katika kikao kilichofanyika tarehe 18 Agosti 2026, Menejimenti ya Chuo Kikuu Mzumbe ilieleza kuwa itaendelea kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa

taratibu za manunuzi ya umma, ikiwemo kuhakikisha vigezo vya zabuni vinafuatwa kikamilifu katika hatua zote za manunuzi. Aidha, Menejimenti ilieleza kuwa itaimarisha uwezo na uwajibikaji wa Timu za Tathmini na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU) ili kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za manunuzi ya umma.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, pamoja na Menejimenti ya Chuo Kikuu Mzumbe kueleza hatua za kuimarisha usimamizi wa manunuzi ya umma, majibu hayo yanaonesha zaidi nia ya kuboresha taratibu bila kubainisha hatua mahususi zilizotekelezwa kurekebisha dosari zilizoibuliwa na ukaguzi. Hali hiyo inaweza kusababisha kujirudia kwa ukiukwaji wa taratibu za manunuzi, kuathiri ushindani na uwazi katika utoaji wa zabuni, pamoja na kuongezeka kwa hatari ya matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma. Kwa msingi huo, Kamati imetoa mapendekezo katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii yanayolenga kuhakikisha kuwa vigezo vya zabuni vinafuatwa kikamilifu na Timu za Tathmini pamoja na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi vinawajibika ipasavyo katika kila hatua ya mchakato wa manunuzi.

2.2.4 Dosari Katika Ununuzi wa Pikipiki 700 za Chanjo ya Mifugo Uliofanyika Katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa CAG ulibaini dosari katika ununuzi na usimamizi wa pikipiki 700 zenye thamani ya Shilingi

bilioni 2.2624 zilizonunuliwa kwa ajili ya Kampeni ya Chanjo za Mifugo ya mwaka 2024/2025 kupitia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA). Pikipiki hizo hazikukidhi kikamilifu sifa za kiufundi zilizoidhinishwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa pikipiki zilizonunuliwa zilikuwa na uwezo mdogo wa injini kuliko ule ulioainishwa katika mahitaji ya awali ya ununuzi. Kwa mujibu wa maelezo ya CAG, pikipiki zilizoidhinishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu zilipaswa kuwa na uwezo wa injini wa kati ya CC 150 na CC 200. Hata hivyo, pikipiki zilizonunuliwa zilikuwa za aina ya Hero Hunter zenye uwezo wa injini wa CC 125, badala ya pikipiki aina ya King Lion zenye uwezo wa injini wa CC 150 zilizokuwa zimeainishwa awali.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha tarehe 5 Agosti 2026, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kupata ufafanuzi kuhusu sababu za kubadili sifa za kiufundi bila kupata idhini mpya kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na hatua zilizochukuliwa kuhakikisha kuwa fedha za umma zinalindwa na thamani ya fedha inapatikana.

Mheshimiwa Spika, katika ufafanuzi wake, Afisa Masuuli alieleza kuwa GPSA iliifahamisha Wizara kuwa pikipiki aina ya King Lion zilizokuwa zimeainishwa katika mahitaji ya awali hazikupatikana sokoni wakati wa kuanza kwa kampeni ya chanjo. Kutokana na ufinyu wa muda uliokuwepo kabla ya kuanza kwa zoezi hilo, GPSA ilishauri kununuliwa kwa pikipiki

aina ya Hero Hunter zenye uwezo mdogo wa injini. Kwa mujibu wa Afisa Masuuli, GPSA ilieleza kuwa pikipiki hizo zingeweza kutumika katika kuwasaidia waratibu kufikisha huduma za chanjo katika vijiji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ilibainisha kuwa kutopatikana kwa pikipiki zilizokuwa zimeidhinishwa hakukuondoa wajibu wa Wizara kurejea Ofisi ya Waziri Mkuu ili kupata idhini mpya kabla ya kubadili sifa za kiufundi za bidhaa zilizoidhinishwa. Kutokuchukua hatua hiyo kulisababisha ununuzi kufanyika bila kuzingatia kikamilifu mahitaji yaliyoidhinishwa, hali inayoweza kuathiri ufanisi wa matumizi ya pikipiki hizo katika mazingira yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilisisitiza kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipaswa kurejea Ofisi ya Waziri Mkuu ili kupata idhini ya kubadili aina ya pikipiki zilizoidhinishwa awali kabla ya kuendelea na ununuzi. Msimamo huo unathibitishwa na maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati na Ndugu Richard Masini, Mhasibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kama yalivyonukuliwa katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) ya tarehe 5 Agosti 2026, ukurasa wa 63, kama alisema:-[9]

Nanukuu

[9] Rejea Uk. 63 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 3 Tarehe 05 Agosti , 2026.

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Vile vya awali ni kweli tulipata kibali cha Ofisi ya Waziri Mkuu kununua baada ya kupata specs kutoka ujenzi, na hii ya pili hatukuweza kupata kibali kwa sababu walisema tu tuendelee nao kwa sababu alishakuwa amepokea fedha, akasema ata-deliver zile nyingine. Kwa hiyo, hatukurudi, ilikuwa inakuomba tena kibali..."

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa idhini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya kubadili sifa za kiufundi *(specifications)* za pikipiki zilizoidhinishwa awali kulithibitishwa pia na maelezo yaliyotolewa na Ndugu Willium Mcharo Msoffe, kutoka Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (DPMU) cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kama yanavyonukuliwa alisema[10]:-

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, labda issue nyingine ilikuwa ni ya approval. Sheria baada ya kugundua kwamba katika mazingira fulani, approval inaweza isipatikane labda kwa muda huo, ilitoa option ya kupata approval kwa njia ya retrospective ambayo baada ya kufanya tukio hilo, mnaandika barua na kujenga hoja na kwenda kupata approval. Sasa ninadhani tutalifanya hilo kwa ajili ya kufanikisha hilo..."

Mwisho wa Nukuu.

[10] Rejea Uk. 67 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 3 Tarehe 05 Agosti , 2026.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2023 (Na. 10 ya 2023) na Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2024 (GN Na. 518 ya 2024), manunuzi ya Serikali yanapaswa kuzingatia mahitaji na sifa za kiufundi *(specifications)* zilizoainishwa na kuidhinishwa. Aidha, mabadiliko ya mahitaji hayo yanapaswa kufuata taratibu za kisheria na kupata idhini ya mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, ukaguzi pia ulibaini kuwa kiasi cha Shilingi milioni 212.1 kilichobaki kutokana na ununuzi huo kilikuwa hakijarejeshwa na GPSA hadi Kamati ilipokutana na Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo ya Afisa Masuuli kuwa pikipiki aina ya King Lion hazikupatikana sokoni na GPSA ikashauri kununuliwa kwa pikipiki aina ya Hero Hunter, Kamati ilibaini kuwa mabadiliko hayo yalifanyika bila kupata idhini ya mamlaka iliyokuwa imeidhinisha mahitaji ya awali. Kamati ilisisitiza kuwa ufinyu wa muda wa kuanza kwa Kampeni ya Chanjo za Mifugo hauondoi wajibu wa Wizara na GPSA kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi wa umma. Hivyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa fedha zilizobaki zinarejeshwa na taratibu za ununuzi zinafuatwa ili kulinda fedha za umma na kupata thamani inayostahili.

2.2.5 Mapungufu Katika Utekelezaji wa Mkataba wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Fungu - 68

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua hoja ya ukaguzi kuhusu utekelezaji wa Mkataba Na. ME.006/2021-2022/HQ/W/01 kati ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) wenye thamani ya Shilingi 23,948,057,189, na kubaini hoja za msingi kama ifuatavyo:-

2.2.5.1 Kuchelewa Kukamilika kwa Ujenzi na Matumizi ya Jengo Bila Makabidhiano Rasmi

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa muda wa nyongeza ya mkataba uliishia tarehe 30 Juni 2025, hata hivyo Wizara ilianza kutumia jengo tarehe 1 Julai 2025 bila kufanyika kwa makabidhiano rasmi. Wakati huo, baadhi ya kazi muhimu, ikiwemo mfumo wa pampu za kuzima moto, upakaji rangi na eneo la kuingilia, zilikuwa bado hazijakamilika. Hali hii inaonesha udhaifu katika usimamizi wa utekelezaji na makabidhiano ya mradi.

2.2.5.2 Utekelezaji wa Kazi Kinyume na BOQ na Vigezo vya Kitaalamu Vilivyoidhinishwa

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG ulibaini kuwa safu ya saruji *(cement screed)* iliwekwa juu

ya viungio vya upanuzi *(expansion joints)* kinyume na matakwa yaliyobainishwa katika BOQ. Hatua hiyo inaweza kuathiri utendaji wa viungio hivyo na kusababisha hitaji la kufanya marekebisho ya kazi zilizotekelezwa.

2.2.5.3 Kuendelea kwa Utekelezaji wa Mkataba Baada ya Muda Wake wa Utekelezaji Kuisha

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi ulibaini kuwa muda wa mkataba uliisha bila kuwepo kwa nyongeza nyingine ya muda iliyooneshwa kuwa imeidhinishwa kwa mujibu wa Kifungu 35.1 cha Masharti ya Mkataba. Kamati ilibaini kuwa Addendum Na. 4 iliongeza muda wa utekelezaji hadi tarehe 31 Machi 2026, lakini hadi tarehe 30 Septemba 2026 kazi bado zilikuwa zinaendelea bila ushahidi wa nyongeza nyingine ya muda iliyosainiwa na pande zote.

2.2.5.4 Kutokamilika kwa Kazi Muhimu Licha ya Kumalizika kwa Muda wa Mkataba

Mheshimiwa Spika, uhakiki wa CAG uliofanyika tarehe 29 Septemba 2026 ulionesha kuwa ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 99, lakini mfumo wa kuzima moto ulikuwa bado haujakamilika. Aidha, marekebisho ya viungio vya upanuzi yalikuwa yamefikia asilimia 70, hivyo mradi haukuwa umekamilika kikamilifu licha ya muda wa nyongeza ya mkataba kuwa umeshaisha.

Mheshimiwa Spika, dosari hizo zinaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi, kucheleweshaji kukamilika na makabidhiano rasmi ya jengo, kuathiri ubora na usalama wa jengo, pamoja na kuongeza hatari ya kutokuwapo kwa uwajibikaji wa kimkataba kwa kazi zinazoendelea baada ya muda wa mkataba kuisha.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 06 Oktoba, 2026, Kamati ilikutana na Menejimenti ya Wizara ili kupata ufafanuzi wa hoja zilizojitokeza kuhusu usimamizi wa mkataba wa ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara. Menejimenti iliifahamisha Kamati kuwa hadi tarehe 29 Septemba 2026, ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 99, na kazi za upakaji rangi pamoja na uboreshaji wa eneo la kuingilia zilikuwa zinaendelea. Aidha, menejimenti ilieleza kuwa pampu za kuzima moto zimefungwa na kazi zilizobaki zinatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa Desemba 2026.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viungio vya upanuzi, Menejimenti ilieleza kuwa Mkandarasi anaendelea na marekebisho na utekelezaji ulikuwa umefikia asilimia 70, huku kazi hizo zikitarajiwa kukamilika kabla ya Desemba 2026. Aidha, Menejimenti ilieleza kuwa Addendum Na. 4 iliongeza muda wa mkataba hadi tarehe **3**1 Machi 2026 na imewasilishwa kwa ajili ya mapitio.

Mheshimiwa Spika, baada ya mahojiano na Afisa Masuuli, Ni maoni ya Kamati kuwa, pamoja na Menejimenti kueleza hatua

zinazoendelea kukamilisha ujenzi na marekebisho ya kazi zenye dosari, mradi umeendelea kutekelezwa baada ya muda wa mkataba kuisha bila ushahidi wa nyongeza nyingine ya muda iliyoidhinishwa. Aidha, matumizi ya jengo kabla ya makabidhiano rasmi na kutokamilika kwa mfumo wa kuzima moto pamoja na marekebisho ya viungio vya upanuzi vinaashiria changamoto katika usimamizi wa mkataba, unaoweza kuathiri ubora, usalama na uwajibikaji wa kimkataba.

2.2.6 Mapungufu Katika Usimamizi na Utekelezaji wa Mkataba wa Upangishaji wa Ardhi kati ya UDSM na Mlimani City Holding Limited (MHL)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia hoja za ukaguzi zinazohusu mkataba wa upangishaji wa ardhi kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Mlimani City Holding Limited (MHL). Mkataba huo ulisainiwa tarehe 5 Juni 2004, ambapo UDSM ilikubali kuikodisha MHL eneo la ardhi lenye Hati Miliki Na. 47674, lililopo Plot Na. 2, Block L, Ubungo, Dar es Salaam, lenye ukubwa wa takribani hekta 40 kwa kipindi cha miaka 50.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, pamoja na umuhimu wa mkataba huo katika kuiwezesha Chuo kunufaika na ardhi yake, bado kuna mapungufu katika masharti ya malipo ya pango na usimamizi wa vihatarishi vinavyoweza kujitokeza mkataba utakapomalizika. Mapungufu hayo yamefafanuliwa kama ifuatavyo:-

2.2.6.1 Ukiukwaji wa Masharti ya Malipo ya Ada za Pango kwa UDSM

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 1.1 (j) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 10.1 cha Memorandum for Ground Lease, kinaeleza kuwa UDSM inapaswa kupata asilimia 10 ya pango ghafi *(Gross Rent)*. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:-

a) Mkataba haukufafanua maana ya Gross Rent, jambo linaloweza kusababisha tafsiri tofauti katika ukokotoaji wa mapato yanayostahili kulipwa UDSM;
b) Ongezeko la pango la kila *mwaka (annual escalation)* halikutekelezwa kwa mujibu wa masharti ya mkataba;
c) Utaratibu wa ukokotoaji wa malipo ya pango unaotumiwa na MHL
haukuzingatia kikamilifu masharti yaliyokusudiwa katika mkataba.

Mheshimiwa Spika, mapungufu hayo yanaweza kusababisha UDSM kukosa mapato yanayostahili kutona na upangishaji wa aradhi yake, kupunguza manufaa ya kifedha yanayotarajiwa kutokana na uwekezaji huo na kuibua migogoro kuhusu tafsiri na utekelezaji wa mkataba.

2.2.6.2 Mapungufu ya Masharti ya Mkataba wa MHL Kuhusu Hatima ya Mali Mwishoni mwa Kipindi cha Upangishaji

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa upangishaji wa ardhi kati ya UDSM na MHL una muda wa miaka 50. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa mkataba haujaweka bayana utaratibu wa kushughulikia masuala muhimu yatakayojitokeza mkataba utakapomalizika.Masuala hayo ni pamoja na:-

a) Hatima ya majengo na miundombinu iliyojengwa na kuendelezwa katika eneo la mradi;
b) Utaratibu wa kufanya tathmini ya thamani na hali ya majengo na miundombinu wakati wa kumalizika kwa mkataba; na
c) Haki na wajibu wa kila upande kuhusu mali hizo na utaratibu wa kukabidhi eneo na mali zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Oktoba 2026, Kamati ilikutana na Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na Menejimenti ya Chuo kwa lengo la kupata ufafanuzi kuhusu hoja za ukaguzi zilizobainika katika mkataba wa upangishaji wa ardhi kati ya UDSM na Mlimani City Holding Limited (MHL).

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya malipo ya ada ya upangishaji, Menejimenti ilieleza kuwa ukokotoaji wa malipo yaliyopendekezwa umekamilika na kuwasilishwa kwa mpangaji. Hata hivyo, mapitio ya mkataba yanaendelea kupitia timu ya

majadiliano iliyoteuliwa na Serikali ili kushughulikia mapungufu yaliyobainika na kuhakikisha maslahi ya Chuo yanalindwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya vihatarishi vinavyoweza kujitokeza mwishoni mwa mkataba, Menejimenti ilifafanua kuwa suala hilo linashughulikiwa na timu hiyo hiyo ya majadiliano kama sehemu ya mapitio ya mkataba. Hivyo, hoja zote mbili zinaendelea kufanyiwa kazi kupitia mchakato huo, na uhakiki wa utekelezaji utafanyika baada ya mapitio ya mkataba kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo yaliyotolewa na Menejimenti pamoja na mapungufu yaliyobainika katika usimamizi na utekelezaji wa mkataba huo, ni maoni ya Kamati kuwa, pamoja na Menejimenti kueleza kuwa mapitio ya mkataba yanaendelea kupitia timu ya majadiliano ya Serikali, mapungufu yaliyobainika katika ukokotoaji wa pango na kutokubainishwa kwa hatima ya majengo na miundombinu mkataba utakapomalizika yanaweza kusababisha Chuo kupoteza mapato yanayostahili na manufaa ya mali zake. Hivyo, kukamilika kwa mapitio ya mkataba ni muhimu katika kulinda maslahi ya kifedha na mali za Chuo kwa sasa na baadaye.Kamati imetoa mapendekezo ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha maslahi ya Chuo yanalindwa na vihatarishi vinavyohusiana na mkataba huo vinashughulikiwa ipasavyo. Mapendekezo ya Kamati kuhusu hoja hizo mbili yanapatikana katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii.

2.3 Uchambuzi wa Hoja za Udhibiti wa Ndani *(Internal Control Issues)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la udhibiti wa ndani, Kamati ilichambua hoja za ukaguzi zilizobainishwa katika Taarifa za CAG kwa lengo la kutathmini ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa fedha na mali, uidhinishaji wa miamala, utunzaji wa kumbukumbu na uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu, pamoja na hatua zilizochukuliwa na Taasisi husika kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika eneo hili kama ifuatavyo: -

2.3.1 Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani Katika Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC)

Mheshimiwa Spika, Katika Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), mambo makuu yaliyobainika yanahusu udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani, hususan katika usimamizi wa bidhaa na mali, matumizi ya mifumo ya TEHAMA, usimamizi wa madeni, uzingatiaji wa matakwa ya kodi, pamoja na taratibu za manunuzi na usimamizi wa mikataba, kama ifuatavyo:-

2.3.1.1 Udhaifu Katika Usimamizi wa Bidhaa Ghalani na Mali za Kampuni.

Mheshimiwa Spika, Kampuni iliendelea kutumia taratibu za kimaandishi katika usimamizi wa bidhaa ghalani licha ya kuwepo kwa Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi *(ERMS),* huku kukiwa hakuna mwongozo wa kina na ulioidhinishwa wa usimamizi wa bidhaa ghalani. Aidha, kulibainika kutokulingana kwa kumbukumbu za bidhaa pamoja na upungufu wa bidhaa wenye thamani ya Shilingi milioni 36.17. Hali hii inaonesha udhaifu katika udhibiti, ufuatiliaji na uwajibikaji wa bidhaa za Kampuni na kuongeza hatari ya upotevu wa mali.

2.3.1.2 Kutotumika Kikamilifu kwa Mifumo ya TEHAMA ya Kampuni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kampuni kuwa imenunua na kuanza kutumia mfumo wa *ERMS*, baadhi ya moduli muhimu za manunuzi, usimamizi wa mali na magari hazikuwa zikitumika kikamilifu. Hali hii inapunguza manufaa yaliyokusudiwa ya uwekezaji katika mfumo huo na inaweza kusababisha kuendelea kwa matumizi ya mifumo ya kizamani na kuongezeka kwa uwezekano wa makosa katika utunzaji wa kumbukumbu na udhibiti wa shughuli za Kampuni.

2.3.1.3 Udhaifu Katika Usimamizi na Ufuatiliaji wa Madeni ya Muda Mrefu

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, kulibainika kuwepo kwa madeni ya muda mrefu yenye thamani ya Shilingi bilioni 5.40, tofauti ya Shilingi milioni 100 kati ya kumbukumbu za madai na vitabu vya Kampuni, pamoja na salio la msamaha wa madeni la Shilingi bilioni 4.55 ambalo halikuwa limetatuliwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaashiria udhaifu katika upatanishaji wa kumbukumbu, uthibitishaji wa madeni na ufuatiliaji wa makusanyo, na inaweza kuathiri usahihi wa taarifa za fedha za Kampuni.

2.3.1.4 Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Matakwa ya Kodi na Udhibiti wa Malipo ya Wafanyakazi

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, ilibainika kuwa posho za watumishi zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.09 hazikutozwa Kodi ya Mapato (PAYE). Pamoja na uongozi kueleza kuwa umeomba mwongozo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania, suala hili linaonesha umuhimu wa kuwa na utaratibu madhubuti wa kuhakiki aina za malipo na wajibu wa kodi kabla ya malipo kufanyika, ili kuepusha madeni ya kodi, riba na adhabu zinazoweza kujitokeza.

2.3.1.5 Udhaifu Katika Uzingatiaji wa Taratibu za Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa ya CAG kuhusu TFC, ilibainika kwamba Kampuni ilitumia njia ya mzabuni mmoja katika ununuzi wa mbolea yenye thamani ya Shilingi bilioni 22.24 bila kuwepo kwa ushahidi wa kutosha wa uhalali wa matumizi ya njia hiyo. Aidha, mbolea yenye thamani ya Shilingi bilioni 12.49 ilipokelewa kabla ya mikataba husika kupitiwa kisheria na kusainiwa na wahusika.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaonesha mapungufu katika udhibiti wa mchakato wa manunuzi na utekelezaji wa mikataba, na inaweza kuongeza hatari ya Kampuni kufanya manunuzi yasiyo na ushindani au kuingia katika majukumu ya kimkataba bila ulinzi wa kutosha wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, ili kupata maelezo ya kina kuhusu hoja hizo nilizofafanua hapo awali, Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya TFC Dodoma siku ya tarehe 19 Agosti, 2026. kwa hoja ya mapungufu katika usimamizi wa bidhaa ghalani, Menejimenti ilifafanua kuwa itakamilisha mwongozo na mfumo wa ERMS/eKilimo ndani ya muda uliopangwa. Aidha, mtumishi aliyehusika na upotevu wa bidhaa wa Sh milioni 36.17 amechukuliwa hatua za kinidhamu, huku urejeshaji wa hasara ukiendelea kufuatiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja ya kutokutozwa PAYE kwa posho za watumishi zenye thamani ya Sh bilioni 2.09, Menejimenti ilieleza kuwa imeiandikia TRA kuomba ufafanuzi na itatekeleza maelekezo yatakayotolewa, ikiwemo kulipa kodi stahiki iwapo itabainika kudaiwa. Kuhusu hoja ya dosari katika madeni ya muda mrefu, Menejimenti ilieleza kuwa inaendelea kufanya ulinganisho na Wizara ya Fedha ili kuthibitisha madeni ya Sh bilioni 5.40, tofauti ya Sh milioni 100 na msamaha wa mkopo wa Sh bilioni 4.55 kabla ya kurekebisha taarifa za fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja ya kutotumika kikamilifu kwa mfumo wa *ERMS*, Menejimenti ilieleza kuwa imeiandikia eGA kukamilisha moduli zilizobaki ndani ya miezi mitatu kuanzia tarehe 15 Agosti 2026 na kurasimisha utaratibu wa msaada wa kiufundi.Kwa hoja ya ununuzi wa mbolea wa Sh bilioni 22.24 kwa kutumia utaratibu wa mzabuni mmoja bila uhalali wa kutosha, Menejimenti ilieleza kuwa itazingatia sheria na kanuni za ununuzi wa umma, na kwamba mpango wa ununuzi wa mwaka 2026/27 haujajumuisha manunuzi kwa utaratibu huo. Kuhusu hoja ya kupokea mbolea yenye thamani ya Sh bilioni 12.49 kabla ya mikataba kupitiwa kisheria na kusainiwa, Menejimenti ilieleza kuwa itahakikisha mikataba inakamilishwa kabla ya kupokea mbolea na mahitaji yote yanaingizwa katika Mpango wa Mwaka wa Ununuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hoja za ukaguzi zilizobainika pamoja na majibu na ufafanuzi wa Menejimenti, Kamati imetoa mapendekezo ya maboresho katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii, yanayolenga kuimarisha udhibiti wa ndani, uwajibikaji, uzingatiaji wa sheria na taratibu, pamoja na ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za Kampuni.

2.3.2 Uendeshaji wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF) Bila ya Kuwa na Muundo Rasmi wa Kiutendaji na Kiuwajibakaji

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF),Kamati imebaini hoja kadhaa zinazohusiana na mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kama ifuatavyo:-

2.3.2.1 Udhaifu Katika Muundo wa Kitaasisi na Mipango ya Kimkakati ya TACAF

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, Kamati imebaini kutokuwepo kwa muundo rasmi wa kitaasisi na Mpango Mkakati wa Mfuko wa Utamaduni Tanzania (TACAF). Mfuko hauna Sheria ya uanzishwaji inayoweka hadhi, muundo na majukumu yake kwa msingi wa kisheria. Aidha, Mfuko haukuwa na Mpango Mkakati wake wa kuongoza utekelezaji wa majukumu na shughuli zake, na hivyo kutegemea nyaraka na

miongozo mbalimbali ya Wizara, ikiwemo Mpango Mkakati wa Wizara, katika uendeshaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Mwakilishi wa CAG aliyotoa mbele ya Kamati akifafanua hoja hii kama ifuatavyo[11]:-

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema ni kwamba, huu Mfuko hauna sheria maalum iliyoanzisha kama Mifuko mingine unakuta sijui Road Fund, kuna Mfuko wa Maji, yaani mifuko kama hii ambayo inaanzishwa chini ya Consolidated Fund kwa ajili ya shughuli maalum. Kwa hiyo, huu haujawahi kuanzishwa na sheria maalum..."

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, Aidha,katika kupata maelezo ya ziada kuhusu hoja hii naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Sigmund Kisunga, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu (AAG – NAOT) aliyotoa mbele ya Kamati kama ifuatavyo[12]:-

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inayofuata pia kuhusu eneo la governance ni hoja namba

[11] Rejea Uk. 33 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 3 Tarehe 07 Agosti , 2026.

[12] Rejea Uk. 27 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 3 Tarehe 07 Agosti , 2026.

10; hawakuwa wameandaa Mpango Mkakati wa TACAF kwa maana ya Strategic Plan ili uendane pia na Mpango Mkakati wa Wizara. Wao wametujibu kwamba wanalifanyia kazi suala hili, wakishirikiana na Wizara ili mpango mkakati ukamilike na kuidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji. Kwa ambao watauandaa, utakuwa una-cover mwaka wa fedha wa 2025 hadi 2030. Kwa pendekezo hili lipo pia katika hatua za utekelezaji...”

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inaweza kusababisha kutokuwa na uwazi wa kutosha kuhusu mamlaka, majukumu na uwajibikaji wa TACAF, pamoja na kukosekana kwa mwelekeo mahsusi wa kimkakati, vipaumbele na viashiria vya kupima utekelezaji wa majukumu ya Mfuko. Pia, hali hiyo imeathiri ufanisi katika usimamizi wa rasilimali na utekelezaji wa programu zinazolenga kuwaendeleza wasanii na sekta ya utamaduni.

2.3.2.2 Madeni ya Muda Mrefu ya Mikopo kwa Wasanii Sh. 765,935,433

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF) ulikuwa na madeni ya mikopo ya muda mrefu yanayodaiwa kutoka kwa wasanii yenye jumla ya Sh. 765,935,433, yaliyotokana na mikopo iliyotolewa katika miaka ya fedha 2022/23 na 2023/24.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya mikopo hiyo haikurejeshwa kwa wakati, hali inayoashiria changamoto katika usimamizi na ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo. Aidha, madeni hayo yanapodumu kwa muda mrefu hufunga fedha za Mfuko, kupunguza uwezo wa kutoa mikopo kwa wasanii wengine na kuongeza hatari ya kutorejeshwa kwa fedha hizo.

2.3.2.3 Ukosefu wa Mfumo wa Kielektroniki Katika Usimamizi wa Mikopo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF) hauna mfumo wake wa kielektroniki wa kusimamia mikopo na shughuli za kibiashara, na badala yake unategemea miundombinu na mifumo ya benki washirika, NBC na CRDB, katika uchakataji, utoaji na usimamizi wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inasababisha changamoto katika usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo, ikiwemo upatikanaji wa taarifa za mikopo kwa wakati, ufuatiliaji wa marejesho na udhibiti wa taarifa za wanufaika. Aidha, kukosekana kwa mfumo unaowawezesha wasanii kuomba mikopo moja kwa moja kunaweza kuongeza utegemezi wa taratibu za nje ya Mfuko hivyo kuathiri ufanisi wa upatikanaji wa huduma za mikopo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Mfuko unakabiliwa na hatari ya kuchelewa kubaini mikopo iliyochelewa au isiyorejeshwa, udhaifu katika ufuatiliaji wa marejesho, upungufu

wa ufanisi katika usimamizi wa taarifa za mikopo, pamoja na kuchelewa kuwafikia wanufaika wengine wanaohitaji mikopo.

2.3.2.4 Kushindwa kwa Wadaiwa Kurejesha Mikopo na Kusababisha TACAF Kubeba Dhamana ya Sh. 88,325,998

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa TACAF ililazimika kubeba wajibu wa kifedha kutokana na wadaiwa wa mikopo kushindwa kurejesha mikopo waliyopewa, hali iliyosababisha makato ya jumla ya Sh.88,325,998 kutoka kwenye akaunti ya TACAF iliyokuwa CRDB Bank PLC. Makato hayo yalifanyika kwa mujibu wa utaratibu wa dhamana ya mikopo ambapo TACAF ilikuwa mdhamini wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya ukaguzi inabainisha kuwa tukio hilo linaashiria udhaifu katika usimamizi wa mikopo na ufuatiliaji wa wadaiwa, hususan katika kuhakikisha marejesho ya mikopo yanafanyika kwa wakati. Aidha, kubeba wajibu wa kulipa madeni ya wadaiwa kupitia fedha za TACAF kunaonesha kuwa utaratibu wa kutathmini uwezo wa wakopaji kurejesha mikopo pamoja na ufuatiliaji wa mikopo iliyodhaminiwa haukuwa madhubuti. Hali hii pia inaongeza hatari ya TACAF kutumia fedha zake za uendeshaji kulipia madeni ambayo kimsingi yalipaswa kulipwa na wadaiwa.

Mheshimiwa Spika, makato ya Sh. 88,325,998 yalisababisha upungufu wa fedha za TACAF na kupunguza uwezo wa Mfuko

kutumia rasilimali zake kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa. Aidha, endapo madeni hayo hayatadhibitiwa na kurejeshwa kutoka kwa wadaiwa, TACAF inaweza kuendelea kupata hasara na kudhoofisha mtaji na uendelevu wa mfumo wa dhamana ya mikopo.

2.3.2.5 Kutoteuliwa kwa Bodi ya Wadhamini baada ya Kumalizika kwa Muda wa Uongozi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa muda wa uongozi wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF) ulimalizika tarehe 24 Julai 2024, lakini hadi wakati wa ukaguzi mwezi Oktoba 2025, Bodi mpya haikuwa imeteuliwa. Hali hii ni kinyume na matakwa ya *Ibara ya 6.1 ya Trustees Incorporation Ordinance, Cap. 318*, inayotaka Mfuko kuwa na Bodi ya Wadhamini yenye wajumbe saba wanaoteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Utamaduni na Sanaa kwa kipindi cha miaka mitatu, kinachoweza kuongezwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, Kutoteuliwa kwa Bodi kwa wakati kuliifanya TCAF kuendelea kufanya kazi bila chombo kamili cha usimamizi kwa kipindi kirefu, jambo lililoathiri usimamizi wa shughuli za Mfuko, uelekeo wa kimkakati na uwajibikaji.

2.3.2.6 Ununuzi wa Bidhaa na Huduma Nje ya Mfumo wa NeST wa TZS 30,756,700

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa TCAF ilifanya ununuzi wa bidhaa na huduma wenye thamani ya Sh. 30,756,700 nje ya

Mfumo wa Taifa wa Kielektroniki wa Ununuzi (NeST) katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2025. Hali hiyo ni kinyume na Waraka Na. 2 wa 2023/24, Wenye Kumb. Na. PST/GEN/2023/01/67 wa tarehe 27 Julai 2023, uliotolewa na Wizara ya Fedha na kuagiza Taasisi zote za Serikali kutumia NeST katika ununuzi wa bidhaa na huduma kuanzia tarehe 1 Oktoba 2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa kutotumia mfumo huo kulitokana na udhaifu katika usimamizi na utekelezaji wa matakwa ya matumizi ya NeST. Hali hiyo inaweka Mfuko katika hatari ya kupungua kwa uwazi wa michakato ya ununuzi, udhaifu wa kumbukumbu za ukaguzi, kupungua kwa ushindani na kutokidhi kikamilifu matakwa ya Serikali kuhusu matumizi ya NeST.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli wa Mfuko wa TACAF tarehe 07 Agosti, 2026 Ofisi ya Bunge Dodoma ili kupata ufafanuzi wa hoja za CAG na hatua ambazo zimechukuliwa ili kuondoa mapungufu yaliyobainishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuchelewa kurejeshwa kwa mikopo, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa, TACAF ilianza kutoa mikopo tarehe 22 Desemba 2022 na, katika kipindi cha tarehe 22 Desemba 2022 hadi 2 Februari 2023, ilitoa mikopo kwa wasanii 45 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.077. Mikopo hiyo ilitolewa bila kudai dhamana kwa lengo la kuwawezesha wasanii

wadogo, wachanga na wale ambao hawakuwa na uwezo wa kupata mikopo kupitia mfumo wa kawaida wa kibenki.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli alikiri kuwepo kwa changamoto za marejesho ambapo hadi wakati wa majadiliano, TACAF ilikuwa inadai Sh. milioni 765 kutoka kwa wakopaji. Alieleza kuwa changamoto hiyo ilitokana kwa kiasi kikubwa na kutokuwepo kwa utaratibu wa kudai dhamana wakati wa utoaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli alieleza kuwa TACAF imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha madeni hayo yanarejeshwa, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wadaiwa kuhusu marejesho, kupanga upya muda wa marejesho ya mikopo, kutumia kampuni za ukusanyaji madeni (debt collectors), pamoja na kuwasilisha taarifa za wadaiwa sugu katika "Credit Reference Bureau" ili kuwazuia kupata mikopo kutoka taasisi nyingine za fedha hadi watakapokamilisha marejesho ya mikopo ya TACAF.Aidha, Afisa Masuuli alieleza kuwa kutokana na changamoto hizo, TACAF imebadili mfumo wa utoaji wa mikopo kwa kushirikiana na taasisi za fedha, ikiwemo NBC na CRDB, ili kuimarisha usimamizi na urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika , kwa hoja na jitihada zinazochukuliwa kurejesha mikopo hiyo, naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Gerson Msigwa, Katibu Mkuu – Wizara ya Habari, Sanaa,

Utamaduni na Michezo aliyoyatoa mbele ya Kamati kama ifuatavyo[13]:-

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilitaka nikuombe wewe na Waheshimiwa Wajumbe, ni kweli hizi changamoto zimejitokeza tumejifunza na hizi hatua tulizochukua sasa hivi zimeshatuonesha kwamba zina ufanisi, sababu fedha zinazoenda zinarudi..."

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja ya kutotumia mfumo wa NEST katika manunuzi, Afisa Masuuli alieleza kuwa TACAF haikutumia mfumo wa NeST katika baadhi ya manunuzi kutokana na changamoto za kiutendaji zilizokuwepo wakati huo, ikiwemo kutokuwa na baadhi ya miundombinu na watumishi muhimu kwa ajili ya kuendesha mfumo wa manunuzi, kama vile Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Mwanasheria wa Taasisi na Afisa Manunuzi. Aidha, Afisa Masuuli alieleza kuwa baada ya kubaini hoja hiyo, TACAF ilichukua hatua kwa kuwasiliana na Wizara inayosimamia Mfuko.

[13] Rejea Uk. 65 - 66 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 3 Tarehe 07 Agosti , 2026.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliwasiliana na PPRA kwa ajili ya kupata idhini ya TACAF kutumia mfumo wa manunuzi wa Wizara katika kutekeleza manunuzi yake. Afisa Masuuli alieleza kuwa wakati wa majadiliano, TACAF ilikuwa inasubiri majibu ya PPRA kuhusu ombi hilo ili kuweza kutumia mfumo wa manunuzi wa Wizara kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa na huduma za Mfuko.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli alieleza kuwa TACAF haina muundo rasmi wa uendeshaji kutokana na kutokuwa na sheria ya uanzishwaji, hali inayochangia upungufu wa watumishi. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Mfuko uliwasilisha andiko la kujiendesha kama Wakala kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora mwezi Machi 2026. Baada ya kupokea maoni mwezi Julai 2026, Mfuko uliunda kikosi kazi cha kutekeleza mapendekezo hayo kuanzia Agosti hadi Septemba 2026**,** kabla ya kuwasilisha matokeo kwa Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya kutokuwepo kwa Mpango Mkakati, Afisa Masuuli alieleza kuwa TACAF haikuwa na Mpango Mkakati na hivyo ilitumia nyaraka na miongozo ya Wizara katika utekelezaji wa shughuli zake. Hata hivyo, Mfuko umeandaa Mpango Mkakati ambao umewasilishwa Wizarani kwa ajili ya mapitio ya mwisho, na ulitarajiwa kukamilika na kuanza kutumika mwezi Agosti, 2026.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, licha ya hatua zilizochukuliwa na TACAF, Mfuko bado unakabiliwa na changamoto za kimuundo, kiutawala na kiutendaji, ikiwemo kutokuwepo kwa Sheria ya uanzishwaji, Bodi ya Wadhamini, madeni ya mikopo ya Sh. milioni 765.94 na udhaifu wa mifumo ya usimamizi wa mikopo na ununuzi. Hali hiyo inaathiri uwajibikaji na uendelevu wa Mfuko, hivyo Wizara inapaswa kuhakikisha mapungufu hayo yanatatuliwa kwa wakati ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali na utekelezaji wa majukumu ya TACAF.

2.4 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi Zinazohusu Utendaji *(Performance/ Value for Money Issues)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la utendaji na thamani ya fedha, Kamati ilichambua hoja za ukaguzi katika Taarifa za CAG ili kutathmini ufanisi na tija ya matumizi ya rasilimali za umma, utekelezaji wa mipango, miradi na programu za Serikali kwa kuzingatia muda, gharama, viwango na malengo yaliyowekwa, pamoja na uwiano kati ya rasilimali zilizotumika na matokeo yaliyopatikana.Aidha, Kamati ilitathmini changamoto zilizojitokeza, zikiwemo ucheleweshaji wa miradi, ongezeko la gharama, na kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, pamoja na hatua zilizochukuliwa na Taasisi husika kurekebisha mapungufu hayo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa hoja za Kamati katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

2.4.1 Uchambuzi Kuhusu Hali ya Kifedha na Utendaji wa Benki ya Kilimo Tanzania (TADB)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Taarifa za Fedha za Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2025, pamoja na maelezo yaliyotolewa na Menejimenti na Mkaguzi kuhusu mwenendo wa mali, madeni, mtaji, faida na uwiano muhimu wa kifedha wa Benki.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mali za TADB ziliongezeka kwa asilimia 41 na mikopo iliyotolewa kufikia Shilingi bilioni 451, huku faida ikiongezeka kwa asilimia 50 hadi Shilingi bilioni 27 na ubora wa mikopo kuimarika. Hata hivyo, madeni yaliongezeka kwa asilimia 85, gharama za riba kwa asilimia 99 na gharama za uendeshaji kuongezeka kutokana na upanuzi wa shughuli za Benki. Aidha, uwiano wa gharama dhidi ya mapato ulipanda kutoka asilimia 44.3 hadi 49.6, ingawa uliendelea kuwa chini ya kiwango cha asilimia 55 kinachokubalika. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuimarisha udhibiti wa gharama na usimamizi wa madeni ili kudumisha tija na ukuaji endelevu wa Benki.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa viashiria muhimu vya utendaji wa TADB, uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yenye changamoto ambayo TADB inatakiwa kuyafanyia kazi kwa haraka, maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

2.4.1.1 Mapungufu katika Usimamizi na Uthibitishaji wa Dhamana za Mikopo

Mheshimiwa Spika, CAG alibaini udhaifu katika usimamizi wa dhamana zinazowekwa na wateja wanaokopa kutoka TADB. Katika sampuli ya dhamana 30 zilizopitiwa, dhamana 8, sawa na asilimia 27%, zilikuwa zimeishiwa muda wa bima (*insurance*). Aidha, kulibainika dhamana moja ambayo haikufanyiwa uthamini (*revaluation)* kwa wakati uliotakiwa. Hali hii inaweka Benki katika hatari ya kupata hasara endapo dhamana hizo zitaharibika au thamani yake kushuka na mkopaji kushindwa kulipa.

2.4.1.2 Mapungufu katika Mfumo wa Kukadiria Hasara Zinazotarajiwa kutokana na Mikopo

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini mapungufu katika vigezo, dhana na maamuzi yanayotumiwa na Benki kukadiria hasara zinazoweza kutokea kutokana na mikopo *(Expected Credit Loss – ECL*). Mapungufu hayo yalihusu namna ya kukadiria hasara kwenye ahadi za mikopo *(commitments)*, kiwango cha hasara kinachoweza kutokea mkopaji anaposhindwa kulipa *(Loss Given*

Default – LGD), na tathmini ya mali zenye hatari ndogo ya mikopo. Mapungufu hayo yanaweza kusababisha Benki kukadiria hasara kwa kiwango kisicho sahihi na hivyo kuathiri uwasilishaji wa taarifa zake za fedha.

2.4.1.3 Kutokuwepo kwa Mkataba wa (*On-Lending Agreement)* kwa Mkopo wa JICA wa Sh. Bilioni 354

Mheshimiwa Spika,uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG ulibaini kuwa, licha ya Serikali kuwa imesaini mkataba na JICA wa mkopo wa Yen bilioni 22, sawa na takribani Sh. bilioni 354, na TADB kutajwa kama mtekelezaji *(implementing agency),* wakati wa ukaguzi mkataba wa (*On-Lending Agreement)* kati ya Serikali na TADB ulikuwa haujasainiwa.Aidha, TADB ilikuwa tayari imepokea malipo ya kwanza ya Sh. bilioni 183. Hivyo kamati iliona hii ni hoja muhimu ya uzingatiaji wa masharti ya mkataba na mfumo wa kisheria/kimaandishi wa uendeshaji wa fedha hizo.

2.4.1.4 Kutotumia Mifumo ya Serikali ya HCMIS na PEPMIS

Mheshimiwa Spika, taarifa ya CAG ilibainisha kuwa TADB ilikuwa bado haijatekeleza kikamilifu matumizi ya mifumo miwili ya masuala ya kiutumishi, ambayo ni *Human Capital Management Information System (HCMIS)* na *Performance Management Information System (PEPMIS*), licha ya Serikali kuwa katika mchakato wa kuoanisha matumizi ya mifumo hiyo

katika taasisi zake zote. Hoja hii ilikuwa imeshajitokeza katika miaka iliyopita na bado ilikuwa katika hatua za utekelezaji wakati wa ukaguzi mwaka 2024/2025.

2.4.1.5 Tofauti katika Uamuzi wa Kushughulikia Hasara ya Mikopo Inayotarajiwa *(Expected Credit Loss)* kati ya Matakwa ya IFRS na Miongozo ya BOT

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyoibuliwa na CAG ilihusu uwepo wa tofauti kati ya matakwa ya IFRS na miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania (BOT) katika namna ya kukokotoa hasara ya mikopo inayotarajiwa (*Expected Credit Loss)* kwa mikopo chechefu. Kwa mwaka uliokaguliwa, tofauti hiyo ilikadiriwa kuwa Shilingi milioni 256. Ingawa kiasi hicho hakikuwa kikubwa kiasi cha kuathiri hati ya ukaguzi (*audit opinion)*, hoja iliendelea kuwa katika hatua za utekelezaji kutokana na haja ya Benki kuendelea kudhibiti ongezeko la mikopo chechefu na athari zinazoweza kutokana na tofauti hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maeneo hayo matano ambayo yalibainishwa katika hesabu za TADB, Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya TADB siku ya tarehe 04 Agosti, 2026 ili kujadili hoja hizo na hatua ambazo Benki imechukua ili kulinda fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilihusu matumizi ya mifumo ya HCMIS na PEPMIS. Menejimenti ya TADB ilieleza kuwa utekelezaji wa mifumo hiyo ulicheleweshwa kutokana na

haja ya kufanya ulinganifu wa mifumo na uhakiki wa taarifa za watumishi, zoezi ambalo limekamilika. Hivyo, Benki ilitarajia kuanza kutumia mifumo hiyo mwezi Agosti 2026.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu fedha zilizokopwa kutoka JICA ambapo hapakuwa na mkataba kati ya Serikali na TADB kuhusu mkopo huo. Naomba kunukuu sehemu ya swali la Mhe. Thomas M. Allan, Mbunge, Mjumbe wa PAC aliyetaka kupata maelezo kuhusu hoja hiyo kama ifuatavyo[14]:-

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yako ilipokea taarifa kutoka kwa CAG, ambayo ilisema kwamba tarehe 14 ya mwezi Januari, 2025 Serikali yetu ilipokea mkopo wenye thamani ya Shilingi bilioni 354.3 kutokea JICA. Sasa baada ya hapo shilingi bilioni 183 zikawa zimepelekwa kwenye benki ya TADB tarehe 18 ya mwezi wa Sita mwaka wa 2025. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya kutoka kwa CAG ni kwamba hadi sasa hakuna mkataba rasmi kati ya Benki ya TADB na Serikali yetu, kwa maana ya Wizara ya Fedha ambao waliwapatia fedha hizo.., zaidi ya yote hadi kufikia tarehe 31 mwezi Disemba mwaka 2025 tayari Benki ya TADB ilishatoa takribani shilingi bilioni 17.7 kwa wanufaika kama mikopo kutoka kwenye fedha zile zile ambazo benki haina mkataba na Serikali.,..."

Mwisho wa Nukuu.

[14] [14] Rejea Uk. 68 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 3 Tarehe 04 Agosti , 2026.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya TADB ilifafanua kuwa tarehe 14 Januari 2025 ilikuwa ni tarehe ya kusaini mkataba wa mkopo wa JICA na siyo tarehe ya kupokea fedha. Benki ilipokea awamu ya kwanza ya mkopo wa Shilingi bilioni 183 tarehe 18 Juni 2025. Aidha, ilieleza kuwa rasimu ya mkataba wa makubaliano ya urejeshaji wa mkopo (On-lending Agreement) kati ya Serikali na TADB ilikuwa imeandaliwa, na majadiliano kati ya Benki na Wizara ya Fedha yalikuwa katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Frank Nyabundege – Mkurugenzi Mwendeshaji (TADB) aliyotoa mbele ya Kamati kuhusu hoja hii kama ifuatavyo[15]:-

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri mpaka kufikia mwisho wa mwaka mkataba huu utakuwa umeshasainiwa, na ni kawaida mara nyingi huu mkataba wa ambaye ni on landing inachukua muda kwa sababu unakuwa ni mkataba wetu wa ndani, lakini ule mkataba mama ulishasainiwa kati ya JICA na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania..."

Mwisho wa Nukuu.

[15] [15] Rejea Uk. 69 - 70 wa Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 3 Tarehe 04 Agosti , 2026.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya TADB ilikiri kuwepo kwa udhaifu katika ufuatiliaji wa uthamini na bima za dhamana kutokana na kuongezeka kwa mikopo na matumizi ya mfumo wa usiokuwa wa kidijitali. Benki imeanza kutumia mifumo ya kidijitali, ambapo mfumo wa uthamini ulitarajiwa kukamilika Septemba 2026 na wa bima Desemba 2026. Aidha, baadhi ya bima zilizobainika kutokuwa halali zilihuishwa baada ya ukaguzi, na Benki imechukua hatua za kuimarisha ufuatiliaji ili kuhakikisha uthamini na bima vinafanywa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya TADB ilieleza kuwa upungufu katika mfumo wa kukadiria hasara zinazotarajiwa za mikopo (ECL) umeshughulikiwa kwa kushirikisha mshauri wa kitaalamu. Moduli mpya imekamilika na ipo katika hatua ya majaribio kwa kutumia takwimu za miezi mitatu, ikitarajiwa kukamilika Oktoba 2026 kabla ya ukaguzi unaofuata.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, licha ya TADB kuimarika kwa mali, mikopo na faida, bado kuna changamoto katika usimamizi wa dhamana, ukadiriaji wa hasara za mikopo na kutokamilika kwa mkataba wa mkopo wa JICA wa Sh. bilioni 354. Aidha, kutokamilika kwa matumizi ya mifumo ya HCMIS na PEPMIS kunahitaji hatua za haraka. Hivyo, ni muhimu Menejimenti ya TADB kukamilisha hatua zilizopangwa kwa wakati, kuimarisha udhibiti wa hatari za mikopo na kuhakikisha fedha za umma zinasimamiwa kwa ufanisi na uwajibikaji. Kamati

imezingatia hoja za ukaguzi za CAG na majibu ya Menejimenti ya TADB na kutoa mapendekezo ya maeneo ya maboresho katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii.

2.4.2 Changamoto Zinazoikabili Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama – Shinyanga (KASHWASA)

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25, Kamati ilibaini kuwa KASHWASA inaendelea kukabiliwa na changamoto katika ukusanyaji wa madeni, usimamizi wa miradi, pamoja na ulinzi wa miundombinu ya maji. Kamati ilifanya uhakiki wa utekelezaji wa hoja hizo tarehe 13 Agosti 2026 na kubaini kuwa baadhi ya changamoto zimeendelea na nyingine zimeongezeka. Hoja muhimu ambazo Kamati imeona zinapaswa kuwasilishwa kwa Bunge ni kama ifuatavyo:-

2.4.2.1 Kuongezeka kwa Deni la Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira hadi Shilingi Bilioni 20.15

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2024/25, Mamlaka nane za Majisafi na Usafi wa Mazingira zilikuwa na deni la Sh. bilioni 15.36 kutokana na kutolipa Ankara za huduma ya maji zinazotolewa na KASHWASA. Hata hivyo, uhakiki uliofanyika tarehe 13 Agosti 2026 ulionesha kuwa deni hilo limeendelea kuongezeka na kufikia Sh. bilioni 20.15, sawa na ongezeko la Sh. bilioni 4.79.

Mheshimiwa Spika, Kamati kupitia uchambuzi wa kina wa taarifa ya CAG imebaini kuwa ongezeko hili la madeni linaathiri ukwasi wa KASHWASA na uwezo wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake, ikiwemo kulipa gharama za huduma za umeme.

2.4.2.2 Kuongezeka kwa Deni la Vyombo 122 vya Huduma za Maji Vijijini (CBWSOs) Hadi Shilingi Bilioni 2.32

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa katika ukaguzi wa mwaka 2024/25, Vyombo 122 vya Huduma za Maji Vijijini (CBWSOs) vilikuwa na deni la Sh. bilioni 1.66. Hata hivyo, wakati wa uhakiki tarehe 13 Agosti 2026, deni hilo lilikuwa limeongezeka na kufikia Sh.bilioni 2.32, sawa na ongezeko la Sh. milioni 668.72.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa KASHWASA na CBWSOs ziliingia makubaliano tarehe 30 Machi 2026 ya kulipa Ankara za kila mwezi na wakati huo huo kupunguza madeni yaliyokusanyika. Pamoja na hatua hiyo, ongezeko la deni linaonesha kuwa utekelezaji wa makubaliano hayo bado unahitaji ufuatiliaji wa karibu.

2.4.2.3 Kuongezeka kwa Malimbikizo ya Deni la Umeme hadi Shilingi Bilioni 7.43

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa KASHWASA ilikuwa na malimbikizo ya deni la umeme ya Shilingi bilioni 6.45 wakati

wa ukaguzi wa mwaka 2024/25. Hata hivyo, uhakiki uliofanyika tarehe 13 Agosti 2026 ulionesha kuwa deni hilo limeendelea kuongezeka na kufikia Sh. bilioni 7.43 hadi tarehe 30 Juni 2026, sawa na ongezeko la Sh. milioni 975.29.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa hali hii inaonesha changamoto ya ukwasi katika KASHWASA, inayochangiwa kwa kiasi kikubwa na kutokusanywa kwa wakati kwa madeni kutoka kwa wateja wake.

2.4.2.4 Kuchelewa kwa Utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Mhalo–Ngudu Wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 6.29

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Mradi wa Maji wa Mhalo–Ngudu wenye thamani ya Shilingi bilioni 6.29 ulikuwa umefikia asilimia 5 ya utekelezaji wakati wa ukaguzi wa mwaka 2024/25, licha ya Mkandarasi kuwa amelipwa malipo ya awali ya Sh. milioni 943.37. Hata hivyo, wakati wa uhakiki tarehe 13 Agosti 2026, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 40, lakini Mkandarasi hakuwepo katika eneo la mradi na alikuwa ameondoa vifaa vyake kutokana na kutolipwa madai yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini pia kuwa madai ya Mkandarasi yaliyowasilishwa kupitia Hati Na. 1 yalifikia Sh. bilioni 2.14. Kusimama kwa utekelezaji wa mradi kunaweza kucheleweshe upatikanaji wa huduma na manufaa yaliyokusudiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchambua hoja za ukaguzi na majibu ya Bodi ya KASHWASA, Kamati ina maoni kuwa madeni ya wateja, malimbikizo ya deni la umeme na kusimama kwa Mradi wa Maji wa Mhalo–Ngudu vinaathiri ukwasi wa Mamlaka na kuchelewesha utekelezaji wa majukumu yake, hali inayoweza kuhatarisha uendelevu wa huduma za maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetoa mapendekezo katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii kwa lengo la kuimarisha hali ya ukwasi na utendaji wa KASHWASA, pamoja na kuhakikisha Serikali inachukua hatua stahiki na kwa wakati katika kushughulikia changamoto za kifedha zinazoikabili Mamlaka hiyo.

2.4.3 Uchambuzi wa Taarifa ya CAG Kuhusu Mafanikio, Changamoto na Hatua za Kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua hoja zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu mwenendo wa uendeshaji na mchakato wa kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL). Uchambuzi wa Kamati umejikita katika maeneo ya msingi kama ifuatavyo:-

2.4.3.1 Kuongezeka kwa Wadaiwa na Kufungia Mtaji wa Uendeshaji

Mheshimiwa Spika, CAG alibaini kuwa hadi tarehe 30 Juni 2025, ATCL ilikuwa na wadaiwa wa kibiashara wenye thamani ya Shilingi milioni 139,232 (takribani Shilingi bilioni 139.2), ikiwa ni ongezeko la asilimia 55 kutoka Shilingi milioni 89,811 hadi tarehe 30 Juni 2024. Aidha, salio hilo lilikuwa limeongezeka pia kutoka Shilingi milioni 57,915 mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa ongezeko endelevu la madeni ya wadaiwa lina athari katika mtiririko wa fedha na uwezo wa ATCL kugharamia shughuli zake za kila siku, kwa kuwa fedha ambazo zingetumika katika uendeshaji wa Shirika zinabaki mikononi mwa wadaiwa. Hali hii ni muhimu kuzingatiwa katika mchakato wa kulifanya ATCL kuwa na ufanisi na uendelevu wa kifedha.

2.4.3.2 Utoaji wa Mikopo Mipya kwa Wateja Wenye Madeni ya Awali

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa ya pili kuhusu ufanisi wa ATCL,CAG alibaini kuwa katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025, ATCL ilitoa mikopo mipya yenye thamani ya Sh. 36.13 bilioni kwa wateja 592 ambao tayari walikuwa na madeni ya awali yenye thamani ya Sh. 80.26 bilioni. Katika kipindi hicho, ni Sh. 6.81 bilioni pekee zilizokusanywa kutoka katika madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa utoaji wa mikopo mipya kwa wateja ambao tayari wana madeni yaliyochelewa kulipwa unaongeza hatari ya kuongezeka kwa madeni yasiyokusanywa na kuathiri zaidi mtiririko wa fedha wa ATCL. Pia, hali hiyo inaonesha umuhimu wa kuwa na mfumo madhubuti wa tathmini ya uwezo wa mteja kulipa kabla ya kuidhinisha mikopo au huduma za malipo ya baadaye.

2.4.3.3 Kupungua Kwa Sehemu ya Soko Kutokana na Ushindani

Mheshimiwa Spika, CAG alibainisha kuwa ATCL imekabiliwa na kupungua kwa sehemu ya soko kutokana na kuongezeka kwa ushindani kutoka kwa waendeshaji wengine wa usafiri wa anga. Kamati imebaini kuwa ongezeko la idadi ya ndege na uwezo wa kutoa huduma halijaondoa changamoto ya ushindani, kwani mafanikio ya Shirika yanategemea pia uwezo wa kuvutia abiria, ubora wa huduma, ufanisi wa ratiba na tija ya njia za safari. Hali hii inaweza kusababisha ndege kutotumika kikamilifu, kupungua kwa mapato na tija ya uwekezaji wa Serikali, na kudhoofisha uwezo wa Shirika kushindana katika soko la ndani na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ili kupata majibu ya Serikali kwa hoja zilizoibuliwa na CAG, Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya ATCL siku ya 05 Agosti, 2026 Ofisi ya Bunge Dodoma.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza iliyofafanuliwa na ambayo kwa kiasi kikubwa inahusaina na madeni amabyo ATCL inadaiwa kwa muda mrefu ilihusu kukamilika kwa mchakato wa kuhamisha umiliki wa ndege kutoka Wakala wa wa Ndege za Serikali kwenda ATCL.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilifahamishwa kuwa mchakato wa kuhamisha umiliki wa ndege kutoka TGFA kwenda ATCL umekamilika na ulifanyika kwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 158 la tarehe 26 Juni, 2026.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni la muhimu sana na Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri wa CAG na Bunge katika jambo hili ambao umekuwa ukitolewa kwa muda mrefu. Kukamilika kwa mchakato huu kutatoa fursa muhimu ya ATCL kusafisha mizania ya hesabu zake.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu sehemu ya maelezo Mheshimiwa Aeshi K.Hilaly,Makamu Mwenyekiti (PAC) kuhusu hoja hii wakati wa mahojiano ya Kamati na Bodi na Menejimenti ya ATCL. Sehemu ya nukuu ya swali la Mhe. Aeshi K. Hilaly kwenda kwa Mkaguzi toka kwa CAG alisema[16]:-

[16] Rejea Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Uk. 107, Kikao cha 3, Tarehe 05 Agosti, 2026.

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka arudie hili agizo namba moja. Umeenda kuhakiki kwamba tayari uamuzi huu wa kuhamisha ndege kutoka kwa hii taasisi ya Serikali kwenda ATCL?..."

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, akijibu swali hilo, Ndugu Azizi Dachi, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (AAG) alitoa maelezo kama sehemu ya maelezo hayo alisema[17]:-

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nichukue swali hilo kulielezea kwamba, maamuzi ya Serikali kuhamisha yamefanyika, na ukiangalia ndiyo hiyo tunayoitaja hapo GN No. 158. Hata hivyo, yale maamuzi huwa yanafuatishwa na kuhakikisha kwamba zile taarifa zina-reflect kwenye kitabu cha hesabu sasa. Sasa hiyo ndiyo bado, lakini maamuzi yale ya msingi ya ndege zihamishwe, imefanyika na evidence yake ni hiyo GN 158. Katika ukaguzi huu unaofuata, tutaangalia sasa jinsi ambavyo ilikuwa reported i-reflect decision hii, ndiyo kilichobaki, ahsante..."

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya ziada kuhusu uhamishaji wa ndege kutoka TGFA kwenda ATCL yalitolewa na Mtendaji Mkuu

[17] Rejea Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Uk. 108, Kikao cha 3, Tarehe 05 Agosti, 2026.

wa ATCL Ndugu Peter Ulanga. Sehemu ya nukuu ya maelezo yake mbele ya Kamati alisema[18]:-

Nukuu:-

> ***"...Mheshimiwa Mwenyekiti, nyaraka ya mwisho kabisa ni ya uhamishaji wa ndege ambayo ndiyo hiyo GN iliyotoka. Kwa hiyo, as we are speaking ni kwamba ndege zipo katika umiliki wa Air Tanzania. Kuna kazi za kihasibu za kubadilisha asset register kuingia kwenye asset register ya Serikali kuweza kubadilisha, hizo zinaendelea kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)…"***

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya ATCL ilieleza kuwa hasara za Kampuni zimeanza kupungua kufuatia kufufua ndege 16 zilizokuwa chakavu na kuzirejesha katika huduma. Aidha, Kampuni inaendelea kupanua mtandao wa safari kwa kuongeza njia za ndani ya nchi, ikiwemo Geita, Iringa na Mtwara, pamoja na njia za kimataifa za Victoria Falls, Cape Town na Seychelles, hatua zinazolenga kuongeza mapato na kupunguza hasara.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya ATCL ilieleza kuwa imeimarisha usimamizi wa madeni kwa kuzuia utoaji wa mikopo mipya kwa wateja wenye madeni yaliyochelewa kulipwa hadi watakapolipa. Hatua hizo zimechangia kupungua kwa salio la

[18] Rejea Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Uk. 159, Kikao cha 3, Tarehe 05 Agosti, 2026.

wadaiwa wa kibiashara kutoka Shilingi bilioni 139 hadi Shilingi bilioni 111 kufikia tarehe 30 Juni 2026. Aidha, ukaguzi wa ankara za baadhi ya wateja umebaini kuwa riba hutozwa kutokana na ucheleweshaji wa malipo.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya ATCL ilieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2024/25, Kampuni ilipata hasara ya Shilingi bilioni 191, huku gharama za ukodishaji wa ndege zikiwa Shilingi bilioni 142 na gharama za akiba ya matengenezo zikiwa Shilingi bilioni 58. Menejimenti ilieleza kuwa kuhamia kutoka mfumo wa ukodishaji wa ndege kunatarajiwa kupunguza gharama hizo na hivyo kupunguza hasara katika kipindi kinachofuata.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ilieleza kuwa ATCL inalenga kufikia kiwango cha kutokuwa na hasara wala faida (*break-even*) katika mwaka wa fedha unaofuata (2026/2027), na baada ya hapo kuanza kupata matokeo chanya ya kifedha yatakayochangia katika kuboresha hali ya kifedha ya Kampuni na kuongeza mchango wake katika mapato ya Serikali. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Peter Ulanga – Mtendaji Mkuu (ATCL) aliyotoa mbele ya Kamati kwa hoja hii alisema[19]:-

[19] Rejea Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Uk. 176, Kikao cha 3, Tarehe 05 Agosti, 2026.

Nanukuu

"...Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ninaomba nikizungumze, ukiangalia sura ya hasara ya Air Tanzania, moja ya eneo ambalo lilikuwa linaongeza sana inaonekana kwamba gharama ni kubwa, ni zile gharama za ukodishaji wa ndegeKatika mwaka wa 2024/2025 ambao mnaujadili, hasara yake inaonekana pale ni shilingi bilioni 191 lakini katika zile shilingi bilioni 191, zaidi ya shilingi bilioni 142 ni gharama za ukodishaji wa ndege na shilingi bilioni 58 ni gharama zinaitwa akiba ya matengenezo. Sasa, baada ya hiki kilichotokea kuhamisha ndege, gharama hizo zitapungua. Kwa hiyo, ile the actual net hasara utaiona itakuwa ndogo. Kama nilivyosema, mwaka huu tunatarajia tuta-break even na baada ya hapo tutaanza kuwa na mchango chanya kwenye vitabu vya Serikali.

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkakati wa kuongeza mapato, ATCL waliifahamisha Kamati kuwa mkakati wa kwanza, katika mwaka huu wa fedha ni kufikisha safari ya 47. Sasa hivi wana safari 37, kwa hiyo, kuna safari 10 nyingine zitaongezeka. Aidha ATCL inapanga "kutumia hangar" inazomiliki kufanya matengenezo ya ndege za Kamapuni nyingine ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchambua hoja za ukaguzi na majibu ya Bodi na Menejimenti ya ATCL, Kamati ina maoni kuwa kukamilika kwa uhamishaji wa umiliki wa ndege kutoka TGFA kwenda ATCL ni hatua muhimu katika kuboresha mizania ya hesabu na kupunguza gharama za uendeshaji. Hata hivyo,

ongezeko la madeni ya wadaiwa, hasara ya uendeshaji na kupungua kwa sehemu ya soko vinaonesha umuhimu wa kuimarisha ukusanyaji wa madeni, udhibiti wa gharama na mikakati ya kibiashara ili kuhakikisha Shirika linafikia uendelevu wa kifedha na kuanza kuchangia mapato ya Serikali.

2.5 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi Zinazohusu Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni *(Compliance Issues)*

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu, Kamati ilijikita katika kuchambua uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu katika usimamizi wa fedha na mapato ya Serikali, ununuzi na mikataba, usimamizi wa mali na utekelezaji wa miradi na programu. Aidha, Kamati ilitathmini utekelezaji wa maagizo na mapendekezo ya CAG na mamlaka za usimamizi na udhibiti, hatua za kurekebisha mapungufu, kuwawajibisha wahusika na kuzuia kujirudia kwa ukiukwaji.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelezo hayo, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu hoja za Kamati katika eneo hili kama ifuatavyo: -

2.5.1 Ukusanyaji wa Mapato Yasiyotokana na Utalii Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)

Mheshimiwa Spika,Kamati ilipokea na kujadili hoja ya ukaguzi kuhusu ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na utalii ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kwa mwaka wa fedha 2024/25. Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi hicho, Mamlaka ilikusanya mapato yasiyotokana na utalii yenye jumla ya Shilingi 3,185,206,969, yaliyotokana na tozo za umeme na maji, kodi ya nyumba, kodi ya minara pamoja na kodi ya Ngorongoro Tourism Investment Center (NTC).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, kwa mujibu wa matakwa ya sheria, mapato yanayotokana na vyanzo vilivyopo ndani ya eneo la mamlaka ya NCAA yanapaswa kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kiasi chote cha Shilingi 3,185,206,969 hakikukusanywa na TRA, bali kilikusanywa moja kwa moja na NCAA kupitia akaunti zake za benki za kibiashara na baadaye kuhamishiwa katika akaunti yake ya ukusanyaji iliyopo Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na maoni kuwa utaratibu huo umeibua kutokuwepo kwa uwazi wa kutosha kuhusu mamlaka yenye jukumu la kukusanya mapato hayo na iwapo mapato hayo yanapaswa kuwasilishwa TRA au BoT. Aidha, Menejimenti ilieleza kuwa asilimia 80 ya mapato yatokanayo na

uwekezaji ndiyo yanayotambuliwa kama mapato, huku mapato yanayotokana na kodi ya NTC yakitumika kwa kiasi kikubwa katika ulipaji wa mikopo, ambapo hadi tarehe 30 Juni 2025, mikopo hiyo ilikuwa na salio la takribani Shilingi bilioni 1.9.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini pia kuwa, licha ya hoja hii kubainishwa na CAG, NCAA haikuweza kuwasilisha nyaraka rasmi zinazoonesha msingi wa kisheria au makubaliano yanayoelekeza namna ya kushughulikia na kukusanya mapato hayo. Hali hii inaweza kusababisha kutofautiana kwa tafsiri ya matakwa ya sheria na kuathiri uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji na uwasilishaji wa mapato ya Serikali.

2.5.2 Kutokuwepo Usahihi Katika Kubaini Malipo ya Mwaka Yanayostahili Pensheni (APE) Katika Mifuko ya PSSSF na NSSF

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchambua taarifa ya CAG kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kwa mwaka wa fedha 2024/25, Kamati ilibaini kutokuwepo kwa ulinganifu katika kubaini Malipo ya Mwaka Yanayostahili Pensheni *(Annual Pensionable Emoluments - APE)* katika utekelezaji wa taratibu za ujumuishaji wa vipindi vya michango kati ya PSSSF na NSSF.

Mheshimiwa Spika, CAG alibainisha kuwa, katika sampuli ya mafao mawili ya kiasi cha mafao ya pensheni kinacholipwa mara

moja (CPG)[20] yenye jumla ya Sh.2,423,100,089, PSSSF ilikokotoa APE kwa kutumia mshahara wa msingi wa Sh.578,287,344, tofauti na NSSF iliyotumia mshahara ghafi wa Sh.612,202,146. Tofauti ya mishahara ya Sh.33,914,802 ilisababisha tofauti inayokadiriwa ya Sh.117,308,298 katika mafao ya CPG yaliyolipwa na PSSSF ikilinganishwa na kiasi kilichokadiriwa kulipwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa hali hiyo inatokana na kutokuwepo kwa ulinganifu katika tafsiri na matumizi ya masharti ya Sheria ya PSSSF na Miongozo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuhusu msingi wa kukokotoa Malipo ya Mwaka Yanayostahili Pensheni (APE), hususan katika ujumuishaji wa vipindi vya michango. Hali hii inaweza kusababisha wanachama wenye mazingira yanayofanana kuhesabiwa mafao kwa misingi tofauti, na hivyo kuleta tofauti katika kiasi cha mafao wanachostahili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya PSSSF tarehe 20 Agosti, 2026 ili kupata ufafanuzi wa hoja hii. Kamati ilijulishwa kuwa matumizi ya mshahara wa msingi katika kubaini APE yanaendana na Sheria ya PSSSF Na. 2 ya mwaka 2018. Hata hivyo, suala hilo liliwasilishwa Wizara ya Kazi, Ajira

[20] Commuted Pension Gratuity, CPG.

na Uhusiano kupitia barua Kumb. Na. AB.30/198/01A/67 ya tarehe 8 Julai 2026 kwa ajili ya kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza umuhimu wa kupata ufafanuzi rasmi wa Wizara kuhusu msingi sahihi wa kukokotoa malipo ya APE katika mazingira ya ujumuishaji wa vipindi vya michango, ili kuhakikisha matumizi yanayolingana ya masharti ya sheria na miongozo husika. Suala hili linahitaji kushughulikiwa kwa haraka ili kuondoa tofauti za ukokotoaji wa mafao kwa wanachama wenye mazingira yanayofanana na kuhakikisha wanalipwa mafao stahiki kwa usawa kwa mujibu wa sheria.

2.5.3 Usimamizi wa Mapato ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa hesabu za Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulibaini hoja za msingi zinazohusu ukusanyaji wa mapato, matumizi na usimamizi wa fedha za Tozo, pamoja na ufanisi wa mfumo wa usimamizi wa Tozo. Hoja hizo zinaonesha changamoto katika kuhakikisha mapato yanayostahili yanakusanywa kwa wakati na kikamilifu, fedha zinatumika kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa kisheria, na mifumo ya usimamizi na uwajibikaji inafanya kazi ipasavyo. Kwa ujumla, changamoto hizo zinaathiri ufanisi wa matumizi ya fedha za

umma na uwezo wa TDL kutekeleza malengo yaliyokusudiwa ya kuendeleza sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, hoja hizo ni kama ifuatavyo:-

2.5.3.1 Mapato ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii Ambayo Hayakukusanywa

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya vyanzo vya mapato ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii havikuanza kutumika, hivyo mapato yaliyostahili kutokana na vyanzo hivyo hayakukusanywa kikamilifu. Aidha, kulikuwa na madeni ya Tozo yenye thamani ya Shilingi 13,675,174,229 ambayo hayakuwa yamekusanywa. Hali hii inaonesha changamoto katika usimamizi na ufuatiliaji wa mapato ya Tozo, na kusababisha Serikali kutopata mapato yaliyokusudiwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya utalii.

Mheshimiwa Spika, kutokusanywa kwa mapato ya Serikali, kunapunguza rasilimali kwa ajili ya kuendeleza sekta ya utalii na kudhoofisha utekelezaji wa bajeti na shughuli zilizopangwa. Pia inaongeza hatari ya madeni ya Tozo kuendelea kukua na hatimaye kuwa vigumu kukusanywa.

2.5.3.2 Matumizi ya Fedha za Tozo Nje ya Vipaumbele Vilivyowekwa

Mheshimiwa Spika,ukaguzi ulibaini kuwa fedha za Tozo hazikutumika kwa kuzingatia mgawanyo uliowekwa katika Kanuni ya 10 ya Kanuni za Tozo ya Maendeleo ya Utalii, ambapo asilimia 50 inapaswa kuelekezwa kwenye maendeleo ya miundombinu, asilimia 36 kwenye utafiti, masoko na utangazaji, asilimia 8 kwenye TEHAMA na asilimia 6 kwenye ufuatiliaji na utawala. Kwa mfano, ni asilimia 14 tu ya fedha zilizotumika zilielekezwa kwenye maendeleo ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaweza kusababisha fedha za umma kutotumika kwa madhumuni na vipaumbele vilivyowekwa, hivyo kupunguza ufanisi na thamani ya matumizi ya fedha za Tozo. Aidha, inahatarisha kufikiwa kwa malengo ya Serikali katika kuboresha miundombinu na kukuza utalii.

2.5.3.3 Dosari Katika Matumizi ya Fedha Zitonazo na Tozo

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa Shilingi 14,632,168,740.94 zilitumika bila kupata ushauri wa Kamati ya Ushauri ya Utalii (TAC), wakati Shilingi 38,359,450,969 kati ya Shilingi 52,991,619,710 zilizokusanywa zilibaki bila kutumika katika akaunti za benki za Tozo. Hali hii inaonesha mapungufu katika usimamizi, upangaji na uidhinishaji wa matumizi ya fedha za Tozo.

Mheshimiwa Spika, matumizi bila kufuata taratibu za ushauri na uidhinishaji yanaongeza hatari ya matumizi yasiyozingatia vipaumbele. Kwa upande mwingine, fedha nyingi kubaki bila kutumika kunamaanisha kuwa rasilimali za umma hazitumiki kwa wakati kufikia malengo yaliyokusudiwa, jambo linaloweza kuchelewesha utekelezaji wa shughuli na kupunguza ufanisi wa matumizi ya fedha za Serikali.

2.5.3.4 Kusitishwa kwa Shughuli za Tozo Kutokana na Kutotekelezwa kwa Mageuzi ya Kimuundo

Mheshimiwa Spika, kupitia taarifa ya ukaguzi, Kamati ilibaini kuwa, pamoja na uwepo wa maelekezo ya Bunge ya kuimarisha usimamizi wa Tozo kwa kuanzisha chombo huru, kuandaa mpango mkakati na kusitisha shughuli zisizo na tija, hadi Agosti 2025 Wizara haikuwa imeweka mfumo madhubuti wa utekelezaji, mpango kazi, bajeti, mpango mkakati na ratiba ya kutekeleza mageuzi hayo. Hali hiyo ilisababisha shughuli za Tozo kuendelea kusitishwa.

Mheshimiwa Spika, kusitishwa kwa shughuli za Tozo kunasababisha fedha zilizokusanywa kutotumika kwa wakati na kwa madhumuni yaliyokusudiwa, hivyo kupunguza ufanisi na thamani ya fedha za umma. Aidha, kutokuwepo kwa mfumo wa wazi wa usimamizi, mpango mkakati na uwajibikaji kunaongeza

hatari ya kutotekelezwa kwa malengo ya Tozo na udhaifu katika ufuatiliaji wa matokeo.

2.5.4 Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, taasisi za umma zinapaswa kuandaa taarifa za fedha kwa kuzingatia viwango vya uhasibu vinavyotumika, ikiwemo Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma *(International Public Sector Accounting Standards – IPSAS)*, kulingana na matakwa husika. Viwango hivi vinalenga kuhakikisha taarifa za fedha zinaaminika, zinaeleweka na zinafananishwa, ili kuimarisha uwazi, uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokuzingatia masharti ya IPSAS kikamilifu kunaweza kusababisha taarifa za fedha kutowasilisha hali halisi ya kifedha ya taasisi, kudhoofisha udhibiti wa mali na madeni, na kuathiri maamuzi kuhusu matumizi ya fedha za umma.Kupitia uchambuzi wa taarifa za CAG, Kamati iliweza kubaini masuala yafuatayo kuhusu uzingatiaji wa matakwa ya IPSAS:-

2.5.4.1 Utambuzi kwa Wakati wa Madeni na Majukumu ya Kifedha

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa IPSAS 1 na IPSAS 19, pamoja na IAS 1 na IAS 37 kwa taasisi zinazotumia IFRS, taarifa za fedha zinapaswa kuonesha madeni na majukumu yanayotambulika katika kipindi husika. IPSAS 19 na IAS 37 zinahusu hasa masharti ya kutambua na kutoa taarifa za provisions na contingent liabilities. Katika Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe, deni la huduma za mahema la Sh. 83,500,000 halikutambuliwa katika taarifa za fedha.

Mheshimiwa Spika, kutotambua deni kwa wakati kunaweza kupunguza kiasi cha madeni na gharama zinazooneshwa katika taarifa za fedha, hivyo kutoa picha isiyokamilika ya hali ya kifedha ya taasisi.

2.5.4.2 Ukamilifu na Usahihi wa Kumbukumbu za Mali

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa IPSAS 17, au IPSAS 45 kwa vipindi ambavyo kiwango hicho kinatumika, kinahusu mali za kudumu, ikiwemo utambuzi, upimaji na uwasilishaji wake. Kwa taasisi zinazotumia IFRS, IAS 16 inaweka masharti ya utambuzi na upimaji wa mali, mitambo na vifaa. Kamati ilibaini katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, mali za kudumu zenye thamani ya Sh. 12,787,867,186.90 hazikuwa zimeingizwa katika Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) hadi mwaka wa fedha 2024/25.

Mheshimiwa Spika, kutokujumuisha mali zote katika kumbukumbu za mfumo kunaweza kudhoofisha udhibiti wa mali, kuathiri uthibitishaji wa taarifa za fedha na kuongeza hatari ya mali kupotea au kutumika bila ufuatiliaji wa kutosha.

2.5.4.3 Ulinganifu na Usuluhishi wa Taarifa Kutoka Mifumo Mbalimbali

Mheshimiwa Spika, IPSAS 1 inasisitiza uwasilishaji wa taarifa za fedha kwa namna inayotoa picha ya haki ya hali ya kifedha ya taasisi. IPSAS 3 inahusu sera za uhasibu, mabadiliko ya makadirio na makosa. Kwa taasisi zinazotumia IFRS, IAS 1 na IAS 8 zina masharti yanayohusiana na uwasilishaji wa taarifa na ushughulikiaji wa makosa. Uchambuzi wa Kamati ulibaini katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kulikuwa na tofauti ya Sh. 5,670,234,494.08 kati ya thamani ya mali iliyo katika GAMIS na MUSE tarehe 30 Juni 2025.

Mheshimiwa Spika, tofauti zisizochambuliwa na kusuluhishwa zinaweza kusababisha taarifa za mali kutokuwa sahihi, kudhoofisha uaminifu wa taarifa za fedha na kuathiri maamuzi ya usimamizi.

2.5.4.4 Tathmini ya Thamani na Kushuka kwa Thamani ya Mali

Mheshimiwa Spika, kwa vipindi ambavyo IPSAS 21 na IPSAS 26 zinatumika, viwango hivyo vinahusu upungufu wa thamani ya mali zisizozalisha fedha na zinazozalisha fedha mtawalia. Kwa

taasisi zinazotumia IFRS, IAS 36 inahusu upungufu wa thamani ya mali. Aidha, masharti ya upimaji wa mali hutegemea kiwango husika na sera inayotumika. Uchambuzi wa Kamati ulibaini katika Mamlaka ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) na Sekretarieti za Mikoa ya Dar es Salaam na Njombe, tathmini ya kushuka kwa thamani ya mali ilikuwa bado ikifuatiliwa, huku kumbukumbu za baadhi ya mali zikihitaji kuhuishwa.

Mheshimiwa Spika, kutofanya tathmini inayohitajika kwa wakati kunaweza kusababisha mali kuoneshwa kwa thamani isiyo sahihi na kuathiri uhalisia wa taarifa za mali za Serikali.

2.5.4.5 Utoshelevu na Uhuishaji wa Sera na Miongozo ya Uhasibu

Mheshimiwa Spika, IPSAS 3 inahusu sera za uhasibu, mabadiliko ya makadirio na makosa, huku IPSAS 17/45 na IPSAS 31 zikihusu, kwa vipindi na mazingira husika, mali za kudumu na mali zisizoshikika. Kwa taasisi zinazotumia IFRS, IAS 8, IAS 16 na IAS 38 zina masharti yanayohusiana na maeneo hayo. Sera za uhasibu zinapaswa kuendana na viwango vinavyotumika na aina ya miamala ya taasisi. Uchambuzi wa Kamati Katika TPHPA, Mwongozo wa Fedha wa mwaka 2023 haukujumuisha kikamilifu baadhi ya makundi ya mali, yakiwemo vifaa vya maabara, ndege, mitambo, pikipiki, ndege zisizo na rubani na programu za kompyuta.

Mheshimiwa Spika, kutokamilika kwa sera na miongozo kunaweza kusababisha kutofautiana kwa utambuzi, upimaji, uchakavu na uwasilishaji wa mali, na hivyo kuathiri usahihi na ulinganishwaji wa taarifa za fedha.

2.5.4.6 Uhakika na Ukamilifu wa Taarifa za Mapato

Mheshimiwa Spika, kwa taasisi zinazotumia IPSAS, utambuzi na uwasilishaji wa mapato hutegemea aina ya mapato na kiwango husika, ikiwemo IPSAS 9 na IPSAS 23 kwa vipindi vilivyokuwa chini ya viwango hivyo. Kwa taasisi zinazotumia IFRS, IFRS 15 hutumika kwa mapato yatokanayo na mikataba na wateja pale inapohusika. Masharti ya utambuzi wa mapato yanapaswa kuzingatiwa pamoja na matakwa ya uwasilishaji wa taarifa za fedha. Katika Wakala wa Vipimo (WMA), kulikuwa na tofauti ya Sh. 194,888,095 kati ya taarifa ya malipo ya mwaka na taarifa za makusanyo ya mwezi.

Mheshimiwa Spika, tofauti hiyo inaweza kuashiria mapungufu katika ulinganifu na uhakiki wa taarifa za mapato, na kusababisha mapato kuripotiwa kwa kiasi kisicho sahihi.

2.5.4.7 Uwezo wa Mifumo ya TEHAMA Kuzalisha Taarifa Zinazokidhi Mahitaji ya Uhasibu

Mheshimiwa Spika, IPSAS 1 inahitaji taarifa za fedha ziwe na sifa za ubora zinazowezesha watumiaji kuelewa na kuthibitisha hali ya kifedha ya taasisi. IPSAS 3 inatoa mwongozo kuhusu

sera za uhasibu na makosa. Kwa taasisi zinazotumia IFRS, IAS 1 na IAS 8 zinahusu uwasilishaji wa taarifa na ushughulikiaji wa makosa. Viwango hivi havielekeszi matumizi ya mfumo maalumu wa TEHAMA, lakini taarifa zinazozalishwa na mifumo hiyo zinapaswa kukidhi matakwa ya uhasibu. Mathalani katika Wakala wa Vipimo (WMA), baadhi ya uhakiki wa mita za umeme ulifanyika kwa kutumia fomu za karatasi nje ya moduli mahsusi ya WMA-MIS, na baadhi ya miunganisho ya mfumo na taasisi nyingine ilikuwa bado haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, kutegemea taratibu za nje ya mfumo kunaweza kuongeza hatari ya makosa, miamala kutorekodiwa kikamilifu, kupungua kwa ufuatiliaji wa mapato na kudhoofika kwa udhibiti wa ndani.

2.5.4.8 Uthibitishaji wa Taarifa Kabla ya Kufungwa kwa Hesabu

Mheshimiwa Spika, IPSAS 1 inahitaji taarifa za fedha ziwasilishwe kwa uaminifu na kwa kuzingatia viwango vinavyotumika. IPSAS 3 inahusu pia utambuzi na marekebisho ya makosa ya uhasibu. Kwa taasisi zinazotumia IFRS, IAS 1 na IAS 8 zina masharti yanayohusiana na uwasilishaji wa taarifa na ushughulikiaji wa makosa. Uhambuzi wa Kamati ulibaini katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, salio la vifaa katika MUSE lilikuwa Sh. 689,800, wakati taarifa za fedha zilionesha salio sifuri. Aidha, salio la mafuta katika MUSE lilikuwa sifuri, wakati taarifa ya GPSA ilionesha Sh. 23,364,198.

Mheshimiwa Spika, kutokuthibitisha na kusuluhisha tofauti hizo kabla ya kufungwa kwa hesabu kunaweza kusababisha makosa katika taarifa za fedha, kudhoofisha uaminifu wake na kuongeza uwezekano wa hoja za ukaguzi kujirudia.

2.6 Uchambuzi wa Kaguzi za Kiufundi *(Technical Audit Reports)*

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Kiufundi humwezesha CAG kutathmini ubora, gharama, muda na thamani ya fedha katika miradi ya maendeleo kwa kulinganisha kazi zilizotekelezwa na mikataba, usanifu na viwango vya kitaalamu vilivyowekwa. Kwa msingi huo, Kamati imechambua matokeo ya ukaguzi wa kiufundi wa CAG kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2025, kwa lengo la kubaini mapungufu, athari zake kwa fedha za umma na hatua zinazohitajika kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa miradi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, taarifa hii inawasilisha kwa Bunge hoja muhimu zilizobainishwa na CAG kupitia Kaguzi hiyo ya Kiufundi, pamoja na maoni, ushauri na hatua zinazopendekezwa na Kamati kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa miradi ya maendeleo, kuongeza uwajibikaji wa watendaji na kuhakikisha matumizi ya fedha za umma yanaendana na matokeo na thamani iliyokusudiwa. Taarifa hiyo na matokeo ya ukaguzi ni kama ifuatavyo:-

2.6.1 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ukarabati wa Viwanja va Benjamin Mkapa na Uhuru na Ujenzi wa Uwanja wa Arusha

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilianza kutekeleza miradi ya kuboresha miundombinu ya viwanja vya michezo kwa ajili ya maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON 2027). Miradi hiyo ilihusisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha pamoja na ukarabati na uendelezaji wa Viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru. Ukaguzi wa kiufundi ulifanyika kutathmini utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuzingatia gharama, muda, ubora, wigo wa kazi na masharti ya mikataba.Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

2.6.1.1 Uwanja wa Arusha kusanifiwa kwa kiwango cha CAF Category Three badala ya Category Four

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa usanifu wa awali wa Uwanja wa Arusha ulizingatia kiwango cha CAF Daraja la Tatu badala ya Daraja la Nne, hali iliyosababisha mabadiliko ya mawanda ya mradi na ongezeko la gharama la Sh bilioni 5.99 bila VAT. Kamati ilitaka kufahamu sababu za mahitaji hayo kutobainishwa mapema. Wizara ilieleza kuwa usanifu wa awali ulifanyika kabla Tanzania haijapata nafasi ya kuwa mwenyeji wa AFCON, hivyo ililazimika kuongeza mawanda ya mradi ili kukidhi

matakwa ya CAF. Aidha, Afisa Masuuli alieleza kuwa changamoto nyingi zilizojitokeza katika usimamizi wa ujenzi na ukarabati wa viwanja zilitokana kwa kiasi fulani na Wizara kutokuwa na uzoefu wa kutosha katika kutekeleza na kusimamia miradi ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, CAG alifafanua kuwa Mwongozo wa CAF wa mwaka 2022 ulikuwepo kabla ya kutolewa kwa tuzo ya mkataba, hivyo Wizara ilipaswa kuzingatia mahitaji husika katika hatua za awali za usanifu. Hivyo, maelezo ya Wizara hayakubainisha kwa kina sababu za kiwango cha Daraja la Nne kutokujumuishwa katika usanifu wa awali wa uwanja.

2.6.1.2 Tofauti ya Sh bilioni 2.97 katika gharama za mabadiliko ya usanifu wa Uwanja wa Arusha

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa katika ongezeko la gharama la Sh bilioni 5.99 la Uwanja wa Arusha, thamani ya kazi iliyohakikiwa ilikuwa chini kwa takribani Sh bilioni 2.97. Kamati ilitaka kufahamu msingi wa malipo hayo na hatua za kurejesha fedha zilizolipwa zaidi ya stahili.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilieleza kuwa madai ya awali ya mkandarasi ya Sh bilioni 12 yalipunguzwa hadi Sh bilioni 5.99 baada ya majadiliano. Aidha, ilifafanua kuwa kazi zilizohakikiwa zilihusisha kuboresha kituo cha waandishi wa habari ili kukidhi mahitaji ya CAF.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilieleza kuwa ilipanga kukata Sh. milioni 381.46 katika malipo yaliyofuata, huku gharama nyingine zikihusishwa na kazi za ziada. Hata hivyo, hapakuwa na uthibitisho wa tofauti kati ya thamani ya kazi iliyohakikiwa na malipo yaliyofanyika, wala kama kiasi kilichopangwa kukatwa kilikuwa tayari kimekatwa, hivyo hoja hii itaendelea kufanyiwa kazi na CAG na Kamati imetoa pendekezo la hatua za kuchukuwa.

2.6.1.3 Kutumika kwa bei isiyo sahihi ya Sh 0.02 katika tathmini ya zabuni ya mshauri elekezi wa Uwanja wa Arusha

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa katika tathmini ya zabuni ya mshauri elekezi wa Uwanja wa Arusha, bei ya Sh 0.02 ilitumika badala ya bei halisi ya takribani Sh bilioni 12.24 iliyowasilishwa na kampuni ya Dar Al-Handasah, hali iliyoibua hoja kuhusu mchakato wa tathmini na ushindani. Kamati ilitaka kufahamu chanzo cha dosari hiyo na hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilieleza kuwa changamoto za kiutendaji katika mfumo wa NeST zilisababisha baadhi ya takwimu kubadilika, na kuwa tatizo hilo lilijadiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na kujitokeza pia katika zabuni nyingine. Aidha, Wizara ilieleza kuwa ilichunguza uwezo wa kampuni na uhalisia wa bei zilizowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara haikutoa maelezo ya kina kuhusu dosari hiyo na hatua zilizochukuliwa, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha ushahidi wa kutosha kwa wakaguzi kubainisha namna changamoto za mfumo wa NeST zilivyochangia bei hiyo kuendelea kutumika hadi hatua za mwisho za tathmini na utoaji wa tuzo ya mkataba.

2.6.1.4 Tofauti kati ya makadirio ya gharama na thamani ya mkataba wa Uwanja wa Arusha

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa makadirio ya gharama katika mfumo wa NeST yalikuwa Sh bilioni 187, lakini mkataba ulitolewa kwa Sh bilioni 338.54, sawa na ongezeko la asilimia 81. Kamati pia ilihoji matumizi ya utaratibu wa ununuzi usio na ushindani na namna thamani ya fedha ilivyohakikishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilieleza kuwa makadirio ya awali hayakuzingatia kikamilifu mahitaji ya Uwanja wa Arusha na kiwango cha CAF Daraja la nne *(Category Four).* Aidha, Wizara ilieleza kuwa muda mfupi wa maandalizi ya AFCON ulichangia ongezeko la gharama na matumizi ya utaratibu wa ununuzi usio na ushindani *(single source)* ili kuharakisha utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, maelezo ya Wizara kwa CAG na kwa Kamati hayakufafanua kwa kina sababu za ongezeko la gharama kwa asilimia 81, usahihi wa makadirio ya awali na

namna thamani ya fedha ilivyohakikishwa licha ya kutokuwepo kwa ushindani wa zabuni.

2.6.1.5 Kuongezeka kwa gharama za vifaa vya mwanga katika Uwanja wa Uhuru

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini ongezeko la bei ya vifaa vya mwanga wa uwanja (pitch lights) kutoka Sh milioni 185.8 hadi takribani Sh bilioni 1.85. Kamati ilitaka kufahamu sababu za ongezeko hilo na uhalali wa marekebisho ya bei nje ya mpango ulioidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilieleza kuwa changamoto za mfumo wa NeST zilisababisha bei kuonekana kimakosa, hivyo timu ya majadiliano ilirekebisha bei baada ya majadiliano na mkandarasi. Aidha, Wizara ilieleza kuwa matokeo yaliwasilishwa kwa Bodi ya Zabuni kwa idhini na kumbukumbu za majadiliano zilikuwepo. Hata hivyo, CAG aliifahamisha Kamati kuwa Wizara haikuwasilisha ushahidi wa kutosha kuthibitisha chanzo cha tofauti ya bei, sababu za kutorekebisha changamoto iliyojitokeza mapema na uhalali wa marekebisho hayo kwa mujibu wa taratibu za ununuzi.

2.6.1.6 Kutoa mkataba kwa mzabuni mwenye bei ya juu zaidi katika ukarabati wa Uwanja wa Uhuru

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kufahamu sababu za kutomchagua mzabuni aliyewasilisha bei ya Sh bilioni 18.8 na badala yake kumpa mkataba mzabuni aliyewasilisha bei ya Sh bilioni 19.7, ikiwa ni tofauti ya takribani Sh milioni 865. Wizara ilieleza kuwa zabuni ya awali ilifutwa na kutangazwa upya, na uchunguzi wa kina ulibaini kuwa mzabuni mwenye bei ya chini hakuwa na uzoefu wa kutosha katika ujenzi wa viwanja vya michezo. Hivyo, ilimchagua mzabuni mwenye uzoefu zaidi ili kupunguza hatari za utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, CAG aliifahamisha Kamati kuwa Wizara haikuwasilisha nyaraka za kutosha kuthibitisha kutokuwa na uwezo kwa mzabuni aliyewasilisha bei ya chini, wala kueleza kikamilifu sababu za kumchagua mzabuni mwenye bei ya juu na namna thamani ya fedha ilivyohakikishwa. Kwa kuzingatia umuhimu wa hoja hii, Kamati imetoa mapendekezo ya kuboresha usimamizi wa taratibu za manunuzi katika Sehemu ya Tatu ya taarifa hii.

2.6.1.7 Mapungufu katika udhibiti wa ubora wa vifaa vya ujenzi

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini mapungufu katika udhibiti wa ubora wa kazi na vifaa, ikiwemo matofali na mchanga uliokusudiwa kutumika katika eneo la nyasi bandia. Wizara

ilieleza kuwa mchanga ulikuwa haujaandaliwa wakati wa ukaguzi, lakini baadaye ulichujwa, ukapimwa na kukidhi vigezo. Hata hivyo, majibu hayakufafanua kikamilifu mapungufu kuhusu matofali, taratibu za upimaji na hatua za kuzuia kasoro hizo kujirudia.

2.6.1.8 Malipo ya kazi ambazo hazikufanyika na malipo yaliyolipwa zaidi ya stahili

Mheshimiwa Spika,ukaguzi ulibaini malipo yasiyostahili, kazi ambazo hazikutekelezwa na gharama za ziada katika viwanja vya Benjamin Mkapa, Uhuru na Arusha. Wizara ilikiri kuwa baadhi ya kazi zilizojumuishwa kwenye mkataba wa mshauri elekezi wa Uwanja wa Arusha zilikuwa tayari zimefanywa na mwajiri, na kueleza kuwa ilikuwa imeanza kufuatilia makato ya malipo yaliyopitiliza. Hata hivyo, taarifa kamili ya kiasi kilicholipwa zaidi, kilichorejeshwa, salio lililobaki na muda wa kukamilisha urejeshaji ilikuwa bado haijawasilishwa kwa CAG kwaajili ya uhakiki.

2.6.1.9 Kutofungwa kwa "switchgear" ya nne katika Uwanja wa Benjamin Mkapa

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa kati ya "switchgear" nne zilizonunuliwa kwa ajili ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, ni tatu tu zilizofungwa kutokana na ukosefu wa nafasi ya kifaa cha nne. Wizara ilieleza kuwa mkandarasi na mshauri elekezi walikubaliana kurekebisha mpangilio wa chumba cha umeme ili

kifaa hicho kifungwe mwezi Oktoba 2026. Hata hivyo, wakaguzi hawakuwa wamepata uthibitisho wa utekelezaji wa hatua hiyo na uzingatiaji wa viwango vya kiufundi na usalama, hivyo CAG atatakiwa kuhakiki utekelezaji wa hoja hii katika kaguzi zinazoendelea.

2.6.1.10 Utekelezaji wa mapendekezo ya CAG na uwezo wa Wizara kusimamia miradi ya viwanja vya michezo

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 14 Agosti 2026, kati ya mapendekezo 12 ya CAG, mawili (asilimia 16.7) yalikuwa yametekelezwa, tisa (asilimia 75) yalikuwa katika hatua za utekelezaji na moja (asilimia 8.3) lilikuwa halijaanza. Wizara ilieleza kuwa ilikuwa ikifuatilia urejeshaji wa fedha, kutoa mafunzo kwa wataalamu na kushughulikia changamoto za usajili katika taasisi za ukandarasi. Aidha, ilieleza kuwa mchakato wa kuunda Wakala wa Usimamizi wa Miundombinu ya Michezo ulikuwa umekamilika, huku hatua za kumpata Mkurugenzi Mkuu zikiendelea. Hata hivyo, haikutoa ratiba ya mwisho ya kukamilisha mapendekezo, uthibitisho wa fedha zilizorejeshwa au taarifa ya kuanza kazi kwa wakala huyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla katika hoja za ukarabati na ujenzi wa viwanja vya michezo, Kamati imebaini changamoto katika maeneo ya usanifu na udhibiti wa gharama za miradi, taratibu za manunuzi, matumizi ya mfumo wa NeST, udhibiti wa ubora, uthibitishaji wa malipo na utekelezaji wa mapendekezo

ya CAG. Pamoja na maelezo ya Wizara kuhusu hatua zilizochukuliwa, bado kuna maeneo ya kufanyiwa kazi zaidi kuhusu uhalali wa baadhi ya gharama na malipo, urejeshaji wa fedha na uwajibikaji wa wahusika. Kwa msingi huo, mapendekezo ya Kamati katika sehemu ya tatu ya taarifa hii yanalenga kuimarisha uwajibikaji, thamani ya fedha za umma, usimamizi wa mikataba na ubora wa miradi ya Serikali.

2.7 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT Issues)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua hoja za ukaguzi kuhusu usalama, usimamizi na ufanisi wa mifumo ya TEHAMA katika Taasisi zilizokaguliwa, ikijumuisha ulinzi wa taarifa, udhibiti wa watumiaji, utunzaji na urejeshaji wa taarifa, uendelevu wa mifumo na uzingatiaji wa sera na taratibu husika.Aidha, Kamati ilitathmini udhibiti wa hatari za TEHAMA, thamani ya uwekezaji katika mifumo hiyo katika kuboresha utendaji na uwajibikaji, pamoja na hatua zilizochukuliwa na Taasisi kushughulikia mapungufu yaliyobainishwa na CAG na kuzuia kujirudia kwake.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, Kamati ilibaini hoja za ukaguzi katika maeneo yafuatayo: -

2.7.1 Udhaifu katika Usimamizi na Usalama wa Mifumo ya TEHAMA katika TAFICO

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA katika TAFICO ulibaini upungufu wa watumishi wenye sifa na uzoefu, kutokuwepo kwa Kamati ya Usimamizi na Sera ya TEHAMA, pamoja na kutothibitishwa kwa uwepo wa Mpango wa Kurejesha Mifumo baada ya Maafa na Kituo cha Kuhifadhi Taarifa kinachokidhi viwango vinavyotakiwa. Mapungufu haya yanaweza kuhatarisha usalama na upatikanaji wa taarifa za uzalishaji, mauzo na mapato, kuathiri usahihi wa kumbukumbu za kifedha na upatanisho wa mapato, na kudhoofisha mifumo ya udhibiti wa ndani na uwajibikaji wa menejimenti.

2.7.2 Udhaifu katika Usalama wa Chumba cha Seva na Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA katika Wizara ya Kilimo — Fungu 43

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini udhaifu katika udhibiti wa mazingira na usalama wa chumba cha seva, kutokukamilika kwa mikataba na viwango vya huduma kwa baadhi ya watoa huduma, pamoja na kutotumika kikamilifu kwa Moduli ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika mfumo wa e-Kilimo. Mapungufu haya yanaweza kuhatarisha usalama na upatikanaji wa taarifa za kilimo, kuongeza gharama za matengenezo na kudhoofisha uwajibikaji wa watoa huduma. Aidha, kutokukamilika kwa matumizi ya moduli hiyo kunadhoofisha

upangaji wa bajeti, ugawaji wa rasilimali na ufuatiliaji wa tija ya miradi ya kilimo kutokana na kutokuwepo kwa kanzidata ya taifa iliyohuishwa ya matumizi ya ardhi ya kilimo.

2.7.3 Udhaifu katika Udhibiti na Uunganishaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Shirika la Bima la Taifa (NIC)

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini udhaifu katika usimamizi wa ruhusa za watumiaji na mapitio ya kumbukumbu za mifumo, kutotekelezwa kikamilifu kwa mpango mkakati wa TEHAMA na kutokukamilika kwa uunganishaji wa mfumo wa ERMS na MUSE. Aidha, kulibainika kutokukamilika kwa taarifa za bima na uthibitisho wa mifumo ya HCMIS/e-Watumishi. Mapungufu haya yanaweza kusababisha mabadiliko yasiyoidhinishwa ya taarifa za kifedha, kutolingana kwa kumbukumbu na makosa katika upatanisho wa miamala, hivyo kudhoofisha udhibiti wa ndani na uwajibikaji.

2.7.4 Kutokuwepo kwa Mfumo Jumuishi wa Kusimamia Miradi na Mikataba katika Kampuni ya Ujenzi ya Umeme (ETDCO)

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa ETDCO haina mfumo jumuishi wa kusimamia miradi na mikataba ya ujenzi na matengenezo ya njia za umeme. Aidha, Mpango Mkakati wa TEHAMA haujaainisha kikamilifu matumizi ya TEHAMA yanayohitajika kufikia malengo ya Kampuni. Mapungufu haya

yanadhoofisha ufuatiliaji wa gharama za miradi dhidi ya bajeti na uthibitishaji wa malipo kulingana na kazi zilizotekelezwa, hivyo kuongeza hatari ya makosa, kurudiwa kwa taarifa na kuongezeka kwa gharama ambazo haziwezi kubainika kwa wakati.

2.7.5 Udhaifu katika Urejeshaji na Uunganishaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Idara ya Uhamiaji — Fungu 93

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kutothibitishwa kwa ufanisi wa mipango ya kurejesha mifumo baada ya maafa, kutounganishwa kikamilifu kwa mifumo ya maombi ya pasipoti za ndani na balozini, pamoja na kutotumika kikamilifu kwa mfumo wa e-Citizenship. Mapungufu haya yanaweza kusababisha kupotea kwa taarifa za miamala, kuchelewa kwa utoaji wa huduma, malipo ya ada mara mbili, ucheleweshaji wa marejesho na kutolingana kwa kumbukumbu za mapato. Aidha, kuendelea kutumia njia za kawaida katika baadhi ya shughuli kunaweza kuongeza gharama za kiutawala na hatari ya makosa.

2.7.6 Udhaifu katika Usimamizi wa Makosa, Adhabu na Taarifa za Leseni katika Mifumo ya TEHAMA ya Tume ya Madini

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kutotumika kikamilifu kwa moduli ya makosa katika mfumo wa MiMS, kutokuwepo kwa utaratibu wa kutoa taarifa za adhabu kupitia SMS katika mfumo wa LANDFOLIO, pamoja na kasoro katika taarifa za hali

ya leseni katika mfumo wa MCIMS. Mapungufu haya yanaweza kusababisha kutolingana kwa kumbukumbu za ukiukwaji wa sheria, faini na mapato yaliyokusanywa, kudhoofisha ufuatiliaji wa adhabu na kuathiri usahihi wa taarifa za leseni, hivyo kupunguza ufanisi wa usimamizi na udhibiti wa shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yao, Maafisa Masuuli wa taasisi zilizorejewa hapo awali, walieleza kuwa wanaendelea kufanyia kazi mapungufu yaliyobainika katika mifumo ya TEHAMA kwa kushirikiana na wataalamu wa Serikali Mtandao ili kuimarisha usalama, ufanisi na udhibiti wa mifumo hiyo. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa hoja hizi ni muhimu kwa kuwa zinahusiana moja kwa moja na usimamizi wa mapato ya Serikali, usahihi wa kumbukumbu za kifedha na uwajibikaji wa taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati imeona umuhimu wa kuziwasilisha hoja hizi mbele ya Bunge na kutoa mapendekezo mahsusi ya kuboresha usimamizi, usalama na uunganishaji wa mifumo ya TEHAMA katika taasisi za Serikali. Hatua hizo zinalenga kuimarisha udhibiti wa ndani, kuongeza ufanisi wa ukusanyaji na usimamizi wa mapato, na kuzuia mianya inayoweza kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

2.8 Uchambuzi wa Hoja za Usimamizi wa Mali za Serikali (*Assets Management Issues*)

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua Taarifa CAG, Kamati ilibaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi, utunzaji, matumizi na ulinzi wa mali za Serikali. Mapungufu hayo yanahusu kutokukamilika kwa kumbukumbu, usajili na uthamini wa mali, kutokuwa na nyaraka za kisheria za umiliki wa ardhi, pamoja na kuwepo kwa mali zilizopotea, zilizotelekezwa au zisizotumika kwa tija iliyokusudiwa. Aidha, Kamati ilitathmini mifumo ya udhibiti na ufuatiliaji wa mali, matumizi ya ardhi na majengo, pamoja na hatua zilizochukuliwa na taasisi husika kurekebisha mapungufu hayo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umejikita katika kubainisha mapungufu hayo, athari zake katika ulinzi na matumizi ya rasilimali za umma, pamoja na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuimarisha uwajibikaji na kuhakikisha mali za Serikali zinasimamiwa kwa mujibu wa sheria na kwa manufaa yaliyokusudiwa. Hoja kuu zilizobainika zimefafanuliwa kama ifuatavyo:-

2.8.1 Taasisi Zisizokamilisha Urasimishaji wa Umiliki wa Ardhi

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali muhimu ya Serikali inayotumika kutekeleza majukumu ya taasisi za umma, ikiwemo ujenzi wa ofisi, shule, vyuo, vituo vya kutolea huduma na

miundombinu mingine. Hata hivyo, baadhi ya taasisi hutumia ardhi bila kukamilisha taratibu za kisheria za kuthibitisha na kurasimisha haki zao za umiliki au matumizi. Hali hii huongeza hatari ya migogoro ya ardhi, uvamizi na madai ya umiliki kutoka kwa watu wengine, na hivyo kuhatarisha usalama wa ardhi na uwekezaji wa Serikali uliofanyika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, na Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334, haki na maslahi katika ardhi yanapaswa kutambuliwa na kusimamiwa kwa kuzingatia taratibu za kisheria za umiliki na usajili. Kwa hiyo, taasisi za Serikali zinapaswa kuhakikisha ardhi zinazomiliki au kutumia zinatambuliwa kisheria na nyaraka stahiki za umiliki au matumizi zinapatikana. Hatua hii ni muhimu katika kuthibitisha haki za taasisi, kulinda ardhi dhidi ya madai yanayoweza kujitokeza na kuwezesha matumizi ya ardhi kwa mipango ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kutokukamilika kwa urasimishaji wa ardhi kunaweza kudhoofisha uwezo wa taasisi kulinda haki zake, kusababisha migogoro na gharama za kisheria, pamoja na kuhatarisha mali na miundombinu iliyowekezwa katika maeneo husika. Kwa msingi huo, Kamati ilibaini taasisi zenye changamoto za kutokuwa na hati za umiliki wa ardhi, ambazo zimeainishwa katika Jedwali Na. 2.2.

Jedwali Na. 2.2: Orodha ya Taasisi na idadi ya viwanja visivyokuwa na hati za umiliki

Na.	Taasisi / Fungu	Viwanja bila hati
1.	Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)	2
2.	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara (Fungu 95)	24
3.	Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)	18
4.	Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)	2
5.	Tume ya Madini	1
6.	Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM)	4
7.	Wizara ya Kilimo (Fungu 43)	26
	JUMLA	**77**

Chanzo: *Uchambuzi wa Kamati katika taarifa za mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2025.*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Jedwali Na. 2.2 umebaini kuwa taasisi saba za Serikali zina jumla ya viwanja 77 visivyo na hati za umiliki. Wizara ya Kilimo, Fungu 43, ina idadi kubwa zaidi ya viwanja hivyo (26), ikifuatiwa na Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara (24) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) (18). Hali hii inaonesha udhaifu katika usimamizi na urasimishaji wa umiliki wa ardhi za Serikali, unaoweza kuongeza hatari ya migogoro ya ardhi, uvamizi na upotevu wa mali za umma. Kwa hiyo, ni muhimu kwa taasisi husika kuharakisha taratibu za

kupata hati za umiliki ili kulinda na kuimarisha usimamizi wa ardhi za Serikali.

2.8.2 Kutokukamilika kwa Usajili wa Mali za Serikali Katika Mfumo wa GAMIS

Mheshimiwa Spika, Serikali hutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mali za Serikali (*Government Asset Management Information System – GAMIS*) kuhifadhi na kusimamia taarifa za mali za taasisi za umma. Mfumo huu ni nyenzo muhimu katika kuwezesha usajili, ufuatiliaji na udhibiti wa mali, pamoja na kuboresha usahihi wa kumbukumbu za kihasibu na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Serikali. Ili kufanikisha malengo hayo, taasisi zinapaswa kuhakikisha taarifa za mali zinaingizwa, zinahakikiwa na kuhuishwa mara kwa mara katika mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, Kanuni za Usimamizi wa Mali za Umma za mwaka 2024 na miongozo ya Hazina, taasisi zinapaswa kutunza kumbukumbu sahihi za mali ili kuhakikisha taarifa za usimamizi na hesabu zinaaminika.

Mheshimiwa Spika, kutokukamilika kwa usajili na uhuishaji wa taarifa za mali katika GAMIS kunaweza kusababisha kutokulingana kwa kumbukumbu, kushindwa kuthibitisha uwepo

na thamani ya mali, pamoja na kuongeza hatari ya upotevu na matumizi yasiyo sahihi ya rasilimali za umma. Hali hiyo pia hudhoofisha upangaji, ufuatiliaji na ufanyaji wa maamuzi kuhusu mali za taasisi. Kwa msingi huo, Kamati ilichambua taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu hayo, kama zilivyoainishwa katika Jedwali Na.2.3.

Jedwali Na. 2.3: Mchanganuo wa Taasisi na Uzingatiaji wake katika Mfumo wa GAMIS

Na.	Jina la Taasisi	Jumla ya mali zenye thamani	Thamani inayoonekana kwenye GAMIS mpaka Juni,2025 (TZS)	Thamani ya mali (PPE) iliyotumika kufungia hesabu mpaka Juni,2025 (TZS)	Tofauti (TZS)
1.	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika	297	**8,037,664,563.76**	**9,073,607,046.94**	**(1,035,942,483.18)**
2.	Mamlaka ya Wanyapori Tanzania (TAWA)	6,352	**90,959,505,467.34**	**136,575,607,939.43**	**(45,616,102,472.49)**
3.	Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC)	7,317	**2,366,732,597,907**	**2,443,211,000,000**	**(76,478,402,093)**
4.	Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Fungu 68	1,305	**60,279,616,395.19**	**213,995,106,403.00**	**(153,715,490,007.80)**
5.	Tume ya Pamoja ya Fedha Fungu 10	-	**43,643,197.10**	**879,535,982.00**	**(835,892,784.9)**
6.	Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB)	-	**666,719,370.26**	**59,349,000,000.00**	**(58,682,280,629.74)**
7.	Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)	-	**4,161,648,300.69**	**9,166,662,459.00**	**(5,005,014,158.31)**
8.	Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)	35,841	**48,491,086,870.53**	**68,166,535,924.00**	**(19,675,449,053.47)**
9.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)	9,899	**88,524,330,458**	**80,277,951,000.00**	**(8,246,379,457.78)**
10.	Shirika la Uvuvi	218	**119,196,234,605.85**	**118,279,854,393.85**	**(916,380,212.00)**

Na.	Jina la Taasisi	Jumla ya mali zenye thamani	Thamani inayoonekana kwenye GAMIS mpaka Juni,2025 (TZS)	Thamani ya mali (PPE) iliyotumika kufungia hesabu mpaka Juni,2025 (TZS)	Tofauti (TZS)
	Tanzania (TAFICO)				
11.	Wizara ya Kilimo Fungu 43	21,958	**287,232,576,498.00**	**321,871,306,139.00**	**(34,638,729,641.00)**

Chanzo: ***Uchambuzi wa Kamati Kwenye Taarifa za Hesabu za Mafungu Mbalimbali, Agosti - Oktoba, 2026.***

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Jedwali Na. 2.3 umebaini kuwepo kwa tofauti za thamani ya mali kati ya taarifa zinazoonekana kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) na thamani zilizotumika kufunga hesabu za mali za kudumu (PPE) kwa mwaka ulioishia Juni 2025 katika taasisi zote 11 zilizowasilisha taarifa. Tofauti kubwa zaidi ilibainika katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Fungu 68, ya Shilingi bilioni 153.72, ikifuatiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) ya Shilingi bilioni 76.48, Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) ya Shilingi bilioni 58.68 na Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) ya Shilingi bilioni 45.62.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaashiria udhaifu katika ulinganifu na uthibitishaji wa kumbukumbu za mali kati ya GAMIS na taarifa za hesabu, jambo linaloweza kuathiri usahihi na ukamilifu wa taarifa za fedha pamoja na usimamizi wa mali za umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Maafisa Masuuli wa taasisi husika, ikasikiliza maelezo yao na kutathmini hatua zilizochukuliwa kurekebisha mapungufu ya urasimishaji wa ardhi na usajili wa mali katika GAMIS.Kamati inasisitiza kukamilishwa kwa hatua hizo kwa wakati ili kulinda haki za Serikali katika ardhi, kuimarisha udhibiti wa mali na kuhakikisha kumbukumbu sahihi za rasilimali za umma zinatunzwa, hivyo kuzuia migogoro na upotevu wa mali za Serikali.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2025 Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

3.2 Maoni

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na majadiliano yaliyofanyika na taasisi husika, Kamati imebaini kuwa, pamoja na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali na taasisi zake katika kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma, bado kuna changamoto zinazohitaji hatua madhubuti za kiutawala, kisheria na kiusimamizi. Changamoto hizo zinajitokeza katika maeneo yafuatayo:-

a) **Usimamizi wa fedha na ukusanyaji wa mapato:** Kuna mapungufu katika ufanisi wa ukusanyaji wa mapato, ufuatiliaji wa madeni, usimamizi wa matumizi na udhibiti wa miamala ya kifedha, hali inayoweza

kusababisha upotevu wa mapato na matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma.

b) **Ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba:** Baadhi ya taasisi zimebainika kuwa na mapungufu katika uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa umma, uteuzi wa wazabuni, udhibiti wa ubora wa kazi na usimamizi wa utekelezaji wa mikataba. Mapungufu hayo yanaweza kusababisha ongezeko la gharama, malipo yasiyolingana na thamani ya kazi iliyofanyika na kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi.

c) **Mifumo ya udhibiti wa ndani na uwajibikaji**: Baadhi ya taasisi zina udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani, miundo ya kiutendaji na mgawanyo wa majukumu. Hali hii inaweza kudhoofisha uwajibikaji, ufuatiliaji wa maamuzi na usimamizi wa rasilimali za umma.

d) **Ufanisi wa kiutendaji na thamani ya fedha:** Uchambuzi umebaini changamoto za kifedha na kiutendaji katika baadhi ya taasisi na miradi ya Serikali, zikiwemo madeni, gharama kubwa za uendeshaji, ucheleweshaji wa miradi na kutokufikia kikamilifu malengo yaliyokusudiwa. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuimarisha mipango, usimamizi wa utekelezaji na tathmini ya matokeo.

e) **Uzingatiaji wa sheria na kanuni:** Baadhi ya hoja zinaonesha mapungufu katika utekelezaji wa matakwa ya sheria na kanuni, ikiwemo usimamizi wa mapato, stahili za pensheni na tozo za Serikali. Hali hii inahitaji kuimarishwa kwa mifumo ya ufuatiliaji, uthibitishaji wa miamala na hatua za kuwawajibisha wasimamizi pale kutokuzingatia taratibu kunapobainika.

f) **Usimamizi wa mali za Serikali:** Kuna umuhimu wa kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu, uthamini, ufuatiliaji na matumizi yenye tija ya mali za Serikali ili kuhakikisha mali hizo zinalindwa dhidi ya upotevu, uharibifu na matumizi yasiyoidhinishwa.

g) **Mifumo ya TEHAMA na usalama wa taarifa:** Hoja zilizobainika zinaonesha changamoto katika usalama wa mifumo, uunganishaji wa mifumo ya TEHAMA, udhibiti wa taarifa na uendelevu wa mifumo ya kidijitali. Hali hii inahitaji kuimarishwa kwa udhibiti wa mifumo, usalama wa taarifa na matumizi ya mifumo jumuishi inayowezesha ufanisi na uwajibikaji.

h) **Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi:** Hoja mbalimbali zilizojitokeza zinaonesha umuhimu wa kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya CAG na maelekezo ya Kamati ili kuhakikisha mapungufu yanayobainika yanarekebishwa kwa wakati na hayajirudii katika miaka inayofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, ni maoni ya Kamati kuwa, changamoto zilizobainika zinahitaji Serikali na taasisi zake kuimarisha mifumo ya usimamizi, udhibiti wa ndani, uzingatiaji wa sheria na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma. Aidha, ni muhimu kuweka hatua za marekebisho zenye muda maalumu wa utekelezaji, kuwabainisha watakaowajibika na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha mapendekezo ya ukaguzi yanatekelezwa na dosari zilizobainika hazijirudii. Kwa msingi huo, sehemu inayofuata ya taarifa hii itawasilisha mapendekezo ya Kamati kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha na mali za umma, ufanisi wa taasisi na uwajibikaji kwa wananchi.

3.3 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa athari za hoja zilizobainika, matokeo yanayohusiana na hoja hizo, uwezekano wa kujirudia kwa hoja, pamoja na hatua zinazohitajika kuchukuliwa ili kuzitatua. Mapendekezo hayo pia yameainishwa katika **Randama ya 1** iliyoambatishwa na Taarifa hii. Mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

3.3.1 Kuhusu Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

KWA KUWA, kupitia Taarifa ya Ukaguzi ya CAG katika hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imebainika kuwa; ongezeko la mashauri ya kodi ambayo hayajatatuliwa yenye thamani ya Sh. trilioni 10.72; mapungufu katika ukadiriaji na uthibitishaji wa kodi; kutokuthibitishwa kwa kiasi cha mafuta ya transit chenye thamani ya Sh. bilioni 163.16; ucheleweshaji wa ukaguzi wa kodi; na kutowasilishwa kwa marejesho ya VAT kwa wakati na walipa kodi, pamoja na kuchelewa kuchukua hatua za kuhakikisha uzingatiaji wa sheria za kodi;

NA KWA KUWA, masuala hayo hapo juu yanaweza kuwa na athari zifuatazo:-

a) Kuchelewesha upatikanaji wa uamuzi wa mwisho kuhusu madeni ya kodi na kuongeza mlundikano wa mashauri, hivyo kuathiri uhakika wa mapato ya Serikali na kuongeza gharama kwa walipa kodi;
b) Kusababisha upotevu au ucheleweshaji wa mapato ya Serikali kutokana na kodi kutokadiriwa kwa usahihi na udhaifu katika uhakiki wa taarifa za walipa kodi;
c) Kuongeza hatari ya mafuta yanayosafirishwa kwa transit kuingia katika matumizi ya ndani bila kulipiwa kodi na hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali;

d) Kucheleweshа utambuzi na ukusanyaji wa madeni ya kodi na kuongeza hatari ya baadhi ya madai ya kodi kupoteza uhalali kutokana na muda mrefu wa kutokufanyiwa ukaguzi; na
e) Kudhoofisha uzingatiaji wa sheria za kodi na kuathiri ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kutokana na kutowasilishwa kwa marejesho ya VAT kwa wakati.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Ndani ya mwaka fedha 2026/2027, TRA ihakikishe mashauri yote ya kodi ambayo hayajatatuliwa yanafuatiliwa kwa mfumo madhubuti wa usimamizi wa mashauri, kwa kuweka muda maalum wa utekelezaji na kupunguza kwa hatua mlundikano wa mashauri yaliyochelewa;
b) TRA iimarishe mifumo ya uhakiki na udhibiti wa ubora wa tathmini za kodi ili kuhakikisha kodi inayostahili inalipwa kwa usahihi na kiasi cha Sh.8,310,477,597 ambacho hakikuthibitishwa kikamilifu kinafanyiwa uhakiki na hatua stahiki kwa mujibu wa sheria zinachukuliwa;
c) TRA na mamlaka nyingine zinazohusika ziimarishe mfumo wa ufuatiliaji wa mafuta yanayosafirishwa kwa "transit" kutoka kituo cha kuingilia hadi kituo cha

kutoka, na kuhakikisha kodi inayostahili kwa lita milioni 14 zilizobainika kutothibitishwa kutoka nje ya nchi inakusanywa;

d) TRA ihakikishe ukaguzi wa kodi unafanyika kwa wakati, hasa kwa kuzingatia muda uliowekwa na sheria, na iweke mfumo wa ufuatiliaji wa kesi za ukaguzi ili kuzuia ucheleweshaji wa muda mrefu; na

e) TRA ichukue hatua stahiki dhidi ya walipa kodi 17,573 ambao hawakuwasilisha marejesho 93,953 ya VAT na iimarishe mifumo ya ufuatiliaji ili marejesho yawasilishwe kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

3.3.2 Kuhusu Usimamizi na Utekelezaji wa Mikataba ya BRT Awamu ya II

KWA KUWA, Kamati imebaini katika utekelezaji wa BRT Awamu ya II mambo yafuatayo:-

a) Mabadiliko ya muundo wa utekelezaji wa Mkataba wa Huduma, ikiwemo kuhusishwa kwa kampuni nyingine katika utekelezaji wa majukumu bila ushahidi wa kutosha wa idhini ya mamlaka husika;

b) Mapungufu katika nyaraka za makabidhiano ya vituo, maegesho na miundombinu kwa watoa huduma, ikiwemo kutokuwepo kwa saini za pande zote, thamani ya mali zilizokabidhiwa na uthibitisho wa kupokelewa kwa mali hizo; na

c) Kuwepo kwa suala la Kodi ya Mapato ya USD 90,000 linalohusiana na makubaliano ya huduma yenye thamani ya USD 300,000, pamoja na changamoto katika ufuatiliaji wa masharti na mabadiliko ya mikataba;

NA KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa mapungufu hayo yanaweza kusababisha kutokuwa wazi kwa uhalali wa mabadiliko ya mikataba na uwajibikaji wa wahusika, kuathiri usimamizi na ulinzi wa mali za Serikali, kuibua migogoro ya kimkataba, pamoja na kusababisha madeni, tozo au adhabu za kodi na hivyo kuathiri mapato na maslahi ya Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye mapitio ya kina ya mikataba yote ya BRT Awamu ya II, kwa kushirikisha mamlaka na taasisi husika, ili kubaini mabadiliko yote yaliyofanyika baada ya kusainiwa kwa mikataba, uhalali wake, wajibu wa kila upande na athari zake kwa Serikali. Azimio hili likamilike ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya kupitishwa kwa Azimio husika;

b) Serikali ihakikishe kuwa mabadiliko yoyote ya kimkataba, muundo wa SPV au muundo wa kifedha yanaidhinishwa na mamlaka husika kabla ya kutekelezwa, na kuwepo kwa nyaraka za kutosha zinazoonesha uhalali na uwajibikaji wa wahusika; na

c) Serikali kupitia Wakala ihakikishe kuwa makabidhiano yote ya mali na miundombinu ya BRT yanafanyika kwa nyaraka rasmi zinazosainiwa na pande zote, zikionesha orodha na thamani ya mali, hali yake wakati wa makabidhiano na majukumu ya kila upande, na kwa kushirikiana na TRA ihakikishe kuwa masuala yote ya kodi yanayohusiana na mikataba hiyo yanahakikiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa sheria.

3.3.3 Kuhusu Changamoto za Usimamizi wa Ujenzi na Uboreshaji wa Miundombinu ya Viwanja vya Michezo

KWA KUWA, ukaguzi wa miradi ya ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya michezo vya Arusha, Uhuru na Benjamin Mkapa umebaini changamoto katika usanifu na upangaji wa mahitaji ya miradi, ongezeko la gharama za mikataba, kasoro katika tathmini ya zabuni kupitia mfumo wa NeST, dosari katika udhibiti wa ubora, malipo yasiyostahili, kazi ambazo hazijatekelezwa na kutokamilika kwa baadhi ya kazi za mifumo ya umeme, pamoja na kutotekelezwa kikamilifu kwa mapendekezo ya CAG;

NA KWA KUWA, mapungufu hayo yanaweza kusababisha matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma, upotevu wa rasilimali, ongezeko lisilo la lazima la gharama, kushuka kwa

ubora na usalama wa miundombinu, kuchelewa kwa miradi na kudhoofika kwa uwajibikaji katika usimamizi wa ununuzi na mikataba ya Serikali. Na kwa kuwa, ni muhimu kuhakikisha miradi ya miundombinu ya michezo inatekelezwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za ununuzi wa umma, thamani ya fedha, viwango vya ubora na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Serikali;

KWA HIYO BASI, linaazimia kwamba:-

a) Serikali ihakikishe usanifu na mahitaji ya miradi ya viwanja vya michezo yanaandaliwa kwa usahihi kabla ya zabuni, na ongezeko lolote la gharama za mikataba linathibitishwa kitaalamu na kuidhinishwa kwa mujibu wa taratibu;

b) Serikali ichunguze dosari zilizobainika katika tathmini ya zabuni, matumizi ya mfumo wa NeST na uteuzi wa wakandarasi, na kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi. Azimio hili likamilke ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027;

c) Serikali ihakikishe malipo yasiyostahili na fedha zilizolipwa kwa kazi ambazo hazijatekelezwa zinabainishwa na kurejeshwa, na hatua za uwajibikaji zinachukuliwa kwa mujibu wa sheria;

d) Serikali ihakikishe kasoro zote za ubora wa vifaa na kazi za ujenzi zinarekebishwa kwa viwango vya kitaalamu, ikiwemo kukamilisha mifumo ya umeme katika Uwanja

wa Benjamin Mkapa, kabla ya kazi husika kupokelewa rasmi; na

e) Serikali ihakikishe mapendekezo yote ya CAG yanatekelezwa ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 na kuwasilisha kwa Bunge taarifa ya utekelezaji, fedha zilizorejeshwa na hatua zilizochukuliwa za uwajibikaji.

3.3.4 Kuhusu Ufanisi wa Kifedha na Kiutendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa NHIF inakabiliwa na changamoto katika usimamizi wa michango ya waajiri, madai ya watoa huduma, urejeshaji wa fedha zilizotokana na udanganyifu na udhibiti wa matumizi ya vifurushi vya ziada vya mafao. Hadi Juni 2025, michango ya waajiri iliyokuwa inadaiwa ilikuwa Sh. bilioni 104.1, madai yaliyokataliwa yalikuwa Sh. bilioni 70.8, fedha za udanganyifu zilizokuwa zinadaiwa kurejeshwa zilikuwa Sh. bilioni 3.4 na madeni ya matumizi ya ziada yalikuwa Sh.bilioni 20.15;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinaathiri ukwasi na uendelevu wa Mfuko, zinaongeza hatari ya upotevu wa fedha na zinaweza kuchelewesha malipo ya madai halali ya watoa huduma, hivyo kuathiri upatikanaji wa huduma za afya kwa wanachama;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) NHIF ikamilishe ukusanyaji wa salio la michango ya waajiri kiasi cha Sh. bilioni 104.1 na madeni ya matumizi ya ziada ya Sh. bilioni 1.88, pamoja na kushughulikia Sh. bilioni 5.59 zilizobainika kutokuwa madeni halisi kwa kuzingatia taratibu za kihasibu;

b) NHIF ichambue sababu za kukataliwa kwa madai ya watoa huduma na kuimarisha mifumo ya uhakiki na uchakataji wa madai ili kupunguza madai yanayokataliwa na kulipa madai halali kwa wakati;

c) NHIF iikamilishe urejeshaji wa fedha zote zilizotokana na udanganyifu, ikiwemo kuchukua hatua za kisheria kwa wadaiwa husika na kushughulikia madeni yenye mashaka ya kukusanywa kwa mujibu wa viwango vya uhasibu; na

d) NHIF iimarishe udhibiti wa vifurushi vya ziada vya mafao kwa kuzuia utoaji wa huduma bila fedha za kutosha kulipwa mapema na kuhakiki ufanisi wa mfumo wa kielektroniki ulioanzishwa. Maazimio haya yafanyiwe kazi na kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027.

3.3.5 Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa ATCL inakabiliwa na changamoto za madeni makubwa ya wadaiwa, utoaji wa mikopo mipya kwa wateja wenye madeni ya awali, hasara ya uendeshaji na kupungua kwa sehemu ya soko kutokana na

ushindani, licha ya Serikali kuchukua hatua ya kuhamisha umiliki wa ndege kutoka TGFA kwenda ATCL;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinaathiri mtiririko wa fedha, kuongeza gharama za uendeshaji na kuhatarisha uendelevu wa kifedha wa Shirika, hivyo kuchelewesha kufikia lengo la kufanya kazi bila kupata hasara na kuanza kuchangia mapato ya Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ihakikishe ATCL inakamilisha uingizaji wa ndege zilizohamishwa kutoka TGFA katika rejista ya mali na taarifa za hesabu za Shirika, ili kuakisi kwa usahihi umiliki wa mali na kuboresha mizania ya hesabu. Azimio hili likamilike ifikapo au kabla ya tarehe 30 Juni, 2027;
b) ATCL iimarishe ukusanyaji wa madeni ya wadaiwa, idhibiti utoaji wa mikopo kwa wateja wenye madeni yaliyochelewa kulipwa na kuhakikisha huduma za malipo ya baadaye zinatolewa kwa kuzingatia tathmini ya uwezo wa wateja kulipa; na
c) Serikali ihakikishe ATCL inatekeleza mkakati wa kupunguza gharama za uendeshaji, kuongeza mapato na kutumia kikamilifu uwezo wa ndege, njia za safari na "hangar" za matengenezo, ili kuboresha ushindani na kufikia uendelevu wa kifedha.

3.3.6 Kuhusu Usimamizi wa Mikataba na Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma

KWA KUWA, Kamati ilibaini mapungufu katika usimamizi wa mikataba na manunuzi ya umma, yakiwemo malipo ya Shilingi milioni 523.15 kwa kazi za barabara za Chuo Kikuu Mzumbe zisizokidhi viwango; utoaji wa zabuni na mikataba yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.54 na Shilingi bilioni 29.77 kwa wazabuni wasiokidhi kikamilifu vigezo; ununuzi wa pikipiki 700 za chanjo ya mifugo kwa kubadili sifa za kiufundi bila idhini husika; na kuchelewa kukamilika kwa jengo la Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari huku kazi zikiendelea baada ya muda wa mkataba kuisha;

NA KWA KUWA, mapungufu hayo yanaweza kusababisha hasara na matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma, kupungua kwa thamani ya fedha, kuathiri ubora na usalama wa miradi, pamoja na kudhoofisha uwazi na ushindani katika manunuzi ya umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Chuo Kikuu Mzumbe kihakikishe kazi za barabara zinarekebishwa kwa gharama za mkandarasi ili kufikia viwango vya mkataba, na kuimarisha tathmini ya zabuni ili mikataba itolewe kwa wazabuni wanaokidhi vigezo.Azimio hili likamilike ifikapo tarehe 30 Machi, 2027;

b) Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa kushirikiana na GPSA, ihakikishe Shilingi milioni 212.1 zilizobaki zinarejeshwa kabla ya tarehe 31 Disemba, 2026 na mabadiliko ya sifa za kiufundi za bidhaa yanafanyika kwa kufuata taratibu na kupata idhini husika;

c) Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ihakikishe jengo linakamilika kwa viwango vinavyotakiwa, dosari zinarekebishwa na makabidhiano rasmi yanafanyika baada ya kuthibitisha ubora na usalama wake; na

d) Serikali kupitia PPRA ifanye ukaguzi wa mara kwa mara katika taasisi zote za umma ili kubaini ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma, na kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa kwa wahusika ili kuimarisha usimamizi wa mikataba, kulinda fedha za umma na kupata thamani ya fedha.

3.3.7 Kuhusu Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani Katika Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC)

KWA KUWA, Kamati imebaini mapungufu katika usimamizi wa mali na bidhaa, matumizi yasiyokidhi matakwa ya Mfumo wa ERMS, usuluhishi na urejeshaji wa madeni, uzingatiaji wa sheria za kodi, pamoja na ukiukwaji wa taratibu za ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba;

NA KWA KUWA , Changamoto hizo zinasababisha udhaifu katika udhibiti na uwajibikaji wa mali na fedha za Kampuni,

kuongeza hatari ya upotevu wa mali, kuathiri usahihi wa taarifa za fedha na urejeshaji wa madeni, kusababisha madeni ya kodi na adhabu, pamoja na kuongeza hatari ya ukiukwaji wa taratibu za manunuzi na kuisababishia Kampuni hasara za kifedha;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) TFC iandae, iidhinishe na kutekeleza mwongozo wa usimamizi wa bidhaa na mali, na kuhakikisha ERMS inatumika kikamilifu katika usimamizi wa bidhaa, mali, magari na manunuzi. Azimio hili likamilike kabla ya tarehe 31 Disemba, 2026;
b) Ndani ya Mwaka wa Fedha, 2026/2027, TFC ihakiki na kusuluhisha kumbukumbu za mali na madeni, ikiwemo madeni ya Shilingi bilioni 5.40, tofauti ya Shilingi milioni 100 na salio la msamaha wa madeni la Shilingi bilioni 4.55, na kuweka mpango wa urejeshaji wa madeni;
c) TFC ihakikishe malipo ya watumishi yanazingatia sheria za kodi na, kwa kushirikiana na TRA, kushughulikia PAYE ya Shilingi bilioni 2.09; na
d) TFC izingatie sheria na taratibu za ununuzi wa umma, ikiwemo kuthibitisha uhalali wa matumizi ya mzabuni mmoja na kuhakikisha mikataba inapitiwa kisheria, kuidhinishwa na kusainiwa kabla ya kupokea bidhaa au huduma.

3.3.8 Kuhusu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF)

KWA KUWA, Kamati imebaini kwamba:-

a) TACAF haina Sheria maalum ya uanzishwaji, Mpango Mkakati wa Mfuko, na Bodi ya Wadhamini tangu kumalizika kwa muda wa uongozi tarehe 24 Julai 2024;
b) TACAF ina madeni ya mikopo ya muda mrefu yenye jumla ya Sh.765,935,433, na imelazimika kulipa Sh.88,325,998 kwa niaba ya wadaiwa kutokana na kushindwa kurejesha mikopo; na
c) TACAF haina mfumo wake wa kielektroniki wa kusimamia maombi, utoaji, ufuatiliaji na marejesho ya mikopo, na badala yake inategemea mifumo ya NBC na CRDB.

NA KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa hali hizo zinaathiri uwajibikaji na mwelekeo wa kimkakati wa TACAF, kufungwa kwa fedha za Mfuko na kupungua kwa uwezo wa kutoa mikopo mipya, pamoja na kuongezeka kwa mikopo chechefu kutokana na udhaifu wa ufuatiliaji wa mikopo na marejesho.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Wizara yenye dhamana ya Utamaduni na Sanaa ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 iharakishe kuweka TACAF katika muundo rasmi wa kitaasisi, kuteua Bodi ya

Wadhamini na kuhakikisha Mpango Mkakati wa Mfuko unakamilishwa na kutekelezwa;

b) TACAF itekeleze mpango wa kurejesha madeni ya Sh.765,935,433 na Sh.88,325,998 zilizolipwa kwa niaba ya wadaiwa, kwa kuweka ratiba na muda wa marejesho unaopimika, pamoja na kuimarisha tathmini na ufuatiliaji wa wakopaji; na

c) TACAF ikamilishe na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa mikopo utakaowezesha maombi, utoaji, ufuatiliaji na marejesho ya mikopo kwa ufanisi.

3.3.9 Kuhusu Usimamizi wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL)

KWA KUWA, Bunge limebaini kwamba:-

a) Baadhi ya vyanzo vya mapato ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii havikuanza kutumika na madeni ya Tozo ya Shilingi 13,675,174,229 hayakuwa yamekusanywa;

b) Matumizi ya fedha za Tozo hayakuzingatia mgawanyo uliowekwa katika Kanuni ya 10, ambapo ni asilimia 14 tu iliyotumika kwenye maendeleo ya miundombinu badala ya asilimia 50;

c) Shilingi 14,632,168,740.94 zilitumika bila ushauri wa Kamati ya Ushauri ya Utalii (TAC), huku Shilingi

38,359,450,969 kati ya Shilingi 52,991,619,710 zilizokusanywa zikibaki bila kutumika; na

d) maagizo ya Bunge kuhusu mageuzi ya kimuundo ya usimamizi wa Tozo, ikiwemo kuandaa mpango mkakati, mpango kazi, bajeti na ratiba ya utekelezaji, hayakutekelezwa kikamilifu, hali iliyosababisha shughuli za Tozo kuendelea kusitishwa.

NA KWA KUWA, Kamati imebaini kwamba hoja hizo zimesababisha kutokusanywa kwa mapato yaliyokusudiwa, matumizi ya fedha nje ya vipaumbele vilivyowekwa, fedha za umma kutotumika kwa wakati na kuongeza hatari ya matumizi yasiyo na tija, pamoja na kudhoofisha usimamizi, uwajibikaji na ufanisi wa Tozo katika kuendeleza sekta ya utalii.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Wizara ya Maliasili na Utalii ihakikishe ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 vyanzo vyote vya Tozo vinafanya kazi na kukusanya kikamilifu mapato, ikiwemo madeni ya Shilingi 13,675,174,229;
b) Wizara ihakikishe fedha za Tozo zinatumika kwa kuzingatia mgawanyo uliowekwa kisheria na kwa kupata ushauri unaotakiwa wa TAC;
c) Wizara ihakikishe fedha ambazo hazijatumika zinaelekezwa kwenye shughuli zilizoidhinishwa na kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi ili kupata thamani ya fedha za umma; na

d) Wizara ikamilishe mageuzi ya kimuundo ya usimamizi wa Tozo ya Utalii na kutekeleza mpango mkakati, mpango kazi, bajeti na ratiba ya utekelezaji, na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Kamati husika za Bunge ndani ya miezi sita.

3.3.10 Kuhusu Mkataba wa Upangishaji Ardhi Kati ya Chuo Kikuu Dar es Salaam na Mlimani City Holding Limited (MHL)

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa mkataba wa upangishaji wa ardhi kati ya UDSM na Mlimani City Holding Limited (MHL) haujafafanua maana ya pango ghafi *(Gross Rent),* ongezeko la pango la kila mwaka halikutekelezwa, na mkataba haujaweka bayana utaratibu wa kushughulikia majengo, miundombinu na haki za kila upande utakapomalizika;

NA KWA KUWA, mapungufu hayo yanaweza kusababisha Chuo kukosa mapato yanayostahili, kuibua migogoro ya kimkataba na kuhatarisha maslahi ya Chuo katika umiliki na matumizi ya mali zake baada ya mkataba kumalizika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali, kupitia Wizara yenye dhamana na Chuo Kikuu Dar es Salaam, ikamilishe mapitio ya mkataba wa MHL ndani ya miezi sita tangu kupitishwa kwa Azimio hili, kwa kuweka bayana msingi wa ukokotoaji wa pango ghafi, utekelezaji wa ongezeko la pango la kila mwaka, na haki

na wajibu wa kila upande mwishoni mwa mkataba, ikiwemo umiliki, uthamini na makabidhiano ya majengo na miundombinu; na

b) Chuo Kikuu Dar es Salaam, kwa kushirikiana na mamlaka husika, kifanye uhakiki wa malipo yote ya pango yaliyofanyika, ibaini kiasi chochote kinachodaiwa kutokana na kutotekelezwa kwa masharti ya mkataba na kuchukua hatua za kukidai, na kuwasilisha taarifa ya matokeo ya mapitio ya mkataba pamoja na hatua za utekelezaji kwa Bunge ndani ya miezi sita.

3.3.11 Kuhusu Mapungufu katika Usajili, Udhibiti na Usimamizi wa Mali za Serikali

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwepo kwa mapungufu katika usimamizi wa mali za Serikali katika Taasisi na Wizara mbalimbali, ikiwemo Taasisi za Elimu, Wizara,Idara na Mashirika ya Umma yanayohusisha kutokukamilika kwa usajili na uhakiki wa mali, kutokuwa sahihi kwa kumbukumbu za mali, changamoto za uthamini na umiliki, pamoja na mali kutotumika kwa tija iliyokusudiwa;

NA KWA KUWA, mapungufu hayo yanaweza kusababisha upotevu, matumizi yasiyoidhinishwa na kutotumika ipasavyo kwa mali za Serikali, kudhoofisha udhibiti na uwajibikaji,

pamoja na kuisababishia Serikali hasara na kukosa manufaa yaliyokusudiwa kutokana na uwekezaji wa umma.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ihakikishe ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara, Idara, Wakala na Taasisi zote za Umma zinafanya uhakiki na sensa ya mali zake, kukamilisha usajili na uingizaji wa mali katika GAMIS na rejesta za mali, kuthibitisha umiliki na thamani ya mali, na kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji wa matumizi na hali ya mali hizo; na

b) Wizara ya Fedha isimamie zoezi hilo kwa kuweka muda maalumu wa utekelezaji, kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Bunge na kuhakikisha hatua za kiutawala na kisheria zinachukuliwa kwa watumishi watakaobainika kuwajibika kwa upotevu au usimamizi usiofaa wa mali za Serikali.

3.3.12 Kuhusu Uzingatiaji wa Viwango vya IPSAS na IFRS katika Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Taasisi za Umma

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwepo kwa mapungufu katika uandaaji wa taarifa za fedha za baadhi ya taasisi za umma, ikiwemo kutotambua kwa wakati mali, madeni, mapato, matumizi na majukumu ya kifedha; kutofanya tathmini ya uchakavu na upungufu wa thamani ya mali kwa wakati;

pamoja na kutokulingana kwa taarifa zinazotokana na mifumo mbalimbali ya uhasibu na usimamizi wa mali, hali inayoonesha kutokuzingatiwa kikamilifu kwa matakwa ya viwango vya IPSAS na IFRS vinavyohusika;

NA KWA KUWA, mapungufu hayo yanaweza kusababisha taarifa za fedha kutokuwa sahihi, kamili na zinazoaminika, kudhoofisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma, na kuathiri ubora wa maamuzi ya Serikali kuhusu usimamizi wa mali, madeni na matumizi ya fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ihakikishe kuwa katika hesabu za mwaka wa fedha 2026/2027 taasisi zote za umma zinazingatia matakwa ya IPSAS au IFRS, kulingana na mfumo husika, katika utambuzi, upimaji na uwasilishaji sahihi wa taarifa za fedha;
b) Serikali ihakikishe mifumo ya uhasibu, usimamizi wa mali na mapato inaunganishwa na kuhuishwa, na taarifa zake zinalinganishwa mara kwa mara ili kubaini na kurekebisha tofauti kabla ya taarifa za fedha kuwasilishwa kwa ukaguzi.

3.3.13 Kuhusu Changamoto za Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA Katika Taasisi za Serikali

KWA KUWA, ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA katika taasisi mbalimbali za Serikali ulibaini mapungufu katika usalama na urejeshaji wa mifumo baada ya maafa, usimamizi wa watumiaji, uunganishaji na matumizi ya mifumo, ukamilifu wa

taarifa, pamoja na usimamizi wa mapato, malipo, faini, leseni, miradi na mikataba;

NA KWA KUWA, mapungufu hayo yanaweza kusababisha upotevu wa taarifa, makosa na tofauti za kumbukumbu za fedha, upotevu wa mapato, ongezeko la gharama za uendeshaji, ucheleweshaji wa huduma na kudhoofisha udhibiti wa ndani na uwajibikaji;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ihakikishe ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 taasisi zote za umma zinaimarisha usalama na usimamizi wa mifumo ya TEHAMA, ikiwemo udhibiti wa watumiaji, ufuatiliaji wa miamala, mipango ya kurejesha mifumo baada ya maafa na upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati;
b) Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya TEHAMA na Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) ihakikishe taasisi zinatumia mifumo inayokidhi mahitaji yake, inaunganishwa ipasavyo na inawasiliana kwa ufanisi, huku e-GA ikitoa utaalamu, viwango na huduma za pamoja ili kupunguza kujirudia rudia kwa mifumo na gharama za uendeshaji;
c) Serikali ihakikishe mifumo ya mapato, malipo, faini, leseni, miradi na mikataba inawezesha uthibitishaji wa miamala, usuluhishi wa kumbukumbu na ufuatiliaji wa

mapato na matumizi kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma;

d) Wakuu wa taasisi za Serikali wahakikishe kasoro za TEHAMA zilizobainishwa na ukaguzi zinarekebishwa kwa wakati kupitia mipango yenye hatua, muda wa utekelezaji na watendaji wanaowajibika, na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwa mamlaka husika; na

e) Wizara yenye dhamana ya TEHAMA na e-GA, kwa kushirikiana na CAG na taasisi husika kulingana na majukumu yao, ziimarishe ufuatiliaji na tathmini ya mifumo ya TEHAMA ili kuhakikisha usalama, ufanisi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma na usimamizi wa rasilimali za umma.

3.3.14 Kuhusu Utata wa Kisheria na Kiutendaji Katika Usimamizi wa Mapato Yasiyotokana na Utalii na Mapato ya Uwekezaji wa NCAA

KWA KUWA, Kamati imebaini kutokuwepo kwa utaratibu rasmi wa kisheria unaobainisha mamlaka yenye wajibu wa kukusanya, kutunza na kuwasilisha mapato yasiyotokana na utalii, pamoja na utaratibu wa kushughulikia mapato yatokanayo na uwekezaji wa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA);

NA KWA KUWA, hali hiyo inaweza kusababisha utata wa kisheria na kiutendaji, udhaifu katika usimamizi na udhibiti wa

mapato, pamoja na changamoto katika uwajibikaji na ufuatiliaji wa mapato hayo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, ifikapo tarehe 30 Machi, 2027 NCAA, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), iweke utaratibu rasmi wa kisheria au Mkataba wa Makubaliano (MoU) unaobainisha wazi majukumu ya kila upande katika ukusanyaji, utunzaji, uwasilishaji na usimamizi wa mapato hayo.

3.3.15 Kuhusu Kutokuwepo kwa Ulinganifu katika Ukokotoaji wa Mafao ya Pensheni kwa Wanachama Wanaounganisha Vipindi vya Michango

KWA KUWA, Kamati imebaini kutokuwepo kwa ulinganifu katika tafsiri na matumizi ya masharti ya Sheria ya PSSSF na miongozo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuhusu msingi wa kubaini Malipo ya Mwaka Yanayostahili Pensheni (APE) kwa wanachama wanaounganisha vipindi vya michango;

NA KWA KUWA, hali hiyo inaweza kusababisha wanachama wenye mazingira yanayofanana kuhesabiwa mafao kwa misingi tofauti na hivyo kulipwa mafao yasiyoendana na stahili zao;

KWA HIYO BASI, Serikali kupitia Wizara yenye dhamana na masuala ya kazi na pensheni, kwa kushirikiana na PSSSF na NSSF, itoe ufafanuzi rasmi kuhusu msingi sahihi wa kukokotoa

malipo ya APE na kuhakikisha kuwa mafao yaliyokokotolewa kwa misingi inayotofautiana yanapitiwa na kurekebishwa pale itakapobainika kuwepo kwa malipo yaliyozidi au kuwa pungufu ya stahili za wanachama. Azimio hili likamilike kabla au ifikapo tarehe 30 Machi, 2027.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini. Uongozi wako umeiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Devotha Mathew Minja, Mb - Mwenyekiti
2) Mhe. Khalfan Hilaly Aeshi, Mb – M/ Mwenyekiti
3) Mhe. Japhet Ngailango Hasunga,Mb
4) Mhe. Juma Othman Hija, Mb
5) Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
6) Mhe. Sheila Edward Lukuba, Mb
7) Mhe. Asha Salum Motto, Mb
8) Mhe. Thomas Mvano Alan, Mb

9) Mhe. Morris Joseph Makoi, Mb
10) Mhe. Mohamed Mussa Utaly, Mb
11) Mhe. Charles Mhando Njama, Mb
12) Mhe. Ali Haidar Madeweyya, Mb
13) Mhe. Shah Bolisha Mahesh, Mb
14) Mhe. Bazilio Kapunda Mbwilo, Mb
15) Mhe. Latifa Khamis Juakali, Mb
16) Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb
17) Mhe.Marirta Gido Kivunge, Mb
18) Mhe. Grace Elias Mkoma, Mb
19) Mhe. Beng'I Mazana Issa,Mb
20) Mhe. Shaame Ali , Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka I. Leonard, kwa uongozi wake na uratibu madhubuti wa Sekretarieti ya Bunge, uliochangia kufanikisha shughuli za Kamati na utekelezaji wa majukumu ya Bunge kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), chini ya uongozi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere, kwa kutekeleza jukumu lake la kikatiba la kukagua hesabu za Serikali na kuwasilisha ripoti za ukaguzi kwa Kamati. Ripoti hizo zimekuwa msingi muhimu katika uchambuzi wa Kamati na kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Wizara ya Fedha, kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG), Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen), Kurugenzi ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM), Kamishna wa Bajeti na Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, kwa kuratibu maandalizi ya majibu ya hoja za ukaguzi yaliyowasilishwa na Maafisa Masuuli.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati inatoa shukrani kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina, iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Wizara ya Mipango na Uwekezaji, kwa ushirikiano wake katika kuwezesha upatikanaji wa majibu na ufafanuzi wa hoja za ukaguzi zinazohusu taasisi zilizo chini ya usimamizi wake. Kadhalika, Kamati inatoa shukrani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu kwa kuratibu ratiba za mahojiano na Maafisa Masuuli, yaliyoiwezesha Kamati kupata ufafanuzi wa hoja za ukaguzi na kutekeleza majukumu yake ya kibunge kwa ufanisi.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Khalfan Hilaly Aeshi, Mb
MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)

02 Novemba, 2026

AMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)

RANDAMA YA KWANZA

JEDWALI LA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU TAARIFA ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (PAC) KWA UKAGUZI WA SERIKALI KUU, MASHIRIKA YA UMMA NA KAGUZI ZA UFANISI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2024 NA TAREHE 30 JUNI 2025

NOVEMBA, 2026

RANDAMA YA MAPENDEKEZO YA KAMATI

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
1.	Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato.	a) Kucheleweshaji upatikanaji wa uamuzi wa mwisho kuhusu madeni ya kodi na kuongeza mlundikano wa mashauri, hivyo kuathiri uhakika wa mapato ya Serikali na kuongeza gharama kwa walipa kodi; b) Kusababisha upotevu au ucheleweshaji wa mapato ya Serikali kutokana na kodi kutokadiriwa kwa usahihi na	a) Ndani ya mwaka wa fedha 2026/ 2027 TRA ihakikishe mashauri yote ya kodi ambayo hayajatatuliwa yanafuatiliwa kwa mfumo madhubuti wa usimamizi wa mashauri, kwa kuweka muda maalum wa utekelezaji na kupunguza kwa hatua mlundikano wa mashauri yaliyochelewa; b) TRA iimarishe mifumo ya uhakiki na udhibiti wa ubora wa tathmini za kodi ili kuhakikisha kodi inayostahili inalipwa kwa usahihi na kiasi cha Sh.8,310,477,597 ambacho hakikuthibitishwa kikamilifu kinafanyiwa uhakiki na hatua stahiki kwa

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
		udhaifu katika uhakiki wa taarifa za walipa kodi; c) Kuongeza hatari ya mafuta yanayosafirishwa kwa transit kuingia katika matumizi ya ndani bila kulipiwa kodi na hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali; d) Kuchelewesha utambuzi na ukusanyaji wa madeni ya kodi na kuongeza hatari ya baadhi ya madai ya kodi kupoteza uhalali kutokana na muda mrefu wa kutokufanyiwa ukaguzi; na	mujibu wa sheria zinachukuliwa; c) TRA na mamlaka nyingine zinazohusika ziimarishe mfumo wa ufuatiliaji wa mafuta yanayosafirishwa kwa "transit" kutoka kituo cha kuingilia hadi kituo cha kutoka, na kuhakikisha kodi inayostahili kwa lita milioni 14 zilizobainika hazikuthibitishwa inakusanywa; d) TRA ihakikishe ukaguzi wa kodi unafanyika kwa wakati, hasa kwa kuzingatia muda uliowekwa na sheria, na iweke mfumo wa ufuatiliaji wa kesi za ukaguzi ili kuzuia ucheleweshaji wa muda mrefu; na e) TRA ichukue hatua stahiki dhidi ya walipa kodi 17,573 ambao

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
		e) Kudhoofisha uzingatiaji wa sheria za kodi na kuathiri ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kutokana na kutowasilishwa kwa marejesho ya VAT kwa wakati.	hawakuwasilisha marejesho 93,953 ya VAT na iimarishe mifumo ya ufuatiliaji ili marejesho yawasilishwe kwa wakati kwa mujibu wa sheria.
2.	Kuhusu Usimamizi na Utekelezaji wa Mikataba ya BRT Awamu ya II	Kamati imebaini kuwa mapungufu hayo yanaweza kusababisha kutokuwa wazi kwa uhalali wa mabadiliko ya mikataba na uwajibikaji wa wahusika, kuathiri usimamizi na ulinzi wa mali za Serikali, kuibua migogoro ya kimkataba, pamoja na kusababisha madeni, tozo au	a) CAG afanye mapitio ya kina ya mikataba yote ya BRT Awamu ya II, kwa kushirikisha mamlaka na taasisi husika, ili kubaini mabadiliko yote yaliyofanyika baada ya kusainiwa kwa mikataba, uhalali wake, wajibu wa kila upande na athari zake kwa Serikali. Azimio hili likamilike ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya kupitishwa kwa Azimio husika;

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
		adhabu za kodi na hivyo kuathiri mapato na maslahi ya Serikali;	b) Serikali ihakikishe kuwa mabadiliko yoyote ya kimkataba, muundo wa SPV au muundo wa kifedha yanaidhinishwa na mamlaka husika kabla ya kutekelezwa, na kuwepo kwa nyaraka za kutosha zinazoonesha uhalali na uwajibikaji wa wahusika; na c) Serikali kupitia Wakala ihakikishe kuwa makabidhiano yote ya mali na miundombinu ya BRT yanafanyika kwa nyaraka rasmi zinazosainiwa na pande zote, zikionesha orodha na thamani ya mali, hali yake wakati wa makabidhiano na majukumu ya kila upande, na kwa kushirikiana na TRA ihakikishe kuwa masuala yote ya kodi yanayohusiana na

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			mikataba hiyo yanahakikiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa sheria.
3.	Kuhusu Changamoto za Usimamizi wa Ujenzi na Uboreshaji wa Miundombinu ya Viwanja vya Michezo	Mapungufu hayo yanaweza kusababisha matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma, upotevu wa rasilimali, ongezeko lisilo la lazima la gharama, kushuka kwa ubora na usalama wa miundombinu, kuchelewa kwa miradi na kudhoofika kwa uwajibikaji katika usimamizi wa ununuzi na mikataba ya Serikali. Aidha, ni muhimu kuhakikisha miradi ya miundombinu ya michezo inatekelezwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za	a) Serikali ihakikishe usanifu na mahitaji ya miradi ya viwanja vya michezo yanaandaliwa kwa usahihi kabla ya zabuni, na ongezeko lolote la gharama za mikataba linathibitishwa kitaalamu na kuidhinishwa kwa mujibu wa taratibu; b) Serikali ichunguze dosari zilizobainika katika tathmini ya zabuni, matumizi ya mfumo wa NeST na uteuzi wa wakandarasi, na kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi. Azimio hili likamilke ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
		ununuzi wa umma, thamani ya fedha, viwango vya ubora na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Serikali;	c) Serikali ihakikishe malipo yasiyostahili na fedha zilizolipwa kwa kazi ambazo hazijatekelezwa zinabainishwa na kurejeshwa, na hatua za uwajibikaji zinachukuliwa kwa mujibu wa sheria; d) Serikali ihakikishe kasoro zote za ubora wa vifaa na kazi za ujenzi zinarekebishwa kwa viwango vya kitaalamu, ikiwemo kukamilisha mifumo ya umeme katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, kabla ya kazi husika kupokelewa rasmi; na e) Serikali ihakikishe mapendekezo yote ya CAG yanatekelezwa ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 na kuwasilisha kwa Bunge taarifa ya

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			utekelezaji, fedha zilizorejeshwa na hatua zilizochukuliwa za uwajibikaji.
4.	Kuhusu Ufanisi wa Kifedha na Kiutendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)	changamoto hizo zinaathiri ukwasi na uendelevu wa Mfuko, zinaongeza hatari ya upotevu wa fedha na zinaweza kuchelewesha malipo ya madai halali ya watoa huduma, hivyo kuathiri upatikanaji wa huduma za afya kwa wanachama;	a) NHIF ikamilishe ukusanyaji wa salio la michango ya waajiri kiasi cha Sh. bilioni 1.95 na madeni ya matumizi ya ziada ya Sh. bilioni 1.88, pamoja na kushughulikia Sh. bilioni 5.59 zilizobainika kutokuwa madeni halisi kwa kuzingatia taratibu za uhasibu; b) NHIF ichambue sababu za kukataliwa kwa madai ya watoa huduma na kuimarisha mifumo ya uhakiki na uchakataji ili kupunguza madai yanayokataliwa na kulipa madai halali kwa wakati; c) NHIF iikamilishe urejeshaji wa fedha

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			zote zilizotokana na udanganyifu, ikiwemo kuchukua hatua za kisheria kwa wadaiwa husika na kushughulikia madeni yenye mashaka ya kukusanywa kwa mujibu wa viwango vya uhasibu; na d) NHIF iimarishe udhibiti wa vifurushi vya ziada vya mafao kwa kuzuia utoaji wa huduma bila fedha za kutosha kulipwa mapema na kuhakiki ufanisi wa mfumo wa kielektroniki ulioanzishwa. Maazimio haya yafanyiwe kazi na kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027
5.	Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)	changamoto hizo zinaathiri mtiririko wa fedha, kuongeza gharama za uendeshaji na	a) Serikali ihakikishe ATCL inakamilisha uingizaji wa ndege zilizohamishwa kutoka TGFA katika rejista ya mali na

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
		kuhatarisha uendelevu wa kifedha wa Shirika, hivyo kuchelewesha kufikia lengo la kufanya kazi bila kupata hasara na kuanza kuchangia mapato ya Serikali.	taarifa za hesabu za Shirika, ili kuakisi kwa usahihi umiliki wa mali na kuboresha mizania ya hesabu. Azimio hili likamilike ifikapo au ya kabla ya tarehe 30 Juni, 2027; b) ATCL iimarishe ukusanyaji wa madeni ya wadaiwa, idhibiti utoaji wa mikopo kwa wateja wenye madeni yaliyochelewa kulipwa na kuhakikisha huduma za malipo ya baadaye zinatolewa kwa kuzingatia tathmini ya uwezo wa wateja kulipa; na c) Serikali ihakikishe ATCL inatekeleza mkakati wa kupunguza gharama za uendeshaji, kuongeza mapato na kutumia kikamilifu uwezo wa ndege,

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			njia za safari na "hangar" za matengenezo, ili kuboresha ushindani na kufikia uendelevu wa kifedha.
6.	Kuhusu Usimamizi wa Mikataba na Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma	Mapungufu hayo yanaweza kusababisha hasara na matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma, kupungua kwa thamani ya fedha, kuathiri ubora na usalama wa miradi, pamoja na kudhoofisha uwazi na ushindani katika manunuzi ya umma;	a) Chuo Kikuu Mzumbe kihakikishe kazi za barabara zinarekebishwa kwa gharama za mkandarasi ili kufikia viwango vya mkataba, na kuimarisha tathmini ya zabuni ili mikataba itolewe kwa wazabuni wanaokidhi vigezo.Agizo hili likamilike ifikapo tarehe 30 Machi, 2027; b) Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa kushirikiana na GPSA, ihakikishe Shilingi milioni 212.1 zilizobaki zinarejeshwa ifikapo au kabla ya

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			tarehe 31 Disemba, 2026 na mabadiliko ya sifa za kiufundi za bidhaa yanafanyika kwa kufuata taratibu na kupata idhini husika; c) Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ihakikishe jengo linakamilika kwa viwango vinavyotakiwa, dosari zinarekebishwa na makabidhiano rasmi yanafanyika baada ya kuthibitisha ubora na usalama wake; na d) Serikali kupitia PPRA ifanye ukaguzi wa mara kwa mara katika taasisi zote za umma ili kubaini ukiukwaji wa Sheria na

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			Kanuni za Ununuzi wa Umma, na kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa kwa wahusika ili kuimarisha usimamizi wa mikataba, kulinda fedha za umma na kupata thamani ya fedha.
7.	Kuhusu Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani Katika Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC).	Changamoto hizo zinasababisha udhaifu katika udhibiti na uwajibikaji wa mali na fedha za Kampuni, kuongeza hatari ya upotevu wa mali, kuathiri usahihi wa taarifa za fedha na urejeshaji wa madeni, kusababisha madeni ya kodi na adhabu, pamoja na kuongeza hatari ya ukiukwaji wa	a) TFC iandae, iidhinishe na kutekeleza mwongozo wa usimamizi wa bidhaa na mali, na kuhakikisha ERMS inatumika kikamilifu katika usimamizi wa bidhaa, mali, magari na manunuzi. Azimio hili likamilike kabla ya tarehe 31 Disemba, 2026.; b) TFC ihakiki na kusuluhisha kumbukumbu za mali na madeni,

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
		taratibu za manunuzi na kuisababishia Kampuni hasara za kifedha;	ikiwemo madeni ya Shilingi bilioni 5.40, tofauti ya Shilingi milioni 100 na salio la msamaha wa madeni la Shilingi bilioni 4.55, na kuweka mpango wa urejeshaji wa madeni; c) TFC ihakikishe malipo ya watumishi yanazingatia sheria za kodi na, kwa kushirikiana na TRA, kushughulikia PAYE ya Shilingi bilioni 2.09; na d) TFC izingatie sheria na taratibu za ununuzi wa umma, ikiwemo kuthibitisha uhalali wa matumizi ya mzabuni mmoja na kuhakikisha mikataba inapitiwa kisheria, kuidhinishwa na kusainiwa kabla ya kupokea bidhaa au huduma.

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
8.	Kuhusu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF).	Kamati imebaini kuwa hali hizo zinaathiri uwajibikaji na mwelekeo wa kimkakati wa TACAF, kufungwa kwa fedha za Mfuko na kupungua kwa uwezo wa kutoa mikopo mipya, pamoja na kuongezeka kwa mikopo chechefu kutokana na udhaifu wa ufuatiliaji wa mikopo na marejesho.	a) Wizara yenye dhamana ya Utamaduni na Sanaa ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 iharakishe kuweka TACAF katika muundo rasmi wa kitaasisi, kuteua Bodi ya Wadhamini na kuhakikisha Mpango Mkakati wa Mfuko unakamilishwa na kutekelezwa; b) TACAF itekeleze mpango wa kurejesha madeni ya Sh.765,935,433 na Sh.88,325,998 zilizolipwa kwa niaba ya wadaiwa, kwa kuweka ratiba na muda wa marejesho unaopimika, pamoja na kuimarisha tathmini na ufuatiliaji wa wakopaji; na c) TACAF ikamilishe na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa usimamizi

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			wa mikopo utakaowezesha maombi, utoaji, ufuatiliaji na marejesho ya mikopo kwa ufanisi.
9.	Kuhusu Usimamizi wa Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL)	Kamati imebaini kwamba hoja hizo zimesababisha kutokusanywa kwa mapato yaliyokusudiwa, matumizi ya fedha nje ya vipaumbele vilivyowekwa, fedha za umma kutotumika kwa wakati na kuongeza hatari ya matumizi yasiyo na tija, pamoja na kudhoofisha usimamizi, uwajibikaji na ufanisi wa Tozo katika kuendeleza sekta ya utalii.	a) Wizara ya Maliasili na Utalii ndani ya mwaka waa fedha 2026/2027 ihakikishe vyanzo vyote vya Tozo vinafanya kazi na kukusanya kikamilifu mapato, ikiwemo madeni ya Shilingi 13,675,174,229; b) Wizara ihakikishe fedha za Tozo zinatumika kwa kuzingatia mgawanyo uliowekwa kisheria na kwa kupata ushauri unaotakiwa wa TAC; c) Wizara ihakikishe fedha ambazo hazijatumika zinaelekezwa kwenye shughuli zilizoidhinishwa na kuimarisha

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			ufuatiliaji wa matumizi ili kupata thamani ya fedha za umma; na d) Wizara ikamilishe mageuzi ya kimuundo ya usimamizi wa Tozo ya Utalii na kutekeleza mpango mkakati, mpango kazi, bajeti na ratiba ya utekelezaji, na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Kamati husika ndani ya miezi sita.
10.	Kuhusu Mkataba wa Upangishaji Ardhi Kati ya Chuo Kikuu Dar es Salaam na Mlimani City Holding Limited (MHL)	Mapungufu hayo yanaweza kusababisha Chuo kukosa mapato yanayostahili, kuibua migogoro ya kimkataba na kuhatarisha maslahi ya Chuo katika umiliki na matumizi ya mali zake baada ya mkataba kumalizika;	a) Serikali, kupitia Wizara yenye dhamana na Chuo Kikuu Dar es Salaam, ikamilishe mapitio ya mkataba wa MHL ndani ya miezi sita tangu kupitishwa kwa Azimio hili, kwa kuweka bayana msingi wa ukokotoaji wa pango ghafi, utekelezaji wa ongezeko la pango la kila mwaka, na haki na wajibu wa kila

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			upande mwishoni mwa mkataba, ikiwemo umiliki, uthamini na makabidhiano ya majengo na miundombinu; na b) Chuo Kikuu Dar es Salaam, kwa kushirikiana na mamlaka husika, ihakiki malipo yote ya pango yaliyofanyika, ibaini kiasi chochote kinachodaiwa kutokana na kutotekelezwa kwa masharti ya mkataba na kuchukua hatua za kukidai, na kuwasilisha taarifa ya matokeo ya mapitio ya mkataba pamoja na hatua za utekelezaji kwa Bunge ndani ya miezi sita.
11.	Kuhusu Mapungufu katika Usajili,	Mapungufu hayo yanaweza kusababisha upotevu, matumizi	a) Serikali ihakikishe ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara, Idara,

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
	Udhibiti na Usimamizi wa Mali za Serikali.	yasiyoidhinishwa na kutotumika ipasavyo kwa mali za Serikali, kudhoofisha udhibiti na uwajibikaji, pamoja na kuisababishia Serikali hasara na kukosa manufaa yaliyokusudiwa kutokana na uwekezaji wa umma.	Wakala na Taasisi zote za Umma zinafanya uhakiki na sensa ya mali zake, kukamilisha usajili na uingizaji wa mali katika GAMIS na rejesta za mali, kuthibitisha umiliki na thamani ya mali, na kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji wa matumizi na hali ya mali hizo; na b) Wizara ya Fedha isimamie zoezi hilo kwa kuweka muda maalumu wa utekelezaji, kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Serikali na kuhakikisha hatua za kiutawala na kisheria zinachukuliwa kwa watumishi watakaobainika kuwajibika kwa upotevu au usimamizi usiofaa wa mali

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			za Serikali.
12.	Kuhusu Uzingatiaji wa Viwango vya IPSAS na IFRS katika Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Taasisi za Umma.	Mapungufu hayo yanaweza kusababisha taarifa za fedha kutokuwa sahihi, kamili na zinazoaminika, kudhoofisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma, na kuathiri ubora wa maamuzi ya Serikali kuhusu usimamizi wa mali, madeni na matumizi ya fedha za umma.	a) Serikali ihakikishe kuwa ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 kuwa katika hesabu za mwaka wa fedha 2026/2027 taasisi zote za umma zinazingatia IPSAS au IFRS, kulingana na mfumo husika, katika utambuzi, upimaji na uwasilishaji sahihi wa taarifa za fedha; b) Serikali ihakikishe mifumo ya uhasibu, usimamizi wa mali na mapato inaunganishwa na kuhuishwa, na taarifa zake zinalinganishwa mara kwa mara ili kubaini na kurekebisha tofauti kabla ya taarifa za fedha kuwasilishwa kwa ukaguzi.

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
13.	Kuhusu Changamoto za Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA Katika Taasisi za Serikali.	Mapungufu hayo yanaweza kusababisha upotevu wa taarifa, makosa na tofauti za kumbukumbu za fedha, upotevu wa mapato, ongezeko la gharama za uendeshaji, ucheleweshaji wa huduma na kudhoofisha udhibiti wa ndani na uwajibikaji.	a) Serikali ihakikishe ndani ya mwaka wa fedha 2026/ 2027 taasisi zote za umma zinaimarisha usalama na usimamizi wa mifumo ya TEHAMA, ikiwemo udhibiti wa watumiaji, ufuatiliaji wa miamala, mipango ya kurejesha mifumo baada ya maafa na upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati; b) Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya TEHAMA na Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) ihakikishe taasisi zinatumia mifumo inayokidhi mahitaji yake, inaunganishwa ipasavyo na inawasiliana kwa ufanisi, huku e-GA ikitoa utaalamu, viwango na huduma

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			za pamoja ili kupunguza kujirudia rudia kwa mifumo na gharama za uendeshaji; c) Serikali ihakikishe mifumo ya mapato, malipo, faini, leseni, miradi na mikataba inawezesha uthibitishaji wa miamala, usuluhishi wa kumbukumbu na ufuatiliaji wa mapato na matumizi kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma; d) Wakuu wa taasisi za Serikali wahakikishe kasoro za TEHAMA zilizobainishwa na ukaguzi zinarekebishwa kwa wakati kupitia mipango yenye hatua, muda wa utekelezaji na watendaji

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
			wanaowajibika, na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwa mamlaka husika; na e) Wizara yenye dhamana ya TEHAMA na e-GA, kwa kushirikiana na CAG na taasisi husika kulingana na majukumu yao, ziimarishe ufuatiliaji na tathmini ya mifumo ya TEHAMA ili kuhakikisha usalama, ufanisi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma na usimamizi wa rasilimali za umma.
14	Kuhusu Utata wa Kisheria na Kiutendaji Katika Usimamizi wa Mapato. Yasiyotokana na	hali hiyo inaweza kusababisha utata wa kisheria na kiutendaji, udhaifu katika usimamizi na udhibiti wa mapato, pamoja na changamoto katika uwajibikaji na ufuatiliaji wa mapato hayo.	Bunge linaazimia kwamba, ifikapo au kabla ya tarehe 30 Machi, 2027 NCAA, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), iweke utaratibu rasmi wa kisheria au Mkataba wa Makubaliano (MoU) unaobainisha wazi

NA.	HOJA	ATHARI YA HOJA HUSIKA	PENDEKEZO LA KAMATI
	Utalii na Mapato ya Uwekezaji wa NCAA.		majukumu ya kila upande katika ukusanyaji, utunzaji, uwasilishaji na usimamizi wa mapato hayo.
15	Kuhusu Kutokuwepo kwa Ulinganifu katika Ukokotoaji wa Mafao ya Pensheni kwa Wanachama Wanaounganisha Vipindi vya Michango.	hali hiyo inaweza kusababisha wanachama wenye mazingira yanayofanana kuhesabiwa mafao kwa misingi tofauti na hivyo kulipwa mafao yasiyoendana na stahili zao.	Serikali kupitia Wizara yenye dhamana na masuala ya kazi na pensheni, kwa kushirikiana na PSSSF na NSSF, itoe ufafanuzi rasmi kuhusu msingi sahihi wa kukokotoa malipo ya APE na kuhakikisha kuwa mafao yaliyokokotolewa kwa misingi inayotofautiana yanapitiwa na kurekebishwa pale itakapobainika kuwepo kwa malipo yaliyozidi au kuwa pungufu ya stahili za wanachama.Azimio hili likamilike kabla au ifikapo tarehe 30 Machi, 2027.

×